**RITA** yaanza kutoa mafunzo kuandika wosia

UKURASA 15



**SAMIA** apiga simu Njombe fidia Liganga, Mchuchuma

UKURASA 4

**ACT** yashtuka kushuka bei ya pamba

UKURASA 4



HOTUBA | Alhamisi Juni 8, 2023 | Nipashe 9

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO
MHE. DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB)
AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA 2023/24

MHE. DKT. MWIGULU L. NCHEMBA (MB) — WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO

DKT. NATU EL-MAAMRY MWAMBA — KATIBU MKUU WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

MHE. HAMAD HASSAN CHANDE (MB) — NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO

BI. JENIFA C. OMOLO — NAIBU KATIBU MKUU WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

BW. LAWRENCE N. MAFURU — NAIBU KATIBU MKUU WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

BI. AMINA KHAMIS SHABAAN — NAIBU KATIBU MKUU WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

UKURASA 9


# Nipashe

Alhamisi Juni 8, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581335

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Mwigulu ajipanga na trilioni 15/-

UKURASA 2, 9, 10, 11 NA 12



01 Leseni 11,880 michezo ya kubahatisha kutolewa

02 Ofisi ya Usuluhishi wa Kodi yaanzishwa

03 Wastaafu 49,407 waneemeka pensheni

04 Kampasi mpya za IFM Geita, Simiyu

05 Kusaka Tril. 40.8/- za kuendesha serikali

06 Sheria Msajili Hazina kufumuliwa



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya wizara hiyo, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kapteni JWTZ kizimbani mashtaka kudukua mifumo

UKURASA 2



Ofisa wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) kutoka Kikosi cha 603 KJ cha Anga Kituo cha Banana, Kapteni Exavery Mroso (kulia), akiongozwa na askari polisi baada ya kufikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam jana kwa tuhuma za kuingilia mfumo, kubadili neno la siri na kuwazuia viongozi kufanya kazi. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# TPA yatoa ufafanuzi ubinafsishaji wa bandari ulivyo

UKURASA 3

**MICHEZO** **FEI TOTO, AZAM KIMEELEWEKA** UK. 24

**KATUNI** UK. 6




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alipotembelea banda la Watumishi Housing Investments (WHI), katika maadhimisho ya miaka mitano ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, jijini Dodoma juzi. **PICHA: BEATRICE MOSES**

# Mwigulu ajipanga na Tril. 15/-

**Na Jenifer Gilla, DODOMA**

WAZIRI Dk. Mwigulu Nchemba amewasilisha bungeni makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka ujao wa fedha, akiomba Sh. trilioni 15.94 kuhudumia vipaumbele vyake vinane.

Katika uwasilishaji huo jana, kuna maboresho ya kiutendaji, yanayojumuisha kuanzishwa Ofisi ya Msuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi, hali kadhalika Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) kinaanzisha kampasi mpya katika mikoa ya Geita na Simiyu.

Ni hatua ya kiserikali kupitia wizara hiyo, kukiwapo timu inayoendelea na kazi nchini kutafuta migogoro ya kodi nchini, huku Rais naye ametanua wigo wa udhamini vyuoni kufikia ngazi ya diploma.

Kwa mujibu wa Waziri Mwigulu, vipaumbele vingine vinajumuisha mikakati ya kiserikali kutafuta na kukusanya Sh. trilioni 40.8 kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti ya serikali katika mwaka ujao wa fedha na kuhudumia deni la serikali.

Vipaumbele vingine ni kufanya utafiti, tathmini na mapitio ya kitaalamu kuhusu mifumo ya usimamizi wa mipango, uchumi na bajeti ya serikali; kujenga, kuboresha, kufungamanisha na kuhuisha mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ya usimamizi wa mapato na matumizi ya serikali.

Dk. Mwigulu pia alisema watajenga uwezo wa watumishi kuhusu usimamizi wa masuala ya sera, uchumi, mipango na fedha; kuboresha miundombinu ya ofisi za wizara na taasisi zake na miundombinu ya kufundishia na kujifunzia.

Kwa mwaka ujao wa fedha, wizara hiyo pia itafuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo inayotekelezwa na wizara na serikali kwa jumla na kukamilisha maboresho ya Sheria ya Msajili wa Hazina.

Dk. Mwigulu aliliomba Bunge kuidhinisha Sh. trilioni 15.94 kwa ajili ya matumizi ya wizara hiyo. Kati yake, Sh. trilioni 15.38 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. bilioni 564.22 ni kwa ajili ya maendeleo.

Pia aliliomba Bunge liidhinishe Sh. bilioni 97.13 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT). Kati yake, Sh. bilioni 87.72 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. bilioni 9.41 za utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Alibainisha kuwa vyuo vitano vilivyo chini ya Wizara ya Fedha ambavyo ni IFM, Taasisi ya Uhasibu Tanzania, Chuo cha Uhasibu Arusha, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, na Chuo cha Takwimu cha Mashariki mwa Afrika vinatarajia kudahili jumla ya wanafunzi 77,432 kwa ngazi ya cheti 14,108, stashahada 18,744, shahada 41,483 na uzamili 397.

Pia alisema Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inatarajia kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya jumla ya Sh. trilioni 26.7, kuimarisha na kuboresha mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato, kuwajengea uwezo wafanyakazi, kutoa elimu ya kodi na kuendelea kudhibiti uvujaji na upotevu wa mapato.

"Mwaka wa fedha 2023/24, Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imepanga kukuza wastani wa ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) kwa kiwango kisichopungua asilimia 10, ili kuendana na mahitaji ya shughuli za kiuchumi.

"Pia itaboresha mazingira ya kuchochea ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi, kudhibiti na kupunguza kiwango cha mikopo chechefu pamoja na kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosheleza mahitaji ya kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne," alisema.

Waziri huyo alisema Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania imepanga kuzalisha mapato ya Sh. bilioni 45.1 kukuza faida ya benki kabla ya kodi ya Sh. bilioni 18.5, kutoa mikopo ya Sh. bilioni 336.7, kukuza mali za benki ili kufikia Sh. bilioni 562.7 na kufuatilia urejeshaji wa mikopo kutoka kwa wateja Sh. bilioni 62.

Pia alisema Benki ya Maendeleo ya TIB imepanga kutoa mikopo ya Sh. bilioni 51 kwa miradi ya maendeleo katika sekta za maji, nishati na uongezaji thamani mazao ya kilimo, kukusanya Sh. bilioni 39.6 za marejesho ya mikopo kutoka kwa wateja, kukusanya Sh. bilioni 57 za marejesho ya mikopo iliyoshindikana na kuondolewa katika mizania ya benki.

**LESENI 11,880**

Waziri Mwigulu pia alisema kuwa katika mwaka 2023/24, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha inatarajia kutoa leseni 11,880 kwa waendesha michezo ya kubahatisha. Kati yake, 2,273 ni leseni mpya na 9,607 ni leseni zitakazohuishwa. Pia itafanya ukaguzi kwa waendesha michezo ya kubahatisha 101 na kusimamia uendeshaji wa Bahati Nasibu ya Taifa.

***SOMA HOTUBA UK. 9-12***

# Kapteni JWTZ kizimbani mashtaka kudukua mifumo

**Na Kulwa Mzee**

KAPTENI wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), Exavery Mroso (28) kutoka Kikosi cha Jeshi (603 KJ) cha Anga Kituo cha Banana, Dar es Salaam, amefikishwa mahakamani kwa madai ya kuingilia mfumo, kubadili neno la siri na kuwazuia viongozi kufanya kazi.

Mshtakiwa huyo alifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jana, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Rhoda Ndimilanga na kusomewa mashtaka na Wakili wa Serikali, Eric Davies.

Wakili Davies alidai kuwa mshtakiwa anakabiliwa na mashtaka matatu. Katika shtaka la kwanza, anadaiwa Februri 11, mwaka huu, akiwa ndani ya Jamhuri ya India, kwa makusudi aliingilia mfumo wa kompyuta akaunti ya Instagram yenye jina la MAMAKAJATZ kwa kubadili baruapepe ya mamajabackup@gmail.com kwenda kwa Xaviobiashara@gmail.com huku akijua kufanya hivyo ni kosa kisheria.

Katika shtaka la pili anadaiwa kuingilia mfumo wa data wa kompyuta ndani ya Jamhuri ya India. Anadaiwa aliingilia mfumo huo wenye jina la Hashim Ally Mubi, Jerson Brown na Steven Magombeka kwa kubadilisha neno la siri la akaunti ya Instagram kutoka mama2022 kwenda mamakaja 1321 huku akijua kufanya hivyo ni kosa la jinai.

Shtaka la tatu, mshtakiwa anatuhumiwa kwa kuzuia matumizi ya data ya kompyuta ikidaiwa kuwa tarehe hiyo hiyo katika Jamhuri ya India, alizuia data za kompyuta kwa kuwazuia viongozi wa utawala wa akaunti ya Instagram ya Mamajaztz, Hashim Ally Mubi, Jerson Brown na Steven Mgombeka kwa kubadilisha neno la siri la akaunti hiyo kutoka mama2022 kwenda Mamakaja 1321 huku akijua ni kosa.

Upande wa Jamhuri ulidai upelelezi wa shauri hilo haujakamilika. Mahakama ilikubali kumpa dhamana mshtakiwa kwa masharti ya kuwa na wadhamini wawili wenye kitambulisho cha taifa au cha mpigakura, wawe wakazi wa Dar es Salaam na kwamba , watatia saini dhamana ya maandishi ya Sh. milioni tano.

Mshtakiwa alipata dhamana na kesi imeahirishwa hadi Juni 26, mwaka huu.



# TPA yatoa ufafanuzi ubinafsishaji bandari

**Na Restuta James**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), imewaondoa hofu wananchi kutokana na azimio la Bunge kuhusu Bandari ya Dar es Salaam, ikibainisha kuwa ushirikiano baina ya Tanzania na Dubai, unalenga kuongeza ufanisi.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Plasduce Mbossa, ilisema kuwa ushirikiano huo unalenga kuongeza ajira, kufungua fursa za kiuchumi na kijamii kupitia uwekezaji kwenye baadhi ya maeneo ya Bandari ya Dar es Salaam.

Taarifa hiyo ilifafanua kuwa maeneo mengine yatakayoboreshwa kupitia ushirikiano huo ni maeneo huru ya kiuchumi na viwanda, kwa kujenga viwanda na uwekezaji kwenye mnyororo wa usafirishaji.

"Azimio la Bunge linalohusu mkataba ambao serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaingia na serikali ya Dubai wenye ukomo wa miezi 12 ni kwa ajili ya kutoa nafasi ambayo serikali hizo mbili kushirikiana katika uboreshaji wa tasnia ya bandari nchini Tanzania.

"Jitihada zote na hatua zilizochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita katika kuvutia uwekezaji hususani kwenye maeneo ya bandari zinalenga kumaliza changamoto za muda mrefu ikiwamo ucheleweshwaji wa meli, mizigo na kukosekana ufanisi katika bandari zetu," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Aidha, taarifa ilisema Azimio la Bunge linahusu mkataba kati ya Tanzania na Dubai wenye ukomo wa miezi 12 kwa ajili ya kutoa nafasi kwa serikali hizo kuona maeneo ya ushirikiano ili kuboresha bandari.

TPA ilitoa ufafanuzi huo baada ya kuibuka mjadala kwenye mitandao ya kijamii, wananchi na wanasiasa kukosoa ushirikiano kati ya mamlaka hiyo na kampuni ya DP World inayomilikiwa na serikali ya Dubai.

Mbali ya TPA, Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, aliitisha mkutano wa Clubhouse kwenye mtandao wa Twitter, jana usiku. Mkutano wa Msigwa uliwakutanisha wadau muhimu akiwamo Mbossa waliotoa ufafanuzi wa ushirikiano huo.

Jumatatu wiki hii Bunge lilipokea mapendekezo ya serikali za Tanzania na Dubai, kushirikiana kiuchumi na kijamii kwa ajili ya uendelezaji na uboreshaji wa utendaji kazi katika Bandari ya Tanzania.

## Rais afanya mabadiliko ma-DED, Ma-DAS

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameteua na kuhamisha wakurugenzi 184 wa mamlaka za serikali za mitaa na makatibu tawala wa wilaya 139, miongoni mwao yakiwamo majina maarufu.

Baadhi ya wateule hao ni Ruth Magufuli anayekuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Morogoro, Pendo Ndumbaro Katibu Mkuu Wilaya ya Mbinga, Fatima Kubenea Katibu Tawala Wilaya ya Masasi na Geofrey Nnauye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Newala.

Wakurugenzi wa Halmashauri wengine walioteuliwa na vituo vyao kwenye mabano ni Abdul Mtaka (Rorya), Omary Nkullo (Kongwa), Nuru Kindamba (Ileje), Zahara Michuzi (Geita) na Justice Kijazi (Ikungi) ambaye hajawahi kuhamishwa kituo cha kazi tangu ateuliwe mwaka 2016.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Katibu Mkuu Kiongozi, Dk. Moses Kusiluka, wengine walioteuliwa na Rais Samia ni Theresia Mtewele anayekuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Kasulu ambaye ni mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM.

**ALIYETUMBULIWA ARUDISHWA**

Taarifa hiyo imewataja makatibu tawala wa wilaya wengine ni Mtella Mwampamba (Songea) ambaye wakati wa awamu ya tano alitumbuliwa akiwa kwenye nafasi hiyo Wilaya ya Kisarawe, Abdallah Mtulia (Kakonko), James Mkumbo (Uvinza), Neema Mfugale (Uyui), Pendo Mahalu (Kigamboni), Hassan Mkwawa (Ubungo) na Rahma Kondo (Longido).

Wakurugenzi walioachwa katika vituo vyao vya kazi ni Saitoti Zelothe (Wilaya ya Handeni) na Spora Liana anayebaki katika Halmashauri ya Jiji la Tanga. Katika uteuzi huo, Aron Kagurumjuli aliyewahi kuwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni, ameteuliwa tena kuwa Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza.

**MAKATIBU TAWALA WILAYA**

Makatibu tawala wengine ni Charangwa Makwiro (Ilala), Stella Msofe (Kinondoni), Nicodemus Mwikozi (Temeke), Sara Ngalingasi (Bahi), Michael Maganga (Mpwapwa), Augustino Chazua (Chemba), Neema Nyalenge (Chamwino), Sozi Ngate (Kongwa), Christina Kalekezi (Kondoa) na Sakina Mbugi (Dodoma).

Wengine ni Khamana Simba (Arusha), Muhsin Kassim (Monduli), Joseph Mabiti (Arumeru), Faraja Msigwa (Karatu), Nyakia Chirukile (Ngorongoro), Rahma Kondo (Longido), Sospeter Magonera (Hai), Johari Athumani (Rombo), Upendo Wella (Same), Rukia Zubery (Mwanga) na Shaaban Mchomvu (Moshi).

**WAKURUGENZI**

Baadhi ya wakurugenzi ni Selemani Msumi (Arusha), Juma Seph (Jiji Arusha), Hanifa Hamza (Kinondoni), Michael Gwimile (Rufiji), Elias Ntiruhungwa (Ubungo), Elihuruma Mabelya (Temeke), Erasto Kiwale (Kigamboni), Jomary Satura (Jiji Dar es Salaam).

Wengine ni John Kayombo (Jiji Dodoma), Semistatus Mashimba (Chamwino), Zaina Mlawa (Bahi), Omary Nkullo (Kongwa), Mwanahamis Ally (Mpwapwa), Siwema Jumaa (Chemba), Shaban Millao (Kondoa), Rashid Gembe (Manispaa ya Moshi), Dionis Nyinga (Hai), Anastazia Ruhamvya (Same), Mwajuma Nasombe (Mwanga), Shadrack Mhagama (Moshi) na Haji Mnasi (Moshi).

Pia wamo John Nchimbi (Jiji Mbeya), Stephen Katemba (Mbeya), Misana Kwangura (Mbarali), Renatus Mchau (Rungwe) na Tamim Kambona (Chunya).

**LHRC NA 50/50**

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga, alisema mabadiliko hayo yamefuata sheria ingawa bado suala la asilimia 50/50 halijafikiwa.

Alisema katika mabadiliko hayo wanawake ni 46 sawa na asilimia 33 na wanaume ni 93 sawa na asilimia 66.7.


## ARM SOLUTION AUCTION MART AND PROPERTY MANAGEMENT CO LTD

## MNADA WA HADHARA

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA **MuCoBa Bank Plc** TUNAWATANGAZIA WANANCHI WOTE KUWA KUANZIA TAREHE **22-06-2023 NA KUENDELEA** TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI ZA WADAIWA HAPO CHINI ILI KUFIDIA MADENI WANAYODAIWA.

| NO | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | TAWI ALILOKOPA | DHAMANA | MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA/ MUDA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | CHARLES MASHITA | CHARLES MASHITA | MAFINGA | NYUMBA | MTAA WA IHONGOLE – MAFINGA | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 2. | EDSON KILAMLYA | EDSON KILAMLYA | IRINGA | NYUMBA NA KIWANJA | IPOGORO - IRINGA | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 3. | EMMANUEL R WISSO | EMMANUEL R WISSO | MAFINGA | NYUMBA | MTAA WA BALALI-MAFINGA | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 4. | REUBEN MWAKASALA | REUBEN MWAKASALA | MAFINGA | NYUMBA | MTAA WA IHONGOLE – MAFINGA | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 5. | ROBERT PAULO KISEO | ALEX NCHEMWA | IRINGA | NYUMBA | KIJIJI CHA ITUNUNDU - PAWAGA | NA KUENDELEA KUANZA SAA O3 ASUBUHI |
| 6. | CYNTHIA MTUI | KIGUNGA MWANGWA | IRINGA | KIWANJA | MTAA WA MTWIVILA "B" | NA KUENDELEA KUANZA SAA O3 ASUBUHI |
| 7. | GODFREY MHAGAMA | GODFREY MHAGAMA | MAFINGA | NYUMBA | MJI MWEMA MAFINGA | NA KUENDELEA KUANZA SAA O3 ASUBUHI |
| 8. | GAI GAMBA | GAI GAMBA | MAFINGA | NYUMBA | CHANGARAWE | NA KUENDELEA KUANZA SAA O3 ASUBUHI |
| 9. | NGOTI GREEN HILL ESTATE COMPANY (THOMAS NGOTI) | THOMAS NGOTI | IRINGA | NYUMBA | IRINGA MJNI | NA KUENDELEA KUANZA SAA O3 ASUBUHI |
| 10. | GASTON RUGUGA NTAMAKILILO | GASTON RUGUGA NTAMAKILILO | MAFINGA | NYUMBA NA SHAMBA LA MITI | LUNGEMBA NA MAKAMBAKO | NA KUENDELEA KUANZA SAA O3 ASUBUHI |
| 11. | DICKSON MASASI | SAMWELI MASASI | MAFINGA | KIWANJA | MAKALALA | NA KUENDELEA KUANZA SAA O3 ASUBUHI |
| 12. | STEWART MAGIRI | STEWART MAGIRI | MAFINGA | NYUMBA | SAWALA-MUFINDI | NA KUENDELEA KUANZA SAA O3 ASUBUHI |
| 13. | LUKAS LEVIS MSINGWA | LIKAS LEVIS MSINGWA | MAFINGA | NYUMBA | MAFINGA BLOCK J | NA KUENDELEA KUANZA SAA O3 ASUBUHI |
| 14. | FABIAN GODFREY YERINDE | FABIAN GODFREY YERINDE | MAFINGA | NYUMBA | IHONGOLE | NA KUENDELEA KUANZA SAA O3 ASUBUHI |
| 15. | ALBERT DOMINIKUSY SANGA | ALBERT DOMINIKUSY SANGA | MAFINGA | PAGALE | NDOLEZI | NA KUENDELEA KUANZA SAA O3 ASUBUHI |
| 16. | VIOLETH MHAPA | ISSAYA CUPPUSWAMY | MAFINGA | NYUMBA | IGOWOLE | NA KUENDELEA KUANZA SAA O3 ASUBUHI |
| 17. | TUMAIN ISACK MWIKE | TUMAIN ISACK MWIKE | MAFINGA | NYUMBA | MALINGUMU | NA KUENDELEA KUANZA SAA O3 ASUBUHI |
| 18. | GODWIN DITRICK MHESI | GODWIN DITRICK MHESI | MAFINGA | NYUMBA | BALALI | NA KUENDELEA KUANZA SAA O3 ASUBUHI |
| 19. | IDDI RASHID KAONEKA | IDDI RASHID KAONEKA | MAFINGA | GHALA | GANGILONGA | NA KUENDELEA KUANZA SAA O3 ASUBUHI |
| 20. | VAILETH GEORGE HAULE | VAILETH GEORGE HAULE | MAFINGA | NYUMBA | MAKWAWA-RUNGEMBA | NA KUENDELEA KUANZA SAA O3 ASUBUHI |
| 21. | RENATUS JOSHUA LWEGANWA | RENATUS JOSHUA LWEGANWA | MAFINGA | KIWANJA | IVAMBINUNGU | NA KUENDELEA KUANZA SAA O3 ASUBUHI |
| 22. | FILBERT YOVENARY KALINGA | FILBERT YOVENARY KALINGA | MAFINGA | NYUMBA | BALALI | NA KUENDELEA KUANZA SAA O3 ASUBUHI |
| 23. | MOHAMED SELEMAN KINYOGOLI | MOHAMED SELEMAN KINYOGOLI | MAFINGA | NYUMBA | MTAA WA MGODI | NA KUENDELEA KUANZA SAA O3 ASUBUHI |
| 24. | MARY NGELULA | MARY NGELULA | MAFINGA | NYUMBA | IVAMBINUNGU | NA KUENDELEA KUANZA SAA O3 ASUBUHI |
| 25. | MUFINDI INSTITUTE OF AGRICULTURE | GETRO MSAFIRI CHULA | MAFINGA | MAJENGO YA CHUO NA ENEO EKA 12 | NDOLEZI | NA KUENDELEA KUANZA SAA O3 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA**

MSHINDI ATATAKIWA KULIPA ASILIMIA (25%) AU ZAIDI BAADA YA NYUNDO YA DALALI NA BAKI (75%) ITALIPWA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE (14), TOFAUTI NA HAPO MSHINDI ATAPOTEZA HAKI ZAKE NA MNADA UTARUDIWA UPYA.

**MAWASILIANO: 0757 -107 715, 0784 -759 892**

# Samia apiga simu Njombe fidia Liganga, Mchuchuma

**Na Elizabeth John, NJOMBE**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameahidi kuanza mara moja kwa mradi wa Liganga na Mchuchuma pindi tu ulipaji wa fidia zaidi ya Sh. bilioni 15.4 kwa wananchi 1,142 wilayani Ludewa mkoani Njombe ukikamilika.

Alitoa ahadi hiyo jana alipozungumza kwa simu na wananchi wa Wilaya ya Ludewa kupitia Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka. Rais alipiga simu wakati wa uzinduzi wa ulipaji fidia.

Rais Samia alisema:"Nimefurahi leo (jana) kwamba timu ya serikali iko hapo kwa ajili ya kukamisha ile ahadi yetu. Mnakumbuka nilipopita kufanya kampeni nikiwa Makamu wa Rais niliahidi tutakuja kulipa fidia na mradi uanze sasa. Leo ni furaha yangu na faraja kwamba timu ya serikali iko hapo kwa ajili ya kulipa fidia.

"Ninataka niwaahidi fidia zote zitalipwa na kama kutakuwa wataalamu wamekosea, kuna watu wameachwa tutaliangalia lakini tuna hakika tunalipa fidia ambayo tulishaifanyia kazi vizuri.

"Ahadi yetu kwenu baada ya kulipa fidia mradi sasa utaendelea. Mchuchuma na Liganga sasa utakwenda kuchangamka, ajira zitakwenda kupatikana, kodi kwa halmashauri zitakwenda kupatikana kutokana na mradi kuwapo. Kwa hiyo, niwaombe wananchi tushirikiane katika utekelezaji. Katika malipo kila mtu achukue anachostahiki halafu kwa vyema tuje kushirikiana kwenye mradi," alisema Rais Samia.

Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Dk. Ashatu Kijaji, alisema wizara sasa inaanza kwa kasi kubwa kutekeleza mradi wa madini hayo baada ya serikali kuwalipa wananchi fedha zao.

"Sisi sasa kama watendaji ndani ya wizara hii tuko tayari kukimbia na wawekezaji, ili mradi wetu huu uanze kutekelezwa. Mradi huu wa Liganga na Mchuchuma ni mradi ambao una historia ndefu na ya muda mrefu.

"Ni mradi unaojumuisha uchimbaji wa chuma cha Liganga na pamoja na makaa ya mawe ya Mchuchuma ambapo kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na serikali, mradi huu una umuhimu mkubwa kwa ajili ya kukuza uchumi wa nchi yetu.

"Tumesikia kwa pamoja miaka 56 ijayo bado tutaendekea kunufaika na mradi huu, tunafahamu kabisa ni mradi wa kipekee zaidi duniani, hutoupata eneo lolote ndani ya ulimwengu huu zaidi ya Tanzania na sifa yake moja kubwa tunazo rasilimali zote mbili zimewekwa kwa pamoja zinazotegemeana, tunayo makaa, lakini tunacho chuma ambapo bila ya makaa chuma huwezi kukiongeza thamani," alisema.

Dk. Kijaji alisema serikali inatamani kuona miradi mikubwa ya kimkakati nchini, inatekelezwa kwa kutumia chuma cha ndani.

"Chuma tulichokitengeneza wenyewe kutoka Liganga na Mchuchuma na hivyo kuiwezesha nchi kuwa na fedha za kigeni za kutosha kwani hatutonunua tena chuma na nondo kutoka nje ya nchi yetu.

"Kwa hili nikuombe katibu mkuu ile taarifa yetu ya kunileteа kila mwezi muda wake umeisha, ninaomba sasa kila wiki taarifa ya majadiliano yenu wapi mmefika ili tuhitimishe na tuweze kunufaika na mchango huu," aliagiza.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), Dk. Nicolaus Shombe, alisema kuwa hadi usiku wa Juni 6 mwaka huu, watu 39 walikuwa wameshalipwa fedha zao za fidia.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka alisisitiza wanufaika wa fidia hizo kuwa makini na kutofanya udanganyifu kutokana na malalamiko ya fidia za kipindi cha nyuma zilizofanywa na serikali.

Mtaka alisema kuwa uhakiki unaendelea kwa majina 77 kati ya 1,142 ambayo taarifa zake hazijakamilika.

Mmoja wa wanufaika wa fidia hiyo, Fesi Mhagama, alimshukuru Rais Samia kwa kuruhusu kulipwa fidia kwa sababu jambo hilo lilikuwa la muda mrefu. Wapo waliofariki dunia wakisubiri fidia.



Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji (katikati) na Mkuu wa mkoa wa Njombe, Antony Mtaka (kushoto), wakikabidhi mkataba kwa mmoja wa wanufaika wa fidia wa kwanza ili kupisha mradi wa Liganga na Mchuchuma, wilayani Ludewa jana. **PICHA: ELIZABETH JOHN**

## ACT-Wazalendo yashtuka kushuka kwa bei ya pamba

**Na Julieth Mkireri, BUSEGA**

CHAMA cha ACT Wazalendo kimeelezea kusikitishwa na kuporomoka kwa bei ya pamba katika msimu huu wa kilimo hadi kufikia Sh. 1,060 kutoka sh. 2,000-2,600 kwa kilo.

Kimesema hali hiyo imesababisha wakulima wengi kupata hasara kutokana na uzalishaji wa zao hilo kuwa na gharama kubwa, hasa katika pembejeo.

Mjumbe wa Kamati Kuu ya chama hicho, Ishaka Mchinjita alieleza masikitiko yao alipohutubia wananchi mjini Busega jana katika mkutano wa hadhara uliofanyika Kijiji cha Nyamikoma.

Mchinjita alisema wakulima wamekuwa wakikopeshwa dawa za kuzuia wadudu waharibifu lakini hawajui thamani ya dawa hizo huku makato yakifanyika bila kushirikishwa.

"Mathalani katika bei ya pamba msimu huu ni Sh. 1,060. Hapo imeshakatwa bei ya dawa. Kwa hiyo, wakulima hawajui dawa ni kiasi gani," alisema.

Waziri Kivuli wa Fedha wa chama hicho, Emmanuel Mvula, alizungumzia uhaba wa ajira kwa vijana nchini, akiutaja umechangia vijana wengi kuchagua kufanya shughuli za kufanya biashara ndogo.

Mvula alieleza kuwa mbali na kuweka mazingira mazuri ya biashara, kunahitajika mpango wa kuongeza nguvukazi iliyopo nje ya mfumo wa uzalishaji ambao utatoa mbadala kuliko umachinga.

"Kwa sasa nguvu kazi ya watanzania (miaka 15-64) ni milioni 33, waliopo katika soko la ajira ni milioni 25.8. Zaidi ya milioni 2.3 hawana ajira kabisa, wakati watu zaidi ya milioni 20 wanajiajiri na wapo katika sekta isiyo rasmi. Walioajiriwa katika sekta rasmi ni wastani wa watu milioni tatu," alisema.

Mvula alieleza kuwa kila mwaka nguvu kazi inayoingia katika soko la ajira ni takribani watu 800,000. Ajira zinazozalishwa katika sekta mbalimbali huwa ni wastani wa 137,000 kila mwaka huku ikiacha watu husussani vijana zaidi ya 653,000 nje ya mfumo wa uzalishaji na kuwafanya vijana wengi kuishi katika hali ya utegemezi.

"ACT Wazalendo itachukua hatua katika kutengeneza ajira zenye heshima kuhakikisha ajira zinazotokana na viwanda zinaongezeka kutoka 300,000 za sasa hadi kufikia 900,000 ndani ya miaka mitano ya uongozi wake," aliahidi.

Alisema jambo hilo litawezekana kwa kuanzisha maeneo maalum ya viwanda na biashara katika kanda saba za kusini juu, kusini kati, kaskazini, magharibi, Kanda ya Ziwa na Kanda ya Kati ili kuongeza ajira kwa vijana kupitia viwanda vyenye uwezo wa kuajiri watu wasiopungua 20,000 kila kimoja.

## Sarakasi zaendelea CWT

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

SARAKASI zimeendelea kutawala kwenye Chama cha Walimu Tanzania (CWT), baada ya Kamati tendaji Taifa kuazimia kumsimamisha Katibu Mkuu wa chama hicho, Japhet Maganga, kujihusisha na shughuli zote za chama kutokana na kutuhumiwa kuendesha kinyume na Katiba.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, Mwenyekiti wa muda wa kamati hiyo, Mwalimu Thobias Sanga, alisema kikao cha kamati hiyo kimeridhia kwa pamoja kumzuia kiongozi huyo.

Alisema baadhi ya tuhuma ambazo wanamtuhumu katibu huyo ni pamoja na vitendo vya uvunjaji wa Katiba, ikiwemo kufanya uhamisho holela wa wafanyakazi, matumizi ya fedha yasiyo shirikisha wajumbe wa kamati tendaji, kuajiri watumishi bila kuzingatia utaratibu pamoja na kutoa zabuni za fulana za walimu kinyume na miongozo.

"Tumejiridhisha na tumeona utendaji kazi wa katibu huyu hauko sawa tumepitia miongozo yetu tumejiridhisha tunachukizwa kuona fedha za asilimia mbili za walimu zinatumika bila utaratibu tukihoji hatupewi ushirikiano.

"Kwa mamlaka tuliyonayo tumekubaliana shughuli zote zinazohusu chama chetu cha walimu zitafanywa na Naibu Katibu Mkuu ambaye atasimamia masuala yote ya utawala na fedha, naomba nieleweke wazi kuwa hatuna shida na katibu mkuu ila tunachotaka ni mfumo wa utendaji tunataka walimu tunao wawakilisha wapate haki zao na siyo unyanyasaji unaoendelea,"alisema

Naibu Katibu Mkuu wa CWT Taifa, Joseph Msalaba, ambaye ndiye amepewa mamlaka ya utendaji wa shughuli zote za chama, alisema kuwa amelipokea suala hilo na kueleza kuwa kikao hicho kimefanyika kwa amani kama ilivyotarajiwa.

"Nimepokea uwepo wa ujio wa wajumbe hawa 18 wa kamati ya utendaji taifa kati ya 32, lakini hakuna kilicho haribika,"alisema.

Mwalimu Sabina Lipukila mwakilishi wa walimu mkoa wa Ruvuma, alisema mgogoro uliopo unasababisha utendaji kazi wa chama hicho kushuka na Katiba yao haiendi wanavyotaka.

Alisema uhamisho wa makatibu wa mikoa hivi sasa unafanywa kiholela bila wao kushirikishwa jambo ambalo linashusha ari ya kufanya kazi kwa weledi kutokana na hofu ya uhamisho.

"Hakuna asiyefahamu kuwa sisi ni chombo cha ajira kuna vitu vingi tunavifuatilia haviendi sawa kwa muda mrefu sasa tumekuwa tunaomba kikao lakini tumenyimwa tungekubaliwa vikao haya yote tungezungumza na kuyamaliza kwenye vikao tusingefika hapa,"alisisitiza.

Mwanasheria wa Chama hicho, Paschal Msafiri akitolea ufafanuzi suala hilo alisema kuwa wenye mamlaka ya kuitisha vikao vya dharura ni Rais au Katibu Mkuu.

# GIZ yawekeza bil. 7/- kukabili ukatili dhidi ya makundi maalum

**Na Enock Charles**

SERIKALI imetia saini mkataba wa miaka mitatu wenye thamani ya Sh. bilioni 7.5 na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ), kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa haki kwa wanawake, watoto na kupambana na ukatili wa kijinsia kwa makundi hayo.

Akitia saini mkataba huo, Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Mary Makondo, alisema bado kuna viashiria vya kuwapo ukatili wa kijinsia nchini licha ya juhudi mbalimbali zilizofanyika kwa vipindi tofauti kupambana na tatizo hilo na kwamba mkataba huo umefikiwa kwa wakati sahihi.

"Wanawake wanatakiwa kujua haki zao namna ya kuzipata na mahali pa kuzipata pale ambapo zimevunjwa kupata msaada wa kisheria. Mradi huu utaenda sambamba na kampeni yetu Wizara ya Katiba na Sheria ya Huduma ya Msaada wa Kisheria kupitia sheria ya mwaka 2017 ambayo ilianza utekelezaji mwaka 2018 yenye jina la Rais wetu 'Mama Samia Legal Aid Campaign,'" alisema.

Makondo alisema bado wanawake katika maeneo mbalimbali nchini wanabaguliwa na kunyimwa haki ya kumiliki mali katika familia au hata kupata mirathi pale wenzi wao wanapofariki dunia, hivyo mkataba huo pamoja na mambo mengine utawezesha wanawake kupata msaada wa kisheria, ili kuzifikia haki zao zilizoporwa kwa nguvu na wanaume.

Alisema mkataba huo utawezesha kupatikana kwa haki ambazo zimekuwa zikivunjwa kwa baadhi ya watoto kukumbwa na madhila ya ubakaji na ulawiti wakati mwingine kupitia kwa ndugu wa karibu kama vile mjomba, baba mdogo, kaka au binamu.

"Liko tatizo katika mila na desturi katika baadhi ya jamii zetu ambapo unyanyasaji unapotokea basi wao wanamalizana kindugu, wanasema usimseme huyu ni kaka yako, huyu ni mjomba wako ngoja tuyamalize, unakuta pengine aliyefanya ni baba mdogo, baba mzazi anamshambulia mama kwamba usiseme utavunja ukoo.

"Lakini ule ukatili utamwathiri maisha yake yote. Kama ni mwanafunzi hawezi kusoma vizuri pia huwezi kujua kama pengine ameathirika kwa magonjwa, kama vile Ukimwi na mengine ya ngono. Pia anabaki na stigma ya kujikataa kwa hiyo bado tunatakiwa kutoa elimu hasa kwa maeneo ya vijijini ambapo yapo matukio mengi," alisema.

Balozi wa Ujerumani nchini Tanzania, Regine Hess, alisema amefurahishwa na juhudi mbalimbali zinazofanywa na serikali ya Tanzania katika kupambana na ukatili wa kijinsia kupitia mikakati mbalimbali.

Alisema mkataba wa nchi yake kwa kushirikiana na serikali ya Tanzania unalenga kuongeza nguvu katika mapambano hayo.

Katika hatua za utekelezaji, alisema inahitajika kujitolea kwa nguvu zote badala ya kuishia kuzungumza bila utekelezaji na pia kuna haja ya kushirikisha wadau na ikibidi kufanya mabadiliko ya sheria pale inapobainika zipo zenye vikwazo katika mapambano hayo.

Alisema Ubalozi wa Ujerumani umekuwa makini katika suala hilo na kuonyesha juhudi za dhati tangu mwaka 2020 walipoanza kushirikiana na serikali.




Rebeca Mushi mkazi wa Kisongo jijini Arusha, akinunua simu kwa njia ya mkopo alipotembelea banda la Tigo, kwenye maonyesho ya Kili Fair yaliyofanyika viwanja vya Magereza mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Kiwanda kimea kutoa maelfu ajira wakulima wa shayiri

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

UFUFUAJI wa kiwanda cha kusindika kimea (Malt) mkoani Kilimanjaro uko katika hatua nzuri na kitaanza kufanya kazi Machi, 2024 huku kikitarajia kutoa ajira 17,500 za wakulima wa shayiri.

Uwekezaji huo unafanywa na Kampuni ya Bia Tanzania (TBL) na unatarajia kufikia gharama ya Sh. bilioni 90 na utashusha neema kwa wakulima wa zao hilo.

Akizungumza kwenye uzinduzi wa uwekezaji wa kiwanda hicho unaoshirikisha Wizara tatu, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema hatua hiyo ni ukombozi wa wakulima wa zao hilo ambao kwa muda mrefu lilikosa soko kutokana na kutokuwapo na mtambo wa kusindika kimea.

"Kampuni za pombe zinaagiza kimea kutoka nje hivyo usindikaji huu utakapoanza mwezi Machi 2024 utakuwa ni neema kwa wakulima wa mikoa ya Kilimanjaro, Manyara, Rukwa na Mbeya,"alisema.

Alisema kiwanda kitasindika kimea tani 12,000 na inatarajiwa kufikia tani 35,000 baada ya miaka miwili ijayo na kutoa ajira hizo za wakulima.

"Kwa hiyo hatua hii itasaidia yale mashamba yaliyokuwa yamelala kuanza kuzalisha shayiri na wakulima watakuwa na uhakika wa kuzalisha na kuuza zaidi tani 20,000 za shayiri ambayo inatumika kutengenezea malt (kimea),"alisema.

Alisema kutakuwa na usimamizi wa bei ili usiumize mkulima na mwekezaji na mikataba itakuwa ya wazi kati ya wakulima wa zao hilo na kampuni hiyo.

"Mjadala wa kwa nini zao hili linaagizwa kutoka nje badala ya kufufua kiwanda hicho ulianza mwaka 2019/20, niwahakikishie wizara itahakikisha inasimamia mikataba na kuwa na usimamizi mzuri wa bei," alisema.

Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Baishara, Exaud Kigahe, alisema wizara itahakikisha inaendelea kushirikiana na wawekezaji wa viwanda ili watumie malighafi za kilimo hapa nchini.

Mkurugenzi wa Uendeshaji wa TBL, Richmond Raymond, alisema kiwanda hicho kitawezesha serikali kupata mapato ya Sh.Bilioni 226 na kitanunua shayiri moja kwa moja kutoka kwa wakulima.

Alisema awali wataanza na uwekezaji wa Sh.Bilioni 42 wa mitambo kwenye kiwanda hicho na wanatarajia kuongeza na kufikia Sh.Bilioni 90.

# EPZA kuhudumia wawekezaji popote kupitia mfumo mpya

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya nje (EPZA), imetengeneza mfumo mpya utakaowahudumia wawekezaji bila kujali sehemu waliyopo na kuondoa ulazima wa kufika ofisini kufuata huduma.

Mfumo huo unaoitwa EPZA Business Facilitation Portal (BFP) utamwezesha mwekezaji kupata taarifa na taratibu za uwekezaji kutoka kwenye mamlaka wakiwa mahali popote na kuzijaza.

Mkurugenzi Mkuu wa EPZA, Charles Itembe, alisema mafanikio hayo ya kutengeneza mfumo huo ni sehemu ya uungaji mkono juhudi zinazofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan katika kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji nchini na kuifanya Tanzania kuwa chaguo la kwanza na sahihi kwa wawekezaji kuja kuwekeza.

"Tunampongeza sana Rais Samia kwa juhudi kubwa ya kuzitangaza fursa za uwekezaji nchini na kuendelea kuweka mazingira wezeshi ambayo yamepunguza kwa kiasi kikubwa gharama za ufanyaji biashara nchini," alisema.

Itembe alisema mfumo huo ambao umetengenezwa na EPZA kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, dhumuni lake ni kuhudumia wawekezaji bila kujali wako sehemu gani na kuondoa ulazima mwekezaji kufuata huduma ofisini.

Alisema mfumo huo utafanya kazi nyingi zikiwamo kuandikisha mwekezaji, kampuni, kupata vibali vya ujenzi na kuhifadhi taarifa zake.

Alisema utaunganisha EPZA na wawekezaji pamoja na taasisi kama Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Uhamiaji, TBS na taasisi nyingine zinazohudumia wawekezaji nchini.

Alisema mfumo huu utamwezesha mwekezaji kufanya maombi ya leseni na vibali vingine bila kutembelea ofisi za mamlaka ya EPZA.

"Kupitia mfumo huu ambao umetengenezwa na wataalamu wa ndani, utamwezesha mwekezaji kupata habari zote muhimu kuhusu uwekezaji na pia unampa fursa ya kuchagua namna bora ya kujaza taarifa zake kwenye mfumo huo," alisisitiza.

Kwa upande wa maombi ya leseni alisema mamlaka ya EPZA inatoa aina mbili za leseni ambazo ni ya Eneo Maalum la Uwekezaji (EPZ) na (SEZ).

Alisema kupita mfumo huo, taarifa za mwekezaji huwekwa sehemu moja na kuwa rahisi kwake kuongeza vitu vipya au kuzirekebisha.

Itembe alisema mfumo huo ulianza kutengenezwa na wataalamu wa ndani mwaka mmoja na nusu uliopita na mwezi Julai, mwaka huu EPZA inatarajia kuuzindua rasmi uanze kutumiwa na wawekezaji.

Mfumo huo utawahudumia wawekezaji kupata huduma EPZA na pia utatengeneza taarifa muhimu zinazohusu wawekezaji kwa ajili ya taasisi nyingine za umma.

Alisema EPZA ilifanya mafunzo ya kwanza mkoani Dodoma na wawekezaji takribani 50 walishiriki na kupata mafunzo ya mfumo huo.

Akiongea kwa niaba ya wawekezaji wengine, mwakilishi wa kiwanda cha kuchakata nyama cha TanChoice, Kibaha mkoani Pwani, alisema utapunguza muda uliokuwa unatumika kupata huduma EPZA na kupunguza gharama za uendeshaji.

"Hii itaongeza uwezo wetu wa kushindana sokoni na kupunguza gharama za uzalishaji," alisema.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Watanzania kuandika wosia ni kuiondolea familia matatizo

**UAMUZI** wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), kuanzisha huduma ya kutoa mafunzo ya uandishi na utunzaji wa wosia, utasaidia kuelimisha wananchi wengi ambao wanahofia kufanya hivyo kwa kudhani kuwa wanajichulia kifo.

Mafunzo yanayotolewa na RITA yatasaidia kupunguza tatizo la migogoro ya familia itokanayo na ndugu wa marehemu kugombania mali na wakati mwingine kusababisha mauaji.

Migogoro mingi imeshuhudiwa katika jamii hasa mmoja wa wanandoa anapofariki, ndugu kuanzisha vurugu za kugombea mali na kusababisha chuki isiyokwisha na hata kupelekana mahakamani.

RITA imeanzisha huduma ya ushauri, kuandika na kuhifadhi wosia baada ya kubaini kuongezeka kwa tatizo la wajane na watoto kupoteza mali za marehemu ambaye hakuacha wosia.

Baadhi ya watoto hushindwa kuendelea na masomo na familia kushindwa kupata mahitaji muhimu kutokana na kudhulumiwa haki yao.

Wakala huo unaeleza umuhimu wa Watanzania kujenga tabia ya kuandika wosia wanapokuwa hai ili kuwaondolea shida wategemezi wao inapotokea anaondoka duniani.

RITA inaeleza umuhimu wa kuandika wosia mtu anapokuwa hai ili kuwasaidia watoto wao kupata haki zao na kuepuka matukio mengi ya familia kupoteza haki zao kutokana na ndugu kupokonya mali za wajane na watoto wa marehemu.

Pia Watanzania wanatakiwa kuondokana na imani potofu kuwa mtu akiandika wosia anajitabiria kifo badala yake watumie fursa hiyo kwa ajili ya manufaa ya familia zao kupata kile wanacho stahili wakati wanapokuwa hawapo duniani kwa sababu mtoa wosia ana nafasi ya kufanya marekebisho kila mara anapohitaji.

Faida za kuandika wosia ni kuepusha watoto au mke/mume kunyang'anywa mali na kumwezesha mwandishi kumchagua msimamizi wa mirathi.

Wosia unaepusha migogoro katika familia ndugu au jamaa, unampa uhakika wa maisha bora ya baadaye ya warithi wake kulingana na mali alizonazo, kupunguza usumbufu na gharama wakati wa kuendesha mirathi.

Kadhalika, taarifa zinazopaswa kuandikwa kwenye wosia ni pamoja na msimamizi wa mirathi, wapi mtoa wosia angependa azikwe, idadi ya mali za marehemu na mgawanyo wa mali za marehemu.

Wosia kwa mujibu wa RITA upo wa aina mbili. Upo wosia wa maandishi na wosia wa matamshi/mdomo na anayetakiwa kuandika wosia ni mwananchi yeyote awe na umri wa miaka 18 na kuendelea, awe na akili timamu, wosia uwe wa maandishi au matamishi, ushuhudiwe na watu wanne ukiwa ni wa matamshi, wosia usimnyime mrithi halali wa mali bila sababu zinazotambulika kisheria na uwe umeshuhudiwa na mwanasheria.

RITA imeanzisha mfumo wa kutoa huduma kidijitali unaofahamika kama eRITA ambao unamwezesha mtu yeyote kupata huduma sehemu yoyote kwa kutumia simu yake ya mkononi.


Mfumo huo unamwezesha mwananchi kupata huduma ya cheti cha kuzaliwa, kifo pamoja na udhamini kupitia simu yake ya mkononi na anaweza kupata cheti chake katika ofisi yoyote ya RITA iliyopo jirani yake.

Kitu cha muhimu cha kuzingatia ni Watanzania tuache imani potofu kuwa kuandika wosia maana yake unajitabiria kifo chako karibuni.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




# Muungwana Lazima Nilonge

## Sasa kazi ni moja kwetu, wote tuwe wapiganaji magonjwa yasiyoambukiza



Na Yasmine Protace

**HADI** sasa elimu imepamba moto kuhusu vita kwa maradhi yasiyo ya kuambukiza, watu wakielimishwa namna ya kuyakabili, maana yanaonekana kama yamesahaulika.

Ni kweli elimu, inapaswa izidi kutolewa kwa jamii, itoe hatua ya kuimudu kusaidia na wakati huohuo, iendelee kujikinga na magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Kimsingi, unapotaja magonjwa yasiyoambukiza, yamekuwa yakishika kasi kila mwaka na kuibua athari mbalimbali, kupigana na aina ya ugonjwa husika, kusababisha madhara kama vile
ulemavu wa kudumu na wengine wanapoteza maisha.

Namna ya kukabiliana na magonjwa hayo, inaelezwa jamii inatakiwa izidi kupatiwa elimu sahihi katika namna ya kupambana nayo.

Msingi wa magonjwa yasiyoambukizwa, kuna baadhi yanayotokana na ulaji ambao haujapangiliwa na kutofanya mazoezi ya mwili, baada ya kumaliza mlo.

Ili jamii iepuke magonjwa hayo, inatakiwa kuzingatia mfumo wa ulaji na kujenga utamaduni wa kufanya mazoezi kila wakati.

Hivi karibuni, Naibu Waziri wa Afya Dk.Godwin Mollel amesema kuwa, kwa mwaka wa fedha 2022-2023, serikali kupitia Wizara ya Afya imetenga zaidi ya shilingi milioni 725 kwa ajili ya kutekeleza Mpangomkakati wa Tatu wa Kitaifa wa Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza nchini.

Ni kauli ya Naibu Waziri Daktari Mollel, wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalumu Bernabetha Kasabago Mushashu, katika kikao kinachoendelea Bunge la jijini Dodoma.

"Katika mwaka wa fedha 2022-2023, serikali imetenga zaidi ya shilingi milioni 725 kwa ajili ya kutekeleza Mpango Mkakati wa Tatu wa Kitaifa wa Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza 2021-2026 nchini, huku mikakati mahususi ya udhibiti visababishi vya magonjwa hayo yasiyoambukiza," anasema

Ni ufafanuzi anaoongeza na kuwa serikali imeweka mikakati thabiti ya kupambana na magonjwa yasiyoambukiza, ikiwamo kuimarisha ushirikishwaji wa sekta mtambuka, kuimarisha miundombinu ya utoaji huduma, kuwajengea uwezo watumishi, ili kupambana dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza.

Vilevile anataja haja ya kuimarisha na kusimamia shughuli za utafiti na kutoa elimu kwa wananchi, juu ya njia za kujikinga dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza.

Anaongeza kuwa serikali kupitia Wizara ya Afya, imeendelea kutoa elimu ya njia za kujikinga dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza, ikiwamo kuhamasisha wananchi kufanya mazoezi, kuzingatia kanuni bora za lishe, kupunguza unywaji pombe uliopitiliza na matumizi ya mafuta mengi kwenye vyakula.

Anasema serikali iliyoko madarakani imeweka fedha nyingi kupambana na magonjwa yasiyoambukiza, ikiwamo eneo la manunuzi ya vifaa tiba akitumia mfano wa kifaa 'CT-Scan' katika kila Hospitali ya Rufani ya Mkoa, pamoja na kutia saini mikakati kwa wakuu wa mikoa wote, kuhusu masuala ya lishe kwenye kila mkoa.

Anaongeza kuwa mkakati mwingine wa mapambano dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza, ni kuunga mkono kwa Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote, pindi utapoletwa bungeni, ili kumpa haki kila mwananchi kupata matibabu bila malipo kuanzia ngazi ya Zahanati hadi Hospitali ya Taifa Muhimbili.

"Serikali kupitia Wizara ya Afya imeendelea kuongeza kasi kwenye eneo la upatikanaji wa dawa katika Zahanati na Vituo vya Afya, idadi ya dawa, vifaa na vifaa tiba ngazi ya Zahanati imeongezeka kutoka aina 254 mwaka 2015 hadi kufikia aina 451 mwaka 2023, huku ngazi ya Kituo cha Afya ikiongezeka kutoka aina 414 mwaka 2015 hadi kufikia aina 828 mwaka 2023," anasema.

## Kesi mauaji mfanyakazi GGML yapigwa kalenda

**Na Joctan Ngelly, GEITA**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita imeahirisha kesi ya mauaji namba 12/2023 inayowakabili washtakiwa sita wanaotuhumiwa kuhusika na mauaji ya aliyekuwa mfanyakazi wa Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) Milembe Hungwe, baada ya upande wa mashtaka kudai upelelezi haujakamilika.

Washtakiwa hao waliofikishwa mahakamani ni: Dayfath Maunga (30), mkazi wa Usagara; Safari Lubingo (54), mkazi wa Chigunga; Geja Pastory (30), mkazi wa Bugarama; Mussa Fundikila (37), mkazi wa Goba; Mussa Pastory (33), mkazi wa Bulyanhulu na Sesilian Macheni (55), mkazi wa Kalebezo.

Washtakiwa hao wote kwa pamoja walifikishwa kizimbani mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama hiyo, Johari Kijuwile na walisomewa mashtaka hayo, hawakutakiwa kujibu chochote kutokana na mahakama hiyo kutokuwa na uwezo wa kusikiliza kesi ya mauaji kisheria.

Upande wa Mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Venance Mkonongo, alidai mahakamani kuwa upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya kutajwa.

Hakimu Mkazi Mwandamizi Kijuwile alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Juni 21, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa.

Alisema washtakiwa wote kwa pamoja watapelekwa mahabusu katika Gereza la Wilaya ya Geita kutokana na kesi inayowakabili kutokuwa na dhamana.

Awali akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali, Scolastica Teffe alidai kuwa Aprili 26, mwaka huu, katika maeneo ya Mwatulole mkoani Geita, washtakiwa wote kwa pamoja walimuua aliyekuwa mfanyakazi wa GGML, Milembe Hungwe kwa kumcharanga mapanga sehemu mbali mbali za mwili wake na kufariki dunia papo hapo, kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.

**Upande wa Mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Venance Mkonongo, alidai mahakamani kuwa upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya kutajwa.**




Mkurugenzi wa Bodi ya Chai Tanzania, Mary Kipeja (kushoto) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Tanzania Mercantile Exchange Plc, Godfrey Malekano, wakionyesha miongozo ya makubaliano ya mnada wa chai, wakati wa uzinduzi wa mnada wa mwaka 2023 jijini Dar es Salaam juzi. Mnada huo, unatarajiwa kuanza Juni 26, mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwili watambuliwa ajali iliyoua watano, dereva azidi kusakwa

**Na Idda Mushi, MOROGORO**

MWILI wa mtu mmoja kati ya watano waliofariki dunia katika ajali ya basi dogo la abiria aina ya Coaster eneo la Iyovi barabara kuu ya Morogoro-Iringa, umetambuliwa na ndugu na taratibu za kusafirisha kwa ajili ya maziko zinaendelea.

Dereva aliyesababisha ajali hiyo ambayo pia ilisababisha watu 20 kujeruhiwa, hajajisalimisha kwa Jeshi la Polisi.

Mwili wa marehemu uliotambuliwa ni wa Modest Mkude (30), mfanyabiashara na mkazi wa Mbeya ambaye alikuwa akisafiri kuelekea jijini Dar es Salaam kwa shughuli zake na kiasili anatokea Kisaki mkoani Morogoro.

Kaimu Mganga Mkuu wa Hospitali ya St. Kizito Mikumi, Dk. Stephen Mbilinyi, akizungumza kwa njia ya simu, alisema jana kuwa Mkude alikuwa anasafiri pamoja na mama yake mzazi, wakitoka Mbeya na mama yake ilikuwa ashukie mjini Morogoro.

Kuhusu hali za majeruhi tisa waliolazwa hospitalini huko, Dk. Mbilinyi alisema wanaendelea na mtibabu na baadhi yao wameomba waende kupata huduma jirani na maeneo wanayoishi ili iwe rahisi kupata huduma toka kwa ndugu zao.

Kuhusu mgonjwa mmoja aliyehamishiwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, Kaimu Ofisa Uhusiano wa Hospitali hiyo, Scolastica Ndungu, alisema majeruhi huyo anaendelea vizuri na matibabu.

Alisema majeruhi huyo ametambuliwa kuwa ni Said Hani (50).

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Alex Mkama, alisema wanaendelea kumsaka dereva wa gari hilo aliyekimbia baada ya ajali na kumtaka kujisalimisha mara moja.

Ajali hiyo ilitokea asubuhi ya Jumatatu Mei 5, mwaka huu, baada ya dereva huyo kujaribu kuyapita magari mengine yaliyokuwa mbele yake katika kona na milima na kugongwa ubavuni na lori la mafuta wakati akikwepa ajali ya kugongana uso kwa uso. Watu watano walipoteza maisha papo hapo na 20 kujeruhiwa.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# TIB yapongezwa gharama nafuu katika mikopo kilimo

**Na Seleman Mpochi**

BENKI ya Maendeleo (TIB) imepongezwa kwa kutoa mikopo ya gharama nafuu katika sekta ya kilimo kwa wakulima na wawekezaji.

Mikopo ya benki hiyo imekuwa ikielekezwa hasa kwa wakopaji wanaojihusisha na shughuli za uzalishaji na usindikaji wa mazao ya kilimo nchini.

Pongezi hizo zilitolewa jana na Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Conrad Millinga aliyemwakilisha Waziri wa Viwanda wakati wa Maonyesho ya 10 ya Biashara na Utalii Tanga katika Viwanja vya Mwahako jijini Tanga.

Millinga alionyeshwa kufurahishwa na huduma za mikopo inayotolewa na TIB kupitia Dirisha la Kilimo ambalo linawalenga wakulima na wawekezaji wenye miradi ya kilimo na ufugaji ambao wana uzoefu na wanajihusisha na shughuli za kilimo nchini.

"Ninawapongeza kwa kusaidia wakulima nchini kwa kutoa mikopo yenye gharama nafuu ambayo inawezesha Watanzania wengi zaidi kuwekeza zaidi na kukuza biashara zao," alisema.

Akiwa banda hilo, Millinga alijulishwa kuwa riba inayotozwa kupitia kwa mikopo hiyo ni kiwango cha asilimia tano kwa mwaka kwa wakopaji wa moja kwa moja toka benki.

Kupitia dirisha hilo, taasisi zinazokopa kwa ajili ya kukopesha (on-lenders) zinatozwa asilimia nne kwa mwaka ambapo zitatakiwa kukopesha kwa asilimia isiyozidi nane kwa wakulima/wateja wao.

TIB imekuwa ikitoa mikopo kupitia Dirisha la Kilimo ambayo kipindi cha marejesho ni kati ya miezi sita hadi miaka 15 kwa kutegemea aina ya mradi wa kilimo pamoja na makadirio ya hesabu (financial projections).

Mikopo hiyo huwa na kipindi cha rehema (grace period) ambacho hutolewa kulingana na kipindi cha kukomaa kwa mazao husika na makadirio ya mtiririko wa fedha (projected cash flow).

Kipindi cha juu cha rehema ni miaka tatu kwa mazao ya muda mrefu na mwaka mmoja kwa mazao ya muda mfupi.

Wakati huo, TIB imeibuka Mshindi kwa Upande wa Taasisi za Fedha zilizoshiriki Maonyesho ya 10 ya Biashara na Utalii Mkoa wa Tanga ikifuatiwa na Benki ya NMB na Mfuko wa SELF (SELF Microfinance Fund). Na ilifanikiwa kushika nafasi ya tatu kwenye Taasisi za Bima/Bima-Benki zilizoshiriki maonyesho hayo.

Maonyesho ya 10 ya Biashara na Utalii Mkoa wa Tanga yalianza Mei 28 na kufikia tamati Juni 6, mwaka huu yakiwa na kaulimbiu ya 'Kilimo, Viwanda, Utalii na Madini Ndio Msingi wa Maendeleo ya Kiuchumi.

TIB ni taasisi ya serikali iliyoanzishwa kwa malengo ya kuwezesha upatikanaji wa mitaji ya muda mrefu na wa kati kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi nchini.




Wafanyakazi wa Benki ya Maendeleo TIB, wakionyesha ngao ya ushindi kwa upande wa Taasisi za Fedha zilizoshiriki maonyesho ya 10 ya biashara na utalii jijini Tanga juzi, yaliyokuwa na kauli mbiu: "Kilimo, Viwanda, Utalii na Madini ndio msingi wa Maendeleo ya Kiuchumi". Kutoka (kushoto) ni Giusy Mbolile, Saidi Mkabakuli na Alex Mbambaga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Migodi yahamasisha jamii kupanda miti

**Na Mwandishi Wetu, TARIME**

MIGODI ya Barrick North Mara na Bulyanhulu iliyoko halmashauri za wilaya ya Tarime na Msalala katika mikoa ya Shinyanga na Mara, imeadhimisha Siku ya Mazingira Duniani mwaka huu kwa wafanyakazi wake kushiriki kupanda miti ya matunda na kivuli, kuhamasisha jamii kupanda miti na kufanya usafi katika vitongoji jirani.

Katika maadhimisho hayo, Mgodi wa Barrick North Mara umetoa msaada wa miche ya miti ya matunda na kivuli ipatayo 200 na kushirikiana na jamii kuipanda katika Shule ya Sekondari Matongo wilayani Tarime.

Akizungumza wakati wa upandaji wa miti hiyo, Meneja Mazingira wa mgodi huo, Frank Ngoloma, alisema wameelekeza shughuli hiyo katika shule hiyo mpya ili kuiboreshea uoto wa asili na mazingira kwa ujumla.

"Tumeamua kushirikiana na jamii kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani kwa kupanda miti. Tumeanzia ndani ya mgodi ambapo wafanyakazi wa kila idara wameshirikiana na viongozi wao kupanda miti na hii inaonyesha uwajibikaji wa mgodi katika kulinda mazingira," alisema.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Matongo, Lackson Isibhu, aliupongeza mgodi huo kwa kuthamini maadhimisho hayo na kuona umuhimu wa kushirikiana na jamii kupanda miti ili kulinda mazingira.

Kaimu Maneja Uhusiano ya Jamii na Mazingira wa Mgodi wa Barrick Bulyanhulu, Respicius Onesmo, alisema wameamua kuungana na Halmashauri ya Msalala kuhakikisha wanatoa elimu ya utunzaji wa mazingira kwa jamii na mgodi utafadhili kazi ya kufanya usafi katika maeneo ya vijiji na vitongoji vinavyozunguka mgodi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Msalala, Charles Fusi, aliipongeza Barrick Bulyanhulu, kwa kuunga mkono jitihada za serikali za kuhamasisha utunzaji wa mazingira na alitoa wito kwa wananchi kuzingatia utunzaji wa mazingira na kuepuka kuzalisha taka za plastiki ambazo mbali na kuharibu mazingira unasababisha madhara mbalimbali ya kiafya.

# Wakaguzi wapewa angalizo ukaguzi mifumo TEHAMA

**Na Romana Mallya**

MKURUGENZI Mkuu wa Ndani Msaidizi Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali, Paison Mwamnyasi, amewataka wakaguzi wa ndani kuzingatia sheria, kanuni, viwango na miongozo ya serikali mtandao wanapofanya ukaguzi katika miradi na mifumo ya TEHAMA ili kutoa ushauri wenye tija serikalini kupitia taarifa zao za ukaguzi.

Alielekeza hayo wakati wa ufunguzi wa awamu ya pili ya mafunzo maalum kwa wakaguzi wa ndani kutoka Mamlaka 13 za Serikali za Mitaa yaliyofanyika mkoani Morogoro juzi.

Alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa wakaguzi wa ndani kwa kuwa yanawajenga uwezo katika utendaji kazi na kurahisisha shughuli za ukaguzi na kutoa ushauri wenye tija kwa serikali.

"Ukielewa namna mifumo inavyofanya kazi, unaweza kukagua ipasavyo na tutaepuka kutaja majina ya watu katika taarifa zetu za ukaguzi badala ya mifumo.

"Sisi wakaguzi tunatambua kuwa miongozo ya ukaguzi inaeleza kutokagua sehemu ambayo hauna uelewa nayo kwa kuwa unaweza kutoa maoni na ushauri kwa serikali ambao hauna tija," alisema.

Mkurugenzi wa Udhibiti wa Usalama wa TEHAMA Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Sylvani Shayo, aliwasisitiza wakaguzi wa ndani kutumia sheria, kanuni, viwango na miongozo ya serikali mtandao wakati wa kusimamia na kufanya ukaguzi wa miradi na mifumo ya TEHAMA katika taasisi zao.

Alisema e-GA kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wanaendelea na jitihada za kutoa mafunzo kwa kundi hilo ili kufanya ukaguzi kwa ufanisi.

"Ikiwa wakaguzi wa ndani mtazingatia vyema miongozo na sheria hizo mtafanya ukaguzi wenye tija na maslahi kwa taifa," alisema.

Meneja wa Udhibiti wa Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao, Sultana Seiff, alisema e-GA haitaki kuacha kada yoyote nyuma katika matumizi ya TEHAMA kwa kuwa dunia ya sasa inaendeshwa kidijitali.

Alisema wakaguzi wa ndani wanapewa mafunzo hayo ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na kuboresha utoaji wa huduma za serikali kwa njia ya kidijitali.

Mafunzo hayo ya siku tano yanayofanyika mkoani Morogoro yalianza Juni 5, mwaka huu, yakihusisha wakaguzi wa ndani 110 kutoka halmashauri na za mikoa ya Dodoma, Tabora, Singida, Kigoma, Mara, Dar es Salaam, Morogoro, Shinyanga, Rukwa, Kagera, Geita, Simiyu na Katavi.

Awamu ya kwanza ya mafunzo hayo ilikuwa mwezi Machi mwaka huu, wakaguzi wa ndani 133 kutoka halmashauri za mikoa 13 za Tanzania Bara walishiriki.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

# HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO MHE. DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA 2023/24



**MHE. DKT. MWIGULU L. NCHEMBA (MB)**
WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO



**DKT. NATU EL-MAAMRY MWAMBA**
KATIBU MKUU WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO



**MHE. HAMAD HASSAN CHANDE (MB)**
NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO



**BI. JENIFA C. OMOLO**
NAIBU KATIBU MKUU
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO



**BW. LAWRENCE N. MAFURU**
NAIBU KATIBU MKUU
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO



**BI. AMINA KHAMIS SHABAAN**
NAIBU KATIBU MKUU
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

JAMHURI YA MUUNGANO WATANZANIA

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

# HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO, MHESHIMIWA DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA 2023/24

**1.0 Utangulizi**

1. Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mhe. Daniel Baran Sillo – Mbunge wa Babati Vijijini, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2022/23 na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu tisa (9) ya Wizara ya Fedha na Mipango, pamoja na Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2023/24.

2. Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wake, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia uzima na afya njema, na kutupa wasaa wa kukutana kwa mara nyingine kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2022/23 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2023/24.

3. Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuniamini na kunipa fursa ya kuendelea kusimamia majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango. Kwa mara nyingine, napenda kumhakikishia kuwa nitaendelea kutumikia kwa weledi dhamana aliyonipa ya kusimamia masuala ya uchumi, bajeti, fedha na mipango ya Taifa letu. Ni dhahiri kwamba, katika kipindi cha uongozi wake, nchi yetu imepata mafanikio makubwa kiuchumi, kijamii na kisiasa ambayo kila mmoja wetu anapaswa kujivunia na kumuunga mkono. Mwenyezi Mungu aendelee kumjalia afya njema, hekima na busara katika kubadilisha fikra na mifumo ya usimamizi wa maslahi ya wananchi wakiwemo wafanyakazi, wawekezaji, wafanyabiashara, wakulima, wafugaji na wadau wa maendeleo.

4. Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii adhimu, kumpongeza Mheshimiwa Angellah Jasmine Mbelwa Kairuki kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kuteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninawapongeza kwa dhati ya moyo wangu, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge Viti Maalumu na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa kuchaguliwa kuwa wenyeviti wa Bunge lako Tukufu. Ninawaahidi ushirikiano thabiti katika utekelezaji wa majukumu yao ya kukusaidia wewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika katika kuongoza vikao vya Bunge.

5. Mheshimiwa Spika, kwa minajili ya tukio la leo, naomba kutoa pongezi zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, chini ya Mwenyekiti wake, Mhe. Daniel Baran Sillo – Mbunge wa Babati Vijijini pamoja na Makamu Mwenyekiti, Mhe. Omari Mohamed Kigua - Mbunge wa Kilindi kwa maoni na ushauri wenye tija katika kuboresha usimamizi wa majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2023/24. Kwa niaba ya wizara na taasisi zake, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa tutaendelea kufanya kazi kwa pamoja ili kutoa huduma stahiki kwa wananchi waliotupa dhamana ya kusimamia masuala ya kisera katika Taifa letu.

6. Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo ya utangulizi, naomba nijielekeze moja kwa moja kwenye hoja iliyo mbele yetu. Hoja yangu imegawanyika katika maeneo makuu manne (4) ambayo ni: Muhtasari kuhusu majukumu ya Wizara; mwenendo wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/23; vipaumbele vya wizara na taasisi zake kwa mwaka 2023/24; na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2023/24.

**2.0 Majukumu ya Wizara**

7. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa tangazo la Serikali Na. 534 la Julai 2, 2021, Wizara ya Fedha na Mipango imekasimiwa majukumu yafuatayo:
   i. Kusimamia sera za uchumi jumla, fedha, ununuzi wa umma na ubia kati ya sekta ya umma na binafsi:
   ii. Kusimamia mipango, mikakati na miongozo ya kitaifa ya maendeleo;
   iii. Kusimamia bajeti ya Serikali;
   iv. Kuratibu upatikanaji wa fedha kutoka taasisi za fedha za kikanda na kimataifa kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali;
   v. Kudhibiti utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi;
   vi. Kusimamia matumizi ya fedha na mali za umma;
   vii. Kusimamizi mifumo ya uendeshaji wa mashirika na taasisi za umma pamoja na vitega uchumi vya Serikali;
   viii. Kusimamia masuala ya fedha ya pamoja kati ya Tanzania Bara na Zanzibar;
   ix. Kusimamia mafao, pensheni na mirathi kwa wastaafu wasio wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii;
   x. Kusimamia deni la Serikali;
   xi. Kusimamia mifumo ya udhibiti wa michezo ya kubahatisha;
   xii. Kusimamia maendeleo ya sekta ya fedha; na
   xiii. Kusimamia takwimu rasmi za kitaifa.

**3.0 Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/23**

8. Mheshimiwa Spika, wakati nawasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2022/23, niliomba Bunge lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi trilioni 14.94 kwa mafungu tisa (9) kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa Wizara na taasisi zake. Vipaumbele vya matumizi ya kawaida kwa Wizara tunavyoendelea kutekeleza ni:
   i. Kukusanya, kutafuta na kudhibiti mapato na matumizi ya Serikali;
   ii. Kuhudumia deni la Serikali kwa wakati pindi linapoiva;
   iii. Kufanya tathmini ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 kwa ajili ya maandalizi ya Dira Mpya ya Taifa ya Maendeleo 2050;
   iv. Kufanya tathmini ya mfumo na muundo wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo ili kuwezesha kutungwa kwa Sera ya Taifa ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo;
   v. Kufanya tafiti katika sekta za uzalishaji ili kuibua fursa za uwekezaji, uwezeshaji na vyanzo vya mapato ya Serikali katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu;
   vi. Kuendelea kutekeleza maagizo ya Serikali ya kutafsiri sheria za Wizara na taasisi zake kwa lugha ya Kiswahili; na
   vii. Kuhuisha Mwongozo wa Taifa wa Usimamizi wa Viashiria Hatarishi.

9. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi ya maendeleo, Wizara inaendelea kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:
   i. Kuimarisha mifumo ya usimamizi wa fedha za umma kupitia Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma Awamu ya Sita (PFMRP VI);
   ii. Kuandaa na kujenga ghala la takwimu (Data warehouse);
   iii. Kuratibu na kusimamia zoezi la Sensa ya Watu na Makazi;
   iv. Kuziwezesha taasisi za Wizara, hususan taasisi za elimu na mafunzo kuboresha miundombinu ya kujifunzia na kufundishia;
   v. Kuendelea na ujenzi wa jengo la Wizara katika Mji wa Magufuli, Mtumba Dodoma;
   vi. Kujenga na kukarabati Ofisi za Wizara katika mkoa wa Geita, Njombe, Songwe, Dar es Salaam, Morogoro, Kigoma na Ruvuma.

**3.1 Mwenendo wa Matumizi hadi Aprili 2023**

10. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, mafungu tisa (9) ya Wizara ya Fedha na Mipango yaliidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi trilioni 14.94 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 13.62 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 1.32 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Matumizi ya kawaida yanajumuisha shilingi trilioni 12.61 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi trilioni 1.01 kwa ajili ya matumizi ya mishahara. Aidha, matumizi ya maendeleo yanajumuisha shilingi trilioni 1.28 fedha za ndani na shilingi bilioni 36.51 fedha za nje.

11. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2023, fedha zilizopokelewa kwa mafungu yote tisa (9) ya wizara ni shilingi trilioni 11.75 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo, sawa na asilimia 78.61 ya makadirio ya mwaka. Matumizi halisi yalifikia shilingi trilioni 11.62, sawa na asilimia 98.95 ya fedha zilizopokelewa. Kati ya kiasi hicho, matumizi mengineyo yalikuwa shilingi trilioni 10.07, mishahara shilingi bilioni 438.95 na maendeleo shilingi trilioni 1.12 Mchanganuo wa fedha zilizotumika kwa kila Fungu ni kama inavyoonekana katika kiambatisho Na.1 – 3.

12. Mheshimiwa Spika, Fungu 45, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi lilipata ridhaa ya Bunge lako Tukufu ya kutumia jumla ya shilingi bilioni 89 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake. Hadi Aprili 2023, Ofisi imepokea jumla ya shilingi bilioni 76.42, sawa na asilimia 85 ya makisio ya mwaka 2022/23. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 12.66 zimepokelewa kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 60.59 matumizi mengineyo na shilingi bilioni 3.17 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Aidha, matumizi halisi ya mishahara yalifikia shilingi bilioni 12.66 matumizi mengineyo shilingi bilioni 57.85 na maendeleo shilingi bilioni 3.17.

**3.2 Mwenendo wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara**

3.2.1 Kukusanya, kutafuta na kudhibiti mapato na matumizi ya Serikali

13. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Wizara ya Fedha na Mipango ilikadiriwa kutafuta na kukusanya jumla ya shilingi trilioni 38.0. Kati ya kiasi hicho, Fungu 7 – Ofisi ya Msajili wa Hazina lilikadiriwa kukusanya shilingi bilioni 988.3, Fungu 21 – Hazina shilingi trilioni 37.0, Fungu 23 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali shilingi bilioni 60.1 na Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango shilingi bilioni 1.0. Aidha, kati ya kiasi kilichokadiriwa kukusanywa na Fungu 21, shilingi trilioni 23.6 ni mapato ya ndani ya kodi na yasiyo ya kodi yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania, shilingi trilioni 4.6 ni misaada na mikopo yenye masharti nafuu na shilingi trilioni 8.8 ni mikopo yenye masharti ya kibiashara ikiwemo hatifungani za Serikali.

14. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2023, wizara imefanikiwa kutafuta na kukusanya jumla ya shilingi trilioni 30.24, sawa na asilimia 81.5 ya makadirio ya mwaka 2022/23. Kati ya kiasi hicho, Fungu 7 – Ofisi ya Msajili wa Hazina limekusanya shilingi bilioni 704.2, Fungu 21 – Hazina shilingi trilioni 29.37, Fungu 23 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali shilingi bilioni 1.2 na Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango shilingi milioni 439.83 Aidha, kati ya kiasi kilichokusanywa na Fungu 21, shilingi trilioni 18.8 ni mapato ya ndani ya kodi na yasiyo ya kodi yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania, shilingi trilioni 4.61 ni misaada na mikopo yenye masharti nafuu na shilingi trilioni 5.96 ni mikopo yenye masharti ya kibiashara ikiwemo hatifungani za Serikali.

15. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2023, wizara imechukua hatua mbalimbali ili kudhibiti mapato na matumizi ya Serikali pamoja na mali za umma. Hatua hizo ni pamoja na: kuimarisha doria kwenye mipaka yote nchini ili kudhibiti ukwepaji kodi na biashara za magendo; kuendelea kuboresha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA (EFDMS, TANCIS, ITAX) ili kudhibiti uvujaji na upotevu wa mapato; kuendelea na kampeni mbalimbali za kutoa elimu kwa mlipakodi kupitia semina, makongamano na vyombo vya habari ili kuongeza uelewa na uhiari wa kulipa kodi; na kuendelea kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji wa vyanzo vya mapato yasiyo ya kodi.

16. Mheshimiwa Spika, hatua nyingine zilizochukuliwa na wizara kudhibiti mapato na matumizi ya fedha za umma ni pamoja na kuunganisha Mfumo wa MUSE na kuanza kutumika katika Ofisi za Balozi 11 ambazo ni Ubalozi wa Tanzania Lagos - Nigeria; New York - Marekani; Ottawa-Canada; Riyadhi - Saudi Arabia; Muscat - Oman; Seoul-Korea Kusini; Kuwait - Kuwait; Kuala Lumpur - Malaysia; Washington - Marekani; na Brasilia - Brazil; kuboresha Mwongozo wa Ukaguzi wa Ndani; kuandaa Mpango Mahsusi wa Ukaguzi; kuhakiki madeni ya chakula kwa shule za msingi na sekondari katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 45; kuhakiki mikopo inayotolewa na Serikali kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu; kuhakiki madeni ya ununuzi wa pamba msimu wa mwaka 2019/20 pamoja na madeni ya watoa huduma ya pembejeo; kuhakiki fedha za ujenzi wa soko la kisasa katika Manispaa ya Morogoro na deni la mshauri elekezi wa Shirika la Reli; kufanya ukaguzi wa Mfumo wa Mapato wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro; kuhakiki madeni ya Soko la Kariakoo; kuhakiki madeni ya wazabuni wa vifaa kwenye mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Uhuru, Jengo la utawala na Kituo cha Afya Mlowa katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino; kuhakiki taarifa za malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa umma na wastaafu; na kuhuisha kumbukumbu za mali za taasisi 537 zenye thamani ya shilingi trilioni 68.891 kwenye Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali.

3.2.2 Kuhudumia deni la Serikali

17. Mheshimiwa Spika, kupitia Fungu namba 001, Bunge lako Tukufu liliidhinisha jumla ya shilingi trilioni 9.1 kwa ajili ya kuhudumia deni la Serikali pindi linapoiva. Hadi Aprili 2023, wizara imelipa kwa wakati notisi za madai ya deni lililoiva la jumla ya shilingi trilioni 7.4, sawa na ufanisi wa asilimia 82 ya lengo. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani ni shilingi trilioni 4.4, ikijumuisha riba shilingi trilioni 1.7 na mtaji shilingi trilioni 2.7. Aidha, deni la nje ni shilingi trilioni 3, ikijumuisha riba shilingi trilioni 0.8 na mtaji shilingi trilioni 2.2.

3.2.3 Kufanya tathmini ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na maandalizi ya Dira 2050

18. Mheshimiwa Spika, wizara imekamilisha taratibu za ununuzi wa mtaalamu elekezi kwa ajili ya tathmini ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, ambapo mtaalamu elekezi amewasilisha taarifa ya awali Aprili 2023 na anatarajiwa kukamilisha tathmini husika ifikapo Agosti 2023. Sambamba na zoezi la tathmini ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, wizara inaendelea na taratibu za maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ambapo mchakato rasmi ulizinduliwa Aprili 2023. Aidha, warsha elekezi kwa wajumbe wa timu za uandishi na uhariri wa dira ilifanyika Mei 2023 Jijini Dar es salaam. Kipekee, napenda kumpongeza kwa dhati ya moyo wangu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwongozo wake thabiti ambao umetuwezesha kuanza kwa wakati maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

3.2.4 Kufanya tathmini ya mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo

19. Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu liliridhia mapendekezo ya Wizara ya kufanya tathmini ya mfumo na muundo wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo ili kubaini kama kuna uhitaji wa kuandaa Sera ya Taifa ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi na Programu za Maendeleo. Hadi Aprili 2023, wizara imefanikiwa kukusanya maoni na mapendekezo kutoka Wizara za kisekta, taasisi na mashirika ya umma, Bunge, vyuo vikuu na vyuo vya kati, taasisi za utafiti na washirika wa maendeleo. Kazi inayoendelea kwa sasa ni kufanya uchambuzi na kuandaa mapendekezo kulingana na maoni ya wadau pamoja na miongozo ya maandalizi ya nyaraka za Serikali.

3.2.5 Kufanya tafiti ili kuibua fursa za uwekezaji, uwezeshaji na vyanzo vya mapato ya Serikali

20. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Wizara ya Fedha na Mipango ilipata ridhaa ya Bunge ya kufanya tafiti mbalimbali ili kuibua fursa za uwekezaji, uwezeshaji na vyanzo vya mapato ya Serikali. Napenda kutoa taarifa kuwa hadi Aprili 2023, wizara imekamilisha tafiti mbili (2) ambazo ni upatikanaji wa huduma ndogo za fedha na mchango wake katika ukuaji wa shughuli za kiuchumi na matokeo yake katika kupunguza kiwango cha umaskini kwa makundi maalumu pamoja na utafiti kuhusu ufanisi katika ukusanyaji wa Kodi ya Ongezeko la Thamani.

21. Mheshimiwa Spika, pamoja na tafiti zilizokamilika, wizara ipo katika hatua mbalimbali kukamilisha tafiti zifuatazo: Utafiti kuhusu mnyororo wa huduma za utalii nchini; upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya maendeleo; mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya ardhi; na utafiti kuhusu uchumi wa kidijitali na matokeo yake katika matumizi ya fedha taslimu katika ununuzi wa bidhaa na huduma. Vilevile, wizara imefanyia kazi mapendekezo ya wadau kuhusu maboresho ya mfumo wa kodi ambayo hayakuridhiwa na Serikali katika mwaka 2022/23, tathmini ya ufanisi wa misamaha ya kodi katika uchumi na mfumo wa upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Matokeo ya tafiti na tathmini zilizofanyika yatatumika kuboresha mazingira ya uwekezaji, biashara na mifumo ya usimamizi wa mipango, mapato na matumizi ya Serikali.

3.2.6 Utekelezaji wa agizo la Serikali la kutafsiri sheria za Wizara na taasisi zake kwa lugha ya Kiswahili

22. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Bunge lako Tukufu liliridhia mpango wa Wizara wa kuendelea kutafsiri sheria zake kwa lugha ya Kiswahili. Hadi Aprili 2023, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanikiwa kutafsiri sheria saba (7) ambazo ni Sheria ya Ongezeko la Thamani, Sura 148, Sheria ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu, Sura 286, Sheria ya PPP, Sura 103, Sheria ya Usimamizi ya Ushuru wa Forodha, Sura 147, Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura 197, Sheria ya Usajili na Uhamishaji wa Umiliki wa Magari, Sura 124 na Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134.

3.2.7 Kuhuisha Mwongozo wa Taifa wa Usimamizi wa Viashiria Hatarishi

23. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, wizara ilipanga kuhuisha miongozo ya usimamizi wa vihatarishi na udhibiti wa ndani ili kuimarisha mifumo ya usimamizi wa vihatarishi katika sekta ya umma. Hadi Aprili 2023, wizara imefanikiwa kuhuisha Mwongozo wa Taifa wa Usimamizi wa Viashiria Hatarishi wa Mwaka 2012, Mwongozo wa Usimamizi wa Viashiria vya Udanganyifu wa Mwaka 2015 na Mwongozo wa Usimamizi wa Udhibiti wa Ndani ili kuendana na miongozo ya kimataifa. Kazi nyingine iliyofanyika ni kuhuisha mwongozo wa ukaguzi wa miradi ya ujenzi wa miundombinu.

3.2.8 Kuimarisha mifumo ya usimamizi wa fedha za umma

24. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2023, Mfumo wa Malipo Serikalini - MUSE umeboreshwa na kufungamanishwa na Mfumo wa Taarifa za Watumishi wa Umma - HCMIS ili kusomana na kubadilishana taarifa; kuboresha Mfumo wa D-Fund MIS kwa kuunganisha na Mfumo wa Benki Kuu ya Tanzania (Central Banking Systems -CBS) ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za fedha za miradi zinazopelekwa moja kwa moja kwenye miradi na Washirika wa Maendeleo; na kuboresha Mfumo wa GARI–ITS sambamba na kuhuisha taarifa za taasisi za umma 463. Aidha, Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi wa Umma inaendelea kuunda na kujenga mfumo mpya wa kielektroniki wa ununuzi wa umma ili kuimarisha udhibiti wa fedha za umma. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilika kwa moduli ya kusimamia mpango wa ununuzi wa mwaka, moduli ya kuanzisha mchakato wa ununuzi, moduli ya usanifu wa nyaraka za zabuni ndani ya mfumo na usanifu wa nyaraka za kusaini kidijitali ndani ya mfumo, moduli ya uwekaji wa bei kikomo, moduli ya kutumia mfumo wa simu za kiganjani (Mobile App) na moduli ya usajili wa zabuni. Vilevile, mfumo umefungamanishwa (integrated) na mifumo mingine tisa (9) ya taasisi za Serikali ikiwemo TRA TIN, CRB MIS, PLANREP, MUSE, BRELA OTRS, PSPTB MIS, ERB MIS, ERMS, na GePG na unatarajiwa kuanza kutumika Julai 2023.

3.2.9 Kuandaa na kujenga ghala la takwimu (Data warehouse)

25. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, wizara ilipanga kuandaa na kujenga ghala la takwimu ili kurahisha upatikanaji wa taarifa za utekelezaji wa mipango na bajeti ya Serikali. Hadi Aprili 2023, wizara imekamilisha hatua ya awali ya kuainisha mahitaji na vyanzo vya taarifa na takwimu zitakazohifadhiwa kwenye ghala. Mahitaji hayo yamewezesha kuanza kazi ya usanifu na ujenzi wa ghala.

3.2.10 Kuratibu na kusimamia zoezi la Sensa ya Watu na Makazi

26. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, tulikuwa na agenda ya kitaifa ya Sensa ya Watu na Makazi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu na wananchi kwa jumla kuwa zoezi la Sensa ya Watu na Makazi lilifanyika kwa mafanikio makubwa sana. Baada ya uzinduzi wa matokeo ya mwanzo ya Sensa, ripoti nyingine kumi (10) za Sensa ya Watu na Makazi zilizojikita katika mgawanyo wa idadi ya watu katika maeneo ya kiutawala, mgawanyo wa idadi ya watu kwa umri na jinsi na mgawanyo wa idadi ya watu katika majimbo ya uchaguzi zilizinduliwa na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huko Zanzibar Aprili 15, 2023. Aidha, takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 zimetumika katika maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023. Hatua inayoendelea, ni kusambaza ripoti kwa wadau, kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi ya takwimu za Sensa ya Watu na Makazi, kufuatilia utekelezaji wake na kuendelea kuchakata, kuchambua na kuandaa ripoti nyingine za kisekta kulingana na ratiba ya kutoa machapisho ya Sensa. Kwa niaba ya Serikali, natoa wito kwa wadau wote kufuatilia na kutumia takwimu za Sensa ya Watu na Makazi kusimamia mipango yao.

3.2.11 Kuziwezesha taasisi za Wizara, hususan taasisi za elimu na mafunzo kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunza

27. Mheshimiwa Spika, kufuatia mapinduzi makubwa yaliyofanyika katika sekta ya elimu, ngazi ya elimumsingi na sekondari na kusababisha ongezeko la wanafunzi wanaodahiliwa katika vyuo vya elimu ya juu, wizara ilipata ridhaa ya Bunge lako Tukufu

kutumia shilingi bilioni 19 kupitia bajeti yake ya maendeleo ili kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika taasisi tano (5) za elimu ya juu zilizo chini ya wizara. Hadi Aprili 2023, taasisi hizo zimepokea jumla ya shilingi bilioni 11.83, sawa na asilimia 62.27 ya makadirio ya mwaka 2022/23.

3.2.12 Kuendelea na ujenzi wa jengo la Wizara katika Mji wa Magufuli, Mtumba Dodoma

28. Mheshimiwa Spika, wizara inaendelea na ujenzi wa jengo lake katika Mji wa Magufuli, Mtumba Dodoma. Hadi Aprili 2023, utekelezaji umefikia asilimia 42.25 ambapo ujenzi unatarajiwa kukamilika Septemba 2023. Kazi zilizokamilika hadi sasa ni ujenzi wa mihimili ya basement, mihimili ya sakafu ya chini katika jengo kuu, na mihimili ya ghorofa ya kwanza hadi ghorofa ya tisa pamoja sakafu na mihimili ya kumbi. Aidha, kazi zinazoendelea ni nakshi ya kuta na sakafu, ufungaji wa viyoyozi, vifaa vya kuzima moto, mifumo ya umeme, majitaka na maji safi pamoja na ujenzi wa jiko, sehemu ya mapokezi na mgahawa.

3.2.13 Kujenga na kukarabati miundombinu ya Wizara mkoa wa Geita, Njombe, Songwe, Dar es Salaam, Morogoro, Kigoma na Ruvuma.

29. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, wizara ilipanga kujenga ofisi katika mikoa ya Geita, Njombe na Songwe na kukarabati majengo ya ofisi katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Kigoma na Ruvuma. Hadi Aprili 2023, mkataba kwa ajili ya mkandarasi wa ujenzi wa ofisi Geita umethibitishwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, ujenzi wa ofisi katika mkoa wa Njombe na Songwe umefikia hatua ya mshauri elekezi kupewa zabuni kwa ajili ya usanifu wa michoro na kusimamia ujenzi. Vilevile, ukarabati wa ofisi katika mkoa wa Morogoro umekamilika na mkoa wa Dar es salaam pamoja na Kigoma umefikia asilimia 90 na asilimia 43 mtawalia.

3.3 Mwenendo wa Utekelezaji wa Majukumu Mengine ya Wizara

30. Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa vipaumbele vya wizara kwa mwaka 2022/23, kazi nyingine zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu na kutekelezwa kwa ufanisi ni kama ifuatavyo:

3.3.1 Uandaaji wa Mipango, Sheria na Miongozo ya Kisera

31. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2023, wizara imefanikiwa kuandaa mipango, sheria na miongozo mbalimbali ya kisera na kitaalamu ikiwemo: Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2023/24; Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/24; kuhuisha Mwongozo wa Wizara wa Usimamizi wa Vihatarishi; mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya PPP, Sura 103 ambapo muswada uliwasilishwa na kusomwa kwa mara ya kwanza katika Bunge la Februari, 2023; na mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 ambayo yameridhiwa na Baraza la Mawaziri. Aidha, Ofisi ya Msajili wa Hazina inaendelea kufanya mapitio ya Sheria ya Ofisi ya Msajili wa Hazina ambapo hatua iliyofikiwa ni kukusanya maoni na mapendekezo ya wadau kuhusu changamoto, udhaifu na fursa za vitega uchumi vya Serikali.

3.3.2 Uhakiki, Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo

32. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2023, wizara imefanikiwa kufuatilia na kuhakiki fidia kwa wananchi wanaopisha maeneo ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo Bararaba ya Masasi hadi Mtwara (160km), ujenzi wa barabara ya Tanga-Pangani-Bagamoyo sehemu ya Mkange-Mandamazingira, Reli ya kisasa kutoka Isaka hadi Mwanza, Mabasi yaendayo Haraka Awamu ya Pili – Ubungo Kisiwani, Njia za kusafirisha umeme kutoka Chalinze, Morogoro hadi Dodoma, Iringa hadi Sumbawanga na Wilaya ya Monduli hadi Makuyuni. Aidha, Wizara imefanikiwa kufanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo 222 katika mikoa 17 ya Kagera, Kigoma, Geita, Mwanza, Shinyanga, Tabora, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Njombe, Katavi, Rukwa, Mara, Simiyu, Dar es Salaam, Morogoro na Pwani. Kati ya miradi hiyo, miradi nane (8) ya kielelezo ambayo ni: Bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere - MW 2,115; Reli ya Standard Gauge; Kiwanda cha kusindika sukari – Mkulazi; kufufua Shirika la Ndege la Taifa; mpango wa ununuzi wa meli za uvuvi katika Bahari Kuu; ujenzi wa Bandari ya Uvuvi; Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kutoka Hoima, Uganda hadi bandari ya Tanga-Chongoleani na daraja la Kigongo-Busisi. Vilevile, wizara imefanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi 16 inayosimamiwa na Shirika la Maendeleo la Taifa katika mikoa tisa (9), ambayo ni Kilimanjaro, Mwanza, Pwani, Tanga, Ruvuma, Njombe, Dar es Salaam, Arusha na Morogoro.

3.3.3 Kuanzisha Ofisi ya Msuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi

33. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, wizara ilipanga kuanzisha Ofisi ya Msuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi (Tax Ombudsman Office). Hadi Aprili 2023, muundo na mgawanyo wa majukumu ya Ofisi hiyo umeandaliwa na kuidhinishwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, watumishi watakaohudumu katika Ofisi hiyo wamepatikana na kuanza kazi rasmi Februari 2023. Kazi inayoendelea kwa sasa ni kuandaa mifumo ya usimamizi wa malalamiko na taarifa za wadau pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu majukumu ya Ofisi na umuhimu wake katika kuimarisha utawala wa sheria na utawala bora katika tasnia ya masuala ya kodi.

3.3.4 Usimamizi wa Deni la Serikali

34. Mheshimiwa Spika, wizara inaendelea kusimamia deni la Serikali kwa kuzingatia Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, SURA 134. Ili kuwa na taarifa sahihi kuhusu udhibiti wa deni la Serikali, wizara imefanya tathmini ya uhimilivu wa deni la Serikali kwa miaka 20 ijayo, kuanzia 2022/23 hadi 2041/42. Matokeo ya tathmini yanaonesha kuwa, deni la Serikali ni himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu. Aidha, taarifa inaonesha kuwa thamani ya sasa ya deni la Serikali kwa Pato la Taifa ni asilimia 31.8 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu, wananchi na wadau wote wa maendeleo kuwa Taarifa kamili inapatikana katika tovuti ya wizara ambayo ni www.mof.go.tz.

3.3.5 Ushauri wa Kitaalamu kwa Miradi ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi

35. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2023, wizara imetoa mafunzo na ushauri wa kitaalamu ili kuziwezesha Mamlaka za Serikali kuandaa miradi ya maendeleo itakayotekelezwa kwa utaratibu wa PPP. Ushauri na mafunzo umekuwa na matokeo chanya ambapo, Wakala wa Barabara Tanzania umeweza kukamilisha maandalizi ya mradi wa barabara ya haraka ya tozo kutoka Kibaha hadi Morogoro (205 Km) na hatua za ununuzi wa mbia zinaendelea. Aidha, majadiliano na mbia aliyepatikana kwa ajili ya uendeshaji wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam yanaendelea. Vilevile, Chuo cha Elimu ya Biashara kinakamilisha taarifa ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya mradi wa kujenga mabweni ya wanafunzi na Jeshi la Polisi linakamilisha upembuzi yakinifu kwa Mradi wa Ukaguzi wa Lazima wa Vyombo vya Moto.

3.3.6 Huduma za Pensheni na Mafao ya Wastaafu

36. Mheshimiwa Spika, wizara imeboresha mfumo wa usimamizi wa majalada ya wastaafu kwa njia ya kielekroniki ambapo moduli ya ufuatiliaji wa majadala ya wastaafu imeandaliwa ili kuboresha huduma za pensheni na mafao kwa wastaafu wanaohudumiwa na Hazina. Maboresho hayo yamewezesha majalada 148,148 kuingizwa kwenye mfumo. Aidha, katika kipindi hicho, wizara imelipa pensheni kwa wastaafu 49,407, mirathi kwa warithi na walezi 1,474 na malipo ya kiinua mgongo kwa watumishi 1,370 walioajiriwa kwa masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni kwa watumishi 1,673 walioajiriwa kwa mikataba.

3.4 Mwenendo wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Taasisi za Wizara

37. Mheshimiwa Spika, wizara inatekeleza baadhi ya majukumu yake kupitia taasisi zake za elimu na mafunzo, bodi za kitaalamu na kitaaluma, usimamizi wa fedha, kodi, bima, ununuzi na ugavi, michezo ya kubahatisha, uwekezaji na uwezeshaji pamoja na takwimu.

3.4.1 Taasisi za Mafunzo na Elimu ya Juu

38. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, taasisi tano (5) za mafunzo na elimu ya juu zilitarajia kudahili jumla ya wanafunzi 73,074, ikijumuisha ngazi za astashahada 14,017, stashahada 19,427, shahada 37,450 na uzamili 2,180. Aidha, taasisi hizo zilitarajia kuendeleza wahadhiri 196, ambapo ngazi ya uzamivu ni 158 na uzamili 38.

39. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2023, jumla ya wanafunzi 70,638 wamedahiliwa na taasisi zote tano (5), sawa na asilimia 96.7 ya lengo. Kati ya wanafunzi waliodahiliwa, 13,916 ni ngazi ya cheti, stashahada 16,470, shahada ya awali 37,057 na uzamili 31,195. Aidha, jumla ya wahadhiri 159 wamewezeshwa kujiendeleza katika masomo ambapo 144 ni ngazi ya uzamivu na 15 ni uzamili.

40. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Usimamizi wa Fedha kilipanga kukamilisha ujenzi wa mabweni manne (4) yenye ghorofa moja kila moja yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 400, nyumba nne (4) zenye uwezo wa kuhudumia familia nane (8) za wafanyakazi pamoja na maktaba moja (1) katika kampasi ya Geita; kuendelea na ukarabati wa miundombinu katika kampasi ya Dar es Salaam na ujenzi wa jengo la taaluma likijumuisha ofisi zenye uwezo wa kuhudumia wahadhiri 40 na madarasa yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,520 kwa wakati mmoja katika kampasi ya Mwanza. Hadi Aprili 2023, ukarabati katika kampasi kuu umefikia asilimia 88 na ujenzi wa mabweni na nyumba za watumishi katika kampasi ya Geita umefikia asilimia 30 na asilimia 68 mtawalia. Aidha, ujenzi wa kampasi ya Mwanza umefikia asilimia 3.

41. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Chuo cha Uhasibu Arusha kilipata ridhaa ya kuendelea na ujenzi wa mabweni manne (4) yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,000 katika kampasi kuu Arusha; kukamilisha ujenzi wa jengo la utawala linalojumuisha madarasa 17 yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2210 kwa wakati mmoja, mabweni mawili (2) yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja na jengo moja (1) la utawala katika kampasi ya Babati; na kufanya mapitio ya mitaala 10. Hadi Aprili 2023, ujenzi wa mabweni katika kampasi ya Arusha umefikia asilimia 30, madarasa asilimia 99 na ujenzi wa jengo la utawala na mabweni katika kampasi ya Babati umefikia asilimia 55 na asilimia 20 mtawalia. Aidha, kazi ya mapitio ya mitaala imekamilika.

42. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini kilipanga kufanya tafiti saba (7) na kutoa huduma za ushauri elekezi kwa kuzingatia mahitaji ya wadau; kuwezesha mafunzo kwa watumishi 396; kukarabati nyumba 13 za watumishi katika kampasi kuu Dodoma; na kuendelea na ujenzi wa bweni la wanafunzi na maktaba katika Kituo cha Mafunzo, Kanda ya Ziwa Mwanza. Hadi Aprili 2023, Chuo kimefanikiwa kufanya tafiti saba (7), kutoa huduma elekezi tatu (3), kujengea uwezo watumishi 48, kukarabati nyumba za watumishi mbili (2) na ujenzi wa bweni la wanafunzi na maktaba katika Kituo cha Mafunzo, Kanda ya Ziwa Mwanza umefikia asilimia 92 na asilimia 15 mtawalia.

43. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Taasisi ya Uhasibu Tanzania ilipanga kujenga jengo moja la utawala katika kampasi ya Misungwi, Mwanza na kampasi ya Kigoma; jengo moja (1) linalojumuisha ukumbi wa mihadhara, maabara ya kompyuta na maktaba katika Kampasi ya Mbeya; na kuboresha miundombinu na huduma mtandao wa internet katika maktaba za kampasi zote. Hadi Aprili 2023, utekelezaji wa mradi wa jengo la utawala kampasi ya Misungwi, Mwanza umefikia asilimia 72 na Kigoma utekelezaji umefikia hatua ya mkandarasi kukabidhiwa eneo la mradi. Aidha, ujenzi wa jengo katika kampasi ya Mbeya umefikia asilimia 72. Vilevile, maktaba za kampasi zote zimeboreshwa kwa kuunganishwa na huduma ya mtandao wa internet.

44. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika kilipanga kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala, kuendeleza wahadhiri 28 na kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 20. Hadi Aprili 2023, ujenzi wa jengo la utawala umefikia asilimia 34, kuendeleza wahadhiri 28 katika shahada ya uzamivu na kuwajengea uwezo watumishi 9 katika maeneo mbalimbali.

3.4.2 Bodi za Kitaaluma na Kitaalamu

45. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi ilitarajia kusajili wataalamu 3,500 wa ununuzi na ugavi, kuendesha mafunzo na ushauri wa kitaalamu kwa wataalamu 6,500 na kuendesha mitihani ya kitaaluma kwa watahiniwa 4,000. Aidha, Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu ilitarajia kusajili wahasibu 1,125 katika ngazi mbalimbali, kuanza ujenzi wa ofisi ya Makao Makuu Jijini Dodoma, kufanya ukaguzi wa ubora wa uandaaji wa taarifa za fedha kwa taasisi 75 na kutoa mafunzo ya stashahada ya viwango vya uandaaji wa taarifa za fedha serikalini kwa wahitimu 500.

46. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2023, Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi imesajili wataalamu 1,790, sawa na asilimia 51.2, kuendesha mafunzo na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wataalamu 2,508, sawa na asilimia 38.8 na kuendesha mitihani kwa watahiniwa 2,416, sawa na asilimia 60.4. Aidha, Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu imesajili wahasibu na wakaguzi 1,200, kufanya kaguzi za ubora wa uandaaji wa taarifa za fedha kwa taasisi 68 na kutoa mafunzo ya stashahada ya viwango vya uandaaji wa taarifa za fedha Serikalini kwa wahitimu 191 na kuendesha mitihani ya kitaaluma kwa watahiniwa 6,988. Vilevile, ujenzi wa jengo la Ofisi Dodoma umeanza ambapo mtaalamu mshauri ameanza kazi za kuandaa michoro na upimaji wa mitetemo.

3.4.3 Taasisi za Usimamizi wa Kodi

47. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Mamlaka ya Mapato Tanzania -TRA ilikadiriwa kukusanya shilingi trilioni 23.6, kuhuisha Mkakati wa Muda wa Kati na Mrefu wa Ukusanyaji Mapato, kutunga upya Sheria na Kanuni za Ushuru wa Stempu na Bidhaa, kuanzisha Maabara ya Forodha, kujenga na kutekeleza Mfumo Unganifu wa Kusimamia Mapato ya Ndani na kuboresha Kituo cha Udhibiti na Ufuatiliaji wa Mifumo. Aidha, Bodi ya Rufaa za Kodi na Baraza la Rufaa za Kodi zilitarajia kuendelea kusajili, kusikiliza na kutoa maamuzi ya maombi, mashauri na rufaa za kodi ili kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara nchini.

48. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2023, Mamlaka ya Mapato Tanzania imekusanya shilingi trilioni 18.8, sawa na ufanisi wa asilimia 79.5 ya lengo la mwaka. Aidha, Mamlaka imefanikiwa kukusanya mapendekezo ya kuboresha Mkakati wa Muda wa Kati na Mrefu wa Ukusanyaji wa Mapato, kuandaa rasimu ya mapendekezo ya kufuta na kutunga upya Sheria ya Usimamizi na Viwango vya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147, kuboresha moduli za mfumo jumuishi wa ukusanyaji wa kodi za ndani ikiwemo dirisha moja la walipakodi, moduli ya usajili wa walipakodi na moduli ya marejesho ya kodi.

49. Mheshimiwa Spika, Bodi ya Rufaa za Kodi imefanikiwa kusikiliza mashauri 423 yenye thamani ya kiasi cha kodi kinachobishaniwa cha shilingi bilioni 849.83, kati ya mashauri 1,155 yaliyosajiliwa yenye kiasi cha kodi kinachobishaniwa cha shilingi trilioni 7.35 na dola za Marekani milioni 5.22. Kati ya maamuzi yaliyotolewa, Mamlaka ya Mapato Tanzania imeshinda mashauri 344 yenye thamani ya kiasi cha kodi kinachobishaniwa cha shilingi bilioni 824.13 na walipakodi kushinda mashauri 79 yenye thamani ya kiasi cha kodi kinachobishaniwa cha shilingi bilioni 25.71. Aidha, Baraza la Rufaa za Kodi limefanikiwa kusikiliza na kutolea maamuzi mashauri 87 yenye thamani ya kodi inayobishaniwa ya shilingi bilioni 237.71 na dola za Marekani milioni 2.93 ikiwa ni sehemu ya mashauri 244 yaliyosajiliwa. Kati ya maamuzi yaliyotolewa na Baraza, Mamlaka ya Mapato Tanzania imeshinda mashauri 74 yenye thamani ya shilingi bilioni 234.20 na walipa kodi kushinda mashauri 13 yenye thamani ya shilingi bilioni 3.51 na dola za Marekani milioni 2.93.

3.4.4 Bodi ya Michezo ya Kubahatisha

50. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha ilitarajia kutoa leseni 7,697 kwa waendesha michezo ya kubahatisha, ambapo 1,923 ni leseni mpya na 5,774 ni leseni za kuhuishwa; kufanya ukaguzi kwa waendesha michezo ya kubahatisha 83; kufanya mapitio ya Sheria na Kanuni za Michezo ya kubahatisha; na kurejesha Bahati Nasibu ya Taifa. Hadi Aprili 2023, Bodi imetoa jumla ya leseni 8,778 sawa na asilimia 114 ambapo leseni mpya 3,658 na zilizohuishwa 5,120, kufanya kaguzi 88, sawa na asilimia 106, kuandaa mapendekezo ya mapitio ya Sheria na Kanuni za Michezo ya kubahatisha. Aidha, uteuzi wa kampuni ya kuendesha Bahati Nasibu ya Taifa upo katika hatua za mwisho na unatarajiwa kukamilika Juni 2023 ambapo uendeshaji utaanza katika mwaka 2023/24.

3.4.5 Masoko ya Mitaji, Dhamana na Bidhaa

51. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ilipanga kuanza kusimamia masoko ya mitaji kwa kutumia mfumo wa vihatarishi, kupanua wigo wa elimu kwa umma kuhusu masoko ya mitaji, dhamana na bidhaa pamoja na kuongeza idadi ya bidhaa katika soko, hususan hisa, hatifungani na vipande katika mifuko ya uwekezaji wa pamoja. Aidha, Soko la Bidhaa Tanzania lilipanga kutoa elimu kwa umma na kuboresha mfumo wa mauzo kulingana na mazingira ya bidhaa husika.

52. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2023, Mamlaka imefanikiwa kuanza kutumia mfumo wa vihatarishi katika usimamizi wa masoko ya mitaji, kutoa elimu kwa umma kuhusu masoko ya mitaji kwa wadau wapatao milioni 1.2 na kuongeza bidhaa mpya 47 katika masoko ya mitaji kutoka 637 na kufikia 684, ambazo zinajumuisha hisa; hatifungani; na mifuko ya uwekezaji wa pamoja. Aidha, Soko la Bidhaa Tanzania limetoa elimu kwa wadau 190,954 katika mikoa ya Manyara, Simiyu, Rukwa, Morogoro, Mbeya, Kagera, Mwanza, Tabora, Mara, Lindi, Songwe na Shinyanga. Vilevile, Soko limeendelea kuboresha mfumo wa biashara kwa njia ya kielekitroniki ili kuwezesha uuzaji wa mazao mapya ikiwemo chai, pamba, mkonge pamoja na mifugo hai na ngozi. Mpaka sasa mfumo una uwezo wa kuwezesha uuzaji na ununuzi wa ufuta, choroko, dengu, korosho, kakao, kahawa na mbaazi.

3.4.6 Taasisi za kibenki

53. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Benki Kuu ya Tanzania ilipanga kuchochea na kudhibiti ustawi wa viashiria vya uchumi jumla, kukuza wastani wa ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ili kuendana na mahitaji ya shughuli za kiuchumi, kuchochea ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi, kudhibiti na kupunguza kiwango cha mikopo chechefu pamoja na kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosheleza mahitaji ya kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4). Hadi Aprili 2023, wastani wa ongezeko la ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa asilimia 17.2 dhidi ya lengo la asilimia 10.3, na mfumuko wa bei ulifikia asilimia 4.3 ikilinganishwa na lengo la asilimia 5 hadi 7. Aidha, mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa asilimia 22.5 ikilinganishwa na lengo la asilimia 10.7. Mwenendo mzuri wa ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi umetokana na kuimarika kwa mahitaji ya mikopo mipya kufuatia hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji na biashara na usimamizi imara wa sera za fedha na bajeti. Kiwango cha mikopo chechefu kilipungua kufikia asilimia 5.5 dhidi ya lengo la asilimia 5. Vilevile, akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa katika viwango vya kutosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi katika kipindi kisichopungua miezi minne (4).

54. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ilitenga shilingi bilioni 36.1 kwa ajili ya mikopo kwa miradi ya kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao ya kilimo, shilingi bilioni 77.45 kwa ajili ya mikopo ya utekelezaji wa miradi ya kuzuia upotevu wa mazao baada ya kuvuna na shilingi bilioni 90 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kuwezesha ukusanyaji na uuzaji wa mazao ya kilimo. Aidha, Benki ilipanga kushawishi benki nne (4) za biashara kushiriki katika mfuko wa dhamana ili kuchagiza uwekezaji katika sekta ya kilimo.

55. Mheshimiwa Spika, hadi Desemba 2022, shilingi bilioni 33.22 zilitolewa kupitia mfumo wa ukopeshaji wa moja kwa moja kwa miradi inayolenga kuongeza tija katika uzalishaji; shilingi bilioni 44.2 zilikopeshwa kwa wakulima wadogo kwa ajili ya miradi ya kuzuia upotevu wa mazao ambapo kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 35.9 zilitolewa kupitia mfumo wa ukopeshaji wa moja kwa moja na shilingi bilioni 8.3 kupitia mfuko wa dhamana. Aidha, shilingi bilioni 97.7 zilikopeshwa kwa wakulima wadogo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kuwezesha upatikanaji wa masoko ya mazao ambapo kati ya kiasi hicho shilingi bilioni 81.3 zilitolewa kwa mfumo wa ukopeshaji wa moja kwa moja na shilingi bilioni 16.4 zilitolewa kupitia mfuko wa dhamana. Vilevile, ili kuchagiza uwekezaji katika sekta ya kilimo, benki ilifanikiwa kushawishi benki moja (1) ya biashara kujiunga katika mfuko wa dhamana wa wakulima wadogo.

56. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022, Benki ya Maendeleo TIB ilipanga kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 47 katika sekta ya viwanda, maji, nishati, miundombinu ya viwanda, miundombinu ya serikali za mitaa, madini, mafuta na gesi, huduma, utalii na kilimo; kukuza mizania ya benki kufikia kiasi cha shilingi bilioni 902.63; kupunguza ukwasi kwa kuongeza mtaji wa benki kwa shilingi bilioni 373 na kuuza hati fungani zenye thamani ya shilingi bilioni 300. Hadi Desemba 2022, Benki imefanikiwa kutoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 13.71 katika Sekta za maji, utalii, nishati/umeme, kilimo, pamoja na huduma za usafiri na mawasiliano. Aidha, mizania ya benki ilikua na kufikia shilingi bilioni 487.75. Hata hivyo, Benki haikuweza kufikia malengo yake kutokana na changamoto ya mtaji, ukwasi na athari ya kiwango cha mikopo chechefu.

57. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022, Benki ya Biashara ya Tanzania ilipanga kuongeza mapato kufikia shilingi bilioni 185.6, kukuza faida ya Benki kabla ya kodi kufikia shilingi bilioni 21.4, kutoa mikopo salama ya shilingi bilioni 709, kukusanya amana za wateja shilingi bilioni 974, kukuza mali za Benki kufikia shilingi bilioni 1,257 na kukuza thamani ya hisa kufikia shilingi bilioni 128. Hadi Desemba 2022, Benki imeongeza mapato kufikia shilingi bilioni 174, faida kabla ya kodi shilingi bilioni 11.2, mikopo salama shilingi bilioni 842, amana zenye thamani ya shilingi bilioni 987, mali za Benki kufikia shilingi bilioni 1,290 na thamani za hisa kufikia shilingi bilioni 116.

3.4.7 Taasisi za Bima

58. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania ilipanga: kufanya uchambuzi wa mikataba ya bima mtawanyo kwa kampuni 30 za bima nchini; kufanya ukaguzi wa kampuni 30 za bima, madalali 70, benki wakala 26 na mawakala 278; kufanya upekuzi wa kina ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato kwa kampuni 10; kutoa elimu ya bima kwa watu takribani milioni 1.5 kuhusu huduma za bima; na kuhamasisha kampuni za bima kuandaa bidhaa zinazolenga kuchochea kinga dhidi ya vihatarishi vya shughuli za kilimo.

59. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2023, Mamlaka imefanikiwa kuchambua mikataba 255 ya bima mtawanyo kwa kampuni 32, kufanya ukaguzi wa kampuni 10, madalali 11, mawakala 358 na benkiwakala 10. Aidha, mafanikio mengine yaliyopatikana ni upekuzi wa kampuni 10 za bima, kutoa elimu ya bima kwa wananchi takribani 953,816 kupitia njia mbalimbali ikiwemo semina, maonyesho, mikutano na vyombo vya habari na kuidhinisha bidhaa mpya nne (4) za kinga dhidi ya shughuli za kilimo ambazo ni Mtumbwi Salama (Jubilee Insurance Company), Mkulima (Alliance Insurance Company), Livestock Insurance (UAP Insurance Company) na Agriculture (Heritage Insurance Company).

60. Mheshimiwa Spika, Shirika la Taifa la Bima lilitarajia kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa huduma zake, kubuni bidhaa mpya nne (4) na kuandaa mfumo wa usimamizi wa vihatarishi. Hadi Aprili 2023, Shirika limetoa elimu kwa kampuni, mashirika na taasisi 63 na kuingiza sokoni bidhaa mpya za BimaLife na Linda Mjengo. Aidha, Shirika limefanikiwa kuandaa mfumo wa kusimamia vihatarishi.

3.4.8 Taasisi za Uwekezaji na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

61. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Kampuni ya Uwekezaji wa Pamoja - UTT AMIS ilipanga kuongeza rasilimali za mifuko kwa kiwango cha asilimia 15, kuongeza idadi ya wawekezaji kwa asilimia 5 na kuhamasisha taasisi za Serikali, mifuko ya hifadhi za jamii, mashirika na vikundi mbalimbali vya kijamii kama vile SACCOS kujiunga na mifuko ya UTT AMIS. Aidha, Mfuko wa SELF ulipanga kutoa mikopo yenye masharti nafuu ya shillingi bilioni 43.5 kwa wajasiriamali 28,255, kuhakikisha kiwango cha urejeshaji wa mikopo kinafikia asilimia 95 na kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wadau au wanufaika 4,000.

62. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2023, UTT-AMIS imeongeza rasilimali za mifuko kwa shilingi bilioni 465, sawa na ongezeko la asilimia 46.6 ambapo thamani ya mifuko imefikia shilingi bilioni 1,461.5. Aidha, katika kipindi hicho, idadi ya wawekezaji katika mifuko imeongezeka kutoka 201,574 hadi 241,264, sawa na ongezeko la asilimia 19.7. Vilevile, Kampuni inaendelea kutoa elimu kuhusu faida za mifuko ya uwekezaji wa pamoja kwa vikundi vya kijamii ambapo vikundi 239 vimejiunga na mifuko ya UTT AMIS.

63. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mfuko wa SELF umetoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 34.4 kwa wanufaika 20,528. Aidha, mafunzo kuhusu ujuzi wa biashara, usimamizi wa kumbukumbu za kimsingi na usimamizi wa mikopo binafsi yalitolewa kwa vikundi 2,363 na urejeshaji wa mikopo iliyotolewa na mfuko umefikia asilimia 92.4 ya lengo.

3.4.9 Usimamizi wa Takwimu Rasmi

64. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilipata ridhaa ya Bunge lako Tukufu kukamilisha zoezi la Sensa ya Watu na Makazi, kufanya utafiti wa Sekta isiyo rasmi na utafiti wa Afya ya Mama na Mtoto na kuendelea kutoa takwimu za msingi za uchumi kila mwezi, robo mwaka na nusu mwaka kulingana na aina ya takwimu. Hadi Aprili 2023, Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilifanikiwa kusimamia kwa weledi zoezi la Sensa ya Watu na Mkazi na matokeo rasmi yalizinduliwa Aprili 15, 2023. Aidha, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imeendelea kutoa kwa wakati takwimu za mwenendo wa uchumi ambapo takwimu za Pato la Taifa zimetolewa hadi Desemba 2022 na mfumuko wa bei hadi Aprili 2023. Vilevile, Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa kushirikiana na Wizara ya Afya pamoja na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar imefanya Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria kwa Mwaka 2022 katika kipindi cha Februari hadi Julai 2022 ambapo Taarifa ya Viashiria Muhimu kulingana na utafiti huo imetolewa rasmi

Januari 2023.

3.4.10 Usimamizi na Udhibiti wa Ununuzi wa Umma

65. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma ilipanga kuanza ujenzi wa ofisi ya Makao Makuu Jijini Dodoma na ukarabati wa ofisi ya kanda Jijini Dar es Salaam, kuwezesha mafunzo kwa watumishi 940 kutoka katika taasisi nunuzi 170 na wazabuni 1,200 ambao wamejisajili katika mfumo wa TANePS, kufanya mapitio na kuanza ujenzi wa mfumo wa ununuzi wa umma kwa njia ya mtandao na kufanya kaguzi za ukidhi na thamani ya fedha kwa taasisi nunuzi 180. Aidha, Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini ulipanga kukamilisha ujenzi wa Ofisi ya Mkoa wa Kigoma, kituo cha mafuta katika mikoa ya Njombe, Pwani, Arusha na Wilaya ya Kahama na ujenzi wa ghala katika Wilaya ya Korogwe, Masasi na Dodoma. Vilevile, Mamlaka ya Rufaa za Zabuni ilipanga kuandaa mfumo wa kielektroniki wa usajili na usimamizi wa rufaa za ununuzi wa umma na kufanya mapitio ya kanuni za rufaa.

66. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2023, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma imeendelea na ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu Jijini Dodoma ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 49.9. Ukarabati wa Ofisi ya Kanda Dar es Salaam umekamilika na Jengo limeanza kutumika. Aidha, Mamlaka imetoa mafunzo kwa wazabuni 214 na watumishi 691 kutoka katika taasisi nunuzi 113 kuhusu matumizi ya mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma na mafunzo ya Sheria ya Ununuzi wa Umma, SURA 410 kwa washiriki 1,377 kutoka katika taasisi 210. Vilevile, Mamlaka ya Rufaa za Zabuni imefanya mapitio ya kanuni za usikilizaji wa rufaa, kanuni hizo zitaanza kutumika baada kukamilika kwa maboresho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma pamoja na kanuni zake.

67. Mheshimiwa Spika, Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini umewezesha ununuzi wa pamoja wa magari 802 na pikipiki 1,103 za Serikali kwa gharama ya shilingi 127,367,937,558.97 na ujenzi wa ofisi mkoa wa Geita pamoja na ukarabati wa kituo cha mafuta Wilaya ya Kinondoni umekamilika. Aidha, ujenzi wa ofisi katika mikoa ya Pwani, Songwe, Simiyu, na Dodoma umefikia asilimia 75 na ukarabati wa ofisi za Wakala katika mikoa ya Singida na Arusha umefikia asilimia 85 ikiwa ni mwendelezo wa utekelezaji wa miradi iliyopangwa mwaka 2021/22. Vilevile, mshauri elekezi kwa ajili ya kuandaa ramani na gharama za ujenzi wa ofisi katika mikoa ya Kigoma, Njombe na Arusha amepatikana.

3.4.11 Udhibiti wa Utakasishaji wa Fedha Haramu, Ufadhili wa Ugaidi na Ufadhili wa Silaha za Maangamizi

68. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu kilipanga kupokea na kuchambua miamala ya fedha na kuandaa taarifa fiche kwa hatua stahiki. Hadi Aprili 2023, Kitengo kimepokea taarifa 7,313 za fedha taslimu zenye thamani ya shilingi trilioni 56.65, taarifa 8,784 za usafirishaji fedha kwa njia ya kielektroniki zenye thamani ya shilingi trilioni 222.81 na taarifa 2,457 zinazohusu usafirishaji wa fedha taslimu na hati za malipo kupitia mipakani. Aidha, Kitengo kimechambua miamala shuku 769 na kuandaa taarifa fiche 314 na kuwasilisha kwenye taasisi za utekelezaji wa sheria kwa hatua za uchunguzi. Vilevile, mfumo wa Kitengo umeunganishwa na mfumo wa Mamlaka ya Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar pamoja na mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa ili kusomana na kubadilishana taarifa.

3.4.12 Kusimamia masuala ya pamoja ya fedha kati ya Tanzania Bara na Zanzibar

69. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, wizara ilipanga kufanya tathmini kuhusu fursa ya mapato kwa kampuni zinazosajiliwa upande mmoja wa Muungano na kufanya biashara pande zote. Hadi Aprili 2023, Wizara kupitia Tume ya Pamoja ya Fedha imefanikiwa kufanya stadi kuhusu kubainisha majukumu, mapato na matumizi yanayohusu utekelezaji wa mambo ya Muungano katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

3.5 Mwenendo wa utekelezaji wa Vipaumbele vya Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

70. Mheshimiwa spika, katika mwaka 2022/23, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilipata ridhaa ya Bunge lako Tukufu ya kuendelea kutekeleza majukumu yake, hususan kufanya kaguzi za hesabu za fedha, miradi ya maendeleo, ufanisi katika usimamizi wa miongozo, uwekezaji wa mitaji ya Serikali, mifumo ya TEHAMA na usimamizi wa mazingira kwa Serikali Kuu, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; kufuatilia na kutathmini mwenendo wa utekelezaji wa hoja za ukaguzi; kuimarisha maabara ya ukaguzi; na kukusanya maduhuli ya shilingi 900,000,000.

71. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2023, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imefanikiwa kufanya kaguzi zote kama ilivyopangwa na kuwasilisha Ripoti zake bungeni Aprili 6, 2023. Sambamba na Ripoti za Ukaguzi, Ofisi imewasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Ripoti kuhusu mwenendo wa utekelezaji wa hoja za ukaguzi. Aidha, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imefanikiwa kukusanya mapato ya ndani ya jumla ya shilingi 421,912,164 sawa na ufanisi wa asilimia 47 ya lengo la mwaka.

3.6 Changamoto za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti na Mikakati ya kukabiliana nazo

3.6.1 Changamoto

72. Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya 2022/23, Wizara imekabiliana na changamoto zifuatazo:

i. Kasi ndogo ya ujengaji na maboresho ya mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa mapato na matumizi ya Serikali ikilinganishwa na kasi ya mabadiliko ya TEHAMA duniani na hivyo kuhatarisha ufanisi na usalama wa mifumo ya usimamizi wa fedha za umma; na
ii. Kuongezeka kwa bei na gharama za usafirishaji wa bidhaa na huduma kutoka nje, hususan bidhaa za petroli, mafuta ya kula, mbolea kutokana na athari za vita baina ya Urusi na Ukraine, ukame na UVIKO - 19 na hivyo kuongeza gharama katika utekelezaji wa mpango na bajeti, hususan miradi ya maendeleo.

5.2. Mikakati ya kukabiliana na changamoto

73. Mheshimiwa Spika, wizara itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na changamoto zinazoendelea kujitokeza ikiwa ni pamoja na:

i. Kuwekeza katika tafiti na maendeleo pamoja na mafunzo ili kukuza ubunifu na ujuzi katika kukabiliana na kasi ya mabadiliko ya TEHAMA duniani;
ii. Kuongeza kasi katika utekelezaji wa mradi wa kusambaza gesi viwandani, vituo vya gesi kwa matumizi ya magari na majumbani ili kupunguza msukumo wa uagizaji wa bidhaa za petroli kutoka nje ya nchi; na
iii. Kuongeza kasi ya tafiti za mafuta na gesi ili kuvutia uwekezaji wa kimkakati na hivyo kupunguza uhitaji wa uagizaji wa bidhaa hizo kutoka nje ya nchi.

4.0 Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2023/24

74. Mheshimiwa Spika, maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2023/24 yamezingatia miongozo mbalimbali ya kisera ya wizara, kitaifa, kikanda na kimataifa. Miongozo hiyo ni pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26; Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24; Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/24; Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati wa Uzinduzi wa Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Sheria ya Bajeti, Sura 439 pamoja na kanuni zake; Mikakati na makubaliano mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa; Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu; Mpango Mkakati wa Wizara wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26; na masuala mtambuka ikijumuisha jinsia, lishe, mazingira, mabadiliko ya tabia nchi, na UKIMWI.

4.1 Vipaumbele vya Mpango na Bajeti ya Wizara

75. Mheshimiwa Spika, vipaumbele vya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2023/24 ni kama ifuatavyo:

i. Kutafuta na kukusanya mapato ya shilingi trilioni 40.8 kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali;
ii. Kuhudumia deni la Serikali;
iii. Kufanya tafiti, tathmini na mapitio mbalimbali ya kitaalamu kuhusu mifumo ya usimamizi wa mipango, uchumi na bajeti ya Serikali;
iv. Kujenga, kuboresha, kufungamanisha na kuhuisha mifumo ya TEHAMA ya usimamizi wa mapato na matumizi ya Serikali;
v. Kujenga uwezo wa watumishi kuhusu usimamizi wa masuala ya sera, uchumi, mipango na fedha;
vi. Kuboresha miundombinu ya ofisi za Wizara na taasisi zake pamoja na miundombinu ya kufundishia na kujifunzia;
vii. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo inayotekelezwa na Wizara na Serikali kwa jumla; na
viii. Kukamilisha maboresho ya Sheria ya Msajili wa Hazina.

4.2 Vipaumbele vya Mpango na Bajeti kwa Fungu 45-Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

76. Mheshimiwa Spika, vipaumbele vya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni pamoja na: kufanya ukaguzi wa rasilimali za umma kwa Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma; kufanya kaguzi za kiufundi, ufanisi, maalum, kiuchunguzi, miradi ya maendeleo na mifumo ya TEHAMA; kuimarisha matumizi ya TEHAMA ndani ya Ofisi; na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa Ofisi za Ukaguzi mikoani.

4.3 Vipaumbele vya Taasisi

77. Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali, baadhi ya majukumu ya Wizara yanatekeleza kupitia taasisi za elimu, bodi za kitaalamu na kitaaluma, usimamizi na udhibiti wa masuala ya fedha, kodi, bima, ununuzi na ugavi, michezo ya kubahatisha, uwekezaji na uwezeshaji pamoja na takwimu.

4.3.1 Taasisi za Elimu

78. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha na Mipango inasimamia jumla ya taasisi za elimu tano (5) ambazo ni Chuo cha Usimamizi wa Fedha, Taasisi ya Uhasibu Tanzania, Chuo cha Uhasibu Arusha, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, na Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika. Kwa mwaka 2023/24, vyuo vyote vinatarajia kudahili jumla ya wanafunzi 77,432, ikijumuisha ngazi ya cheti 14,108, stashahada 18,744, shahada 41,483 na uzamili 397.

79. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/24, Chuo cha Usimamizi wa Fedha kimepanga kukamilisha ujenzi wa Kampasi ya Geita, kuanza ujenzi wa awamu ya pili wa Kampasi ya Simiyu kupitia Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Juu kwa Ajili ya Mageuzi ya Kiuchumi na kuendelea na ujenzi wa jengo la taaluma likijumuisha ofisi zenye uwezo wa kuhudumia wahadhiri 40 na madarasa yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,520 kwa wakati mmoja katika kampasi ya Mwanza.

80. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/24, Chuo cha Uhasibu Arusha kinatarajia kuendeleza watumishi 45 katika ngazi ya Shahada, Uzamili na Uzamivu ndani na nje ya nchi, kupitia mitaala 10 pamoja na kuandaa mitaala mipya miwili (2), kufungua kampasi mpya ya Songea mkoani Ruvuma, kuanza ujenzi katika kampasi ya Dodoma, kufanya tafiti mbili (2) na kutoa ushauri wa kitaaluma, kuanza ujenzi wa kituo cha TEHAMA katika kampasi ya Arusha na kuanza ujenzi wa jengo la taaluma na maktaba katika kampasi ya Songea.

81. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2023/24, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini kimepanga kukamilisha ujenzi wa bweni la wanafunzi na ukumbi wa mihadhara na kuanza ujenzi wa jengo la utawala katika kampasi ya Dodoma, kuanza ujenzi wa kituo cha mafunzo katika eneo la Nala Dodoma, kukamilisha ujenzi wa bweni, maktaba na kuanza ujenzi wa bweni la wanafunzi katika Kituo cha Mafunzo - Mwanza. Aidha, chuo kinatarajia kufanya tafiti 10 na kutoa huduma za ushauri elekezi kwa kuzingatia mahitaji ya wadau.

82. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/24, Taasisi ya Uhasibu Tanzania itaendelea na ujenzi wa jengo moja (1) linalojumuisha ukumbi wa mihadhara, maabara ya kompyuta na maktaba katika Kampasi ya Mbeya, jengo la taaluma Misungwi - Mwanza, vyumba vya madarasa manne (4), maktaba, maabara ya kompyuta na nyumba ya watumishi na hosteli mbili (2) za wanafunzi wa kike na wa kiume kampasi ya Mtwara, jengo la taaluma katika kampasi ya Kigoma na kuanza ujenzi wa jengo la taaluma katika kampasi ya Zanzibar.

83. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/24, Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika kimepanga kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala, kuendeleza wahadhiri 28 na kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 20.

4.3.2 Bodi za Kitaaluma na Kitaalamu

84. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/24, Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu inatarajia kusajili wahasibu 1,350 katika ngazi mbalimbali, kuanza ujenzi wa ofisi ya Makao Makuu Jijini Dodoma, kufanya ukaguzi wa ubora wa uandaaji wa taarifa za fedha kwa taasisi 75, kufanya ukaguzi wa ubora wa kampuni 65 za ukaguzi, kuendesha mitihani ya kitaaluma kwa watahiniwa 12,500 na kutoa mafunzo ya diploma ya viwango vya uandaaji wa taarifa za fedha serikalini kwa watahiniwa 350. Aidha, Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi inatarajia kusajili wataalamu 3,500 wa ununuzi na ugavi, kuendesha mafunzo na ushauri wa kitaalamu kwa wataalamu 6,500 na kuendesha mitihani ya kitaaluma kwa watahiniwa 4,000.

4.3.3 Taasisi za Usimamizi wa Masuala ya Kodi

85. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/24, Mamlaka ya Mapato Tanzania inatarajia kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya jumla ya shilingi trilioni 26.7, kuendelea kuimarisha na kuboresha mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato, kuwajengea uwezo wafanyakazi, kutoa elimu ya kodi na kuendelea kudhibiti uvujaji na upotevu wa mapato. Aidha, Bodi ya Rufaa za Kodi, Baraza la Rufaa za Kodi na Ofisi ya Usuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi zinatarajia kupokea, kusikiliza na kutolea maamuzi mashauri, malalamiko na taarifa za kodi kutoka kwa walipakodi na wadau wa kodi. Vilevile, Ofisi ya Usuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu huduma zinazotolewa na ofisi hiyo.

4.3.4 Bodi ya Michezo ya kubahatisha

86. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/24, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha inatarajia kutoa leseni 11,880 kwa waendesha michezo ya kubahatisha, ambapo 2,273 ni leseni mpya na 9,607 ni leseni zitakazohuishwa, kufanya ukaguzi kwa waendesha michezo ya kubahatisha 101 na kusimamia uendeshaji wa Bahati Nasibu ya Taifa.

4.3.5 Taasisi za Usimamizi wa Masoko ya Mitaji, Dhamana na Bidhaa

87. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2023/24, Mamlaka ya Usimamizi wa Masoko ya Mitaji na Dhamana imepanga kuanzisha bidhaa mpya za masoko ya mitaji, kufanya mapitio ya kanuni na miongozo ya utoaji wa bidhaa katika masoko ya mitaji na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masoko ya mitaji na bidhaa. Aidha, Baraza la Rufaa za Masoko ya Mitaji linatarajia kuanza kupokea, kusikiliza na kutoa maamuzi kuhusu migogoro ya masoko ya mitaji. Vilevile, Soko la Bidhaa Tanzania linatarajia kuendelea na ujenzi wa jengo la ofisi Jijini Dar es salaam pamoja na kuendelea kuhamasisha matumizi ya mfumo wa soko wa kielektroniki ili kuongeza idadi ya bidhaa zinazouzwa na kununuliwa kupitia mfumo huo.

4.3.6 Taasisi za Benki

88. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2023/24, Benki Kuu ya Tanzania imepanga kukuza wastani wa ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) kwa kiwango kisichopungua asilimia 10 ili kuendana na mahitaji ya shughuli za kiuchumi, kuboresha mazingira ya kuchochea ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi, kudhibiti na kupunguza kiwango cha mikopo chechefu pamoja na kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosheleza mahitaji ya kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

89. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2023, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania imepanga kuzalisha mapato ya shilingi bilioni 45.1 kukuza faida ya benki kabla ya kodi ya shilingi bilioni 18.5, kutoa mikopo ya shilingi bilioni 336.7, kukuza mali za benki ili kufikia shilingi bilioni 562.7 na kufuatilia urejeshaji wa mikopo kutoka kwa wateja shilingi bilioni 62.

90. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2023, Benki ya Maendeleo ya TIB imepanga kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 51 kwa miradi ya maendeleo kwenye sekta za maji, nishati na uongezaji thamani mazao ya kilimo, kukusanya shilingi bilioni 39.6 za marejesho ya mikopo kutoka kwa wateja, kukusanya shilingi bilioni 57 za marejesho ya mikopo iliyoshindikana na kuondolewa kwenye mizania ya benki.

91. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023, Benki ya Biashara Tanzania imepanga kuzalisha mapato ya shilingi bilioni 184.2, kukuza faida ya benki kabla ya kodi ya shilingi bilioni 12.4, kutoa mikopo ya shilingi bilioni 904, kukusanya amana za wateja shilingi bilioni 1,121, kukuza mali za benki ili kufikia shilingi bilioni 1,446, kukuza mtaji kufikia shilingi bilioni 123.8 na kuunda mfumo wa kielektroniki wa tathmini na ufuatiliaji wa mwenendo wa mikopo inayotolewa na benki.

4.3.7 Taasisi za Bima

92. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2023/24, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania inatarajia kufanya uchambuzi wa mikataba ya bima mtawanyo kwa kampuni 32, kufanya ukaguzi wa wadau wa bima, kuandaa mwongozo wa bima za kilimo, kuhamasisha kampuni za bima kuandaa bidhaa za sekta ya kilimo pamoja na kupokea na kushughulikia malalamiko ya wateja wa bima. Aidha, Shirika la Taifa la Bima linatarajia kukamilisha taratibu za kupata uthibitisho wa cheti cha ubora cha utoaji huduma kwa wateja (ISO 9001 2015), kuongeza wateja wapya 116 wa bidhaa za taasisi na kubuni bidhaa tatu (3) mpya zitakazokidhi mahitaji ya soko.

4.3.8 Taasisi za Uwekezaji na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

93. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/24, Kampuni ya Uwekezaji wa Pamoja - UTT AMIS inatarajia kuongeza rasilimali za mifuko kwa kiwango cha asilimia 15, kuongeza idadi ya wawekezaji kwa asilimia 5 na kuhamasisha Taasisi za Serikali, Mifuko ya Hifadhi za Jamii, Mashirika na vikundi mbalimbali vya kijamii kama vile SACCOS kujiunga na mifuko ya UTT AMIS. Aidha, Mfuko wa SELF unatarajia kutoa mikopo yenye masharti nafuu ya shilingi bilioni 44.8 kwa wajasiriamali 38,000, kufuatilia urejeshaji wa mikopo usipungue asilimia 95 na kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa walengwa au wanufaika 5,500.

4.3.9 Usimamizi wa Takwimu Rasmi

94. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/24, Ofisi ya Taifa ya Takwimu inatarajia kusambaza matokeo ya sensa ya watu na makazi, kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi ya takwimu za sensa na kuendelea kuandaa taarifa za sensa za kisekta kulingana na ratiba ya kazi zinazotakiwa kufanyika baada ya zoezi la sensa kukamilika. Aidha, ofisi inatarajia kufanya tafiti za kitaalamu kuhusu watu wenye uwezo wa kufanya kazi, mapato na matumizi ya kaya binafsi, ajira, mapato na ustawi wa watoto katika jamii.

4.3.10 Usimamizi wa Ununuzi wa Umma

95. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/24, Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma inatarajia kuendelea na ujenzi wa ofisi za Makao Makuu Jijini Dodoma, ujenzi wa mfumo wa ununuzi wa umma kwa njia ya mtandao awamu ya pili, kutoa mafunzo kwa watumishi 2,000 kutoka katika taasisi nunuzi 1,000 na wazabuni 5,000 kuhusu mfumo mpya wa ununuzi wa umma kwa njia ya kielektroniki na Sheria ya Ununuzi wa Umma, kufanya kaguzi za thamani ya fedha katika taasisi nunuzi 85 na kaguzi za ukidhi wa sheria kwa taasisi nunuzi 300 na kufanya mapitio ya nyaraka zote sanifu za zabuni.

96. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/24, Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini unatarajia kuanza ujenzi wa ofisi ya mkoa wa Kigoma, ofisi na kituo cha mafuta katika mikoa ya Njombe na Arusha pamoja na Wilaya ya Kahama, Korogwe na Masasi. Aidha, Wakala umepanga kuboresha na kuhuisha mfumo wa GIMIS ili kuwezesha matumizi ya kadi katika huduma za ununuzi wa mafuta na kufanya upembuzi yakinifu ili kubaini uwezekano na mahitaji ya kuunganisha mfumo wa GIMIS na pampu, pamoja na tanki za mafuta. Vilevile, Mamlaka ya Rufaa za Zabuni imepanga kutoa mafunzo kwa wajumbe, wafanyakazi wa mamlaka, wazabuni na taasisi nunuzi kuhusu utumiaji wa mfumo wa kielektroniki wa kusajili na kusimamia rufaa zitokanazo na michakato ya ununuzi wa umma.

4.4 Makadirio ya Matumizi kwa Mafungu ya Wizara pamoja na Fungu 45-Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2023/24.

97. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2023/24, Wizara ya Fedha na Mipango inaomba ridhaa ya Bunge lako Tukufu ya kutumia jumla ya shilingi trilioni 15.94 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mafungu yake tisa (9) ya kibajeti. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 15.38 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 564.22 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe shilingi bilioni 97.13 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 87.72 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 9.41 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa bajeti kwa kila fungu la Wizara na Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na.1.

Jedwali Na.1: Mchanganuo wa Bajeti ya Mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2023/24

| FUNGU | JINA LA FUNGU | MATUMIZI YA KAWAIDA | | | MATUMIZI YA MAENDELEO | | | JUMLA KUU |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA | NDANI | NJE | JUMLA YA FEDHA ZA MAENDELEO | |
| 1 | Deni la Serikali | - | 10,480,130,968,000 | 10,480,130,968,000 | - | - | - | 10,480,130,968,000 |
| 6 | Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali | 1,948,234,000 | 7,618,770,000 | 9,567,004,000 | 360,000,000 | - | 360,000,000 | 9,927,004,000 |
| 7 | Ofisi ya Msajili wa Hazina | 5,229,041,000 | 37,591,275,000 | 42,820,316,000 | 940,000,000 | - | 940,000,000 | 43,760,316,000 |
| 10 | Tume ya Pamoja ya Fedha | 813,300,000 | 2,650,549,000 | 3,463,849,000 | - | - | - | 3,463,849,000 |
| 13 | Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu | - | 3,861,365,000 | 3,861,365,000 | - | 455,000,000 | 455,000,000 | 4,316,365,000 |
| 21 | Hazina | 1,610,820,134,000 | 745,547,085,000 | 2,356,367,219,000 | 464,263,182,000 | 33,493,393,000 | 497,756,575,000 | 2,854,123,794,000 |
| 22 | Huduma Nyinginezo | 13,065,211,000 | 2,301,774,127,000 | 2,314,839,338,000 | - | - | - | 2,314,839,338,000 |
| 23 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 7,157,764,000 | 51,029,321,000 | 58,187,085,000 | 1,880,000,000 | - | 1,880,000,000 | 60,067,085,000 |
| 50 | Wizara ya Fedha na Mipango | 54,120,209,000 | 52,703,766,000.00 | 106,823,975,000 | 22,758,347,000 | 40,075,572,000 | 62,833,919,000 | 169,657,894,000 |
| | JUMLA YA MAFUNGU YA WIZARA | 1,693,153,893,000 | 13,682,907,226,000 | 15,376,061,119,000 | 490,201,529,000 | 74,023,965,000 | 564,225,494,000 | 15,940,286,613,000 |
| 45 | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi | 16,891,720,000 | 70,830,676,000 | 87,722,396,000 | 8,828,000,000 | 583,878,000 | 9,411,878,000 | 97,134,274,000 |
| | JUMLA YA MAFUNGU YOTE | | | | | | | 16,037,420,887,000 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

**5.0 HITIMISHO**.

98. Mheshimiwa Spika, kabla sijahitimisha hoja yangu, napenda kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Hamad Hassan Chande (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushauri na ushirikiano anaoendelea kunipatia katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, nawashukuru watendaji wakuu wa wizara na taasisi zake wakiongozwa na Dkt. Natu E. Mwamba, Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Naibu Makatibu Wakuu Bi. Amina Kh. Shaaban, Bi. Jenifa C. Omolo na Bw. Lawrence N. Mafuru kwa ushauri na usimamizi madhubuti wa majukumu ya wizara na taasisi zake. Vilevile, nawashukuru wakuu wa idara, vitengo na wafanyakazi wote wa wizara na taasisi zake kwa utekelezaji mzuri wa mikakati ya maendeleo, ushauri pamoja na ushirikiano wao mahiri katika kufanikisha majukumu yangu ya kila siku. Asanteni sana na Kazi Iendelee.

99. Mheshimiwa Spika, napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali inaendelea na maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Zoezi hili ni muhimu kwa nchi ili kupata mwongozo thabiti wa kisera utakaosaidia katika uandaaji na utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo kwa Taifa letu katika kipindi cha miaka 25 ijayo baada ya Dira ya sasa kufikia ukomo mwaka 2025. Hivyo, napenda kutoa wito kwa waheshimiwa wabunge kuhamasisha wapiga kura wetu na watanzania wote kwa ujumla, kujitokeza kwa wingi kutoa maoni yao kwa timu zitakazokuwa zinakusanya maoni katika maeneo yao.

100. Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda nikushukuru tena wewe kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha hoja hii ndani ya Bunge lako Tukufu pamoja na waheshimiwa wabunge wote na umma wa watanzania kwa ujumla kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni www.mof.go.tz.

101. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

AFYA

TANZANIA NA SIKU YA MTOTO AFRIKA...

# Rais 'damu damu' nao kutetea afya zao, agawa mshahara kuwanusuru

Na Mwandishi Wetu




Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika hafla ya kuzindua mfumo wa usafirishaji watoto wachanga 'M- Mama' mjini Dodoma. **PICHA: MTANDAO**

SIKU tisa zijazo inatimu kilele cha maadhimisho Siku ya Mtoto wa Afrika, ambayo chimbuko lake ni historia ya mauaji dhidi yao katika mji wa Soweto, Juni 16 mwaka 1976, baada ya watoto kuandamana kudai haki zao za elimu, dhidi ya serikali iliyokuwa ya ubaguzi wa rangi.

Afrika yote ikacharuka wakati huo vuguvugu la kudai uhuru lilikuwa juu, baadhi ya nchi kama Msumbiji zikiwa na mwaka mmoja wa uhuru.

Nchini Tanzania, ni tukio lililoukera umma ukiongozwa na Baba wa Taifa, Rais Julius Nyerere, kwa hisia hiyo akiungwa mkono kwa namna nyingi, ikiwamo bendi maarufu ya muziki wa dansi ya Urafiki, maarufu 'Wana- Chakakua' ikitunga kibao chenye hisia kali kukemea kilichotokea.

Daima suala la kumtetea mtoto halijawahi kusahaulika, akikumbukwa Mwalimu Nyerere, kuna wakati akahoji katika hotuba yake akitamka "Philosophically (kifalsafa) inanipa tabu, kwanini mtoto mdogo anafariki?"

Ni katika mwendelezo huo wa kumpenda mtoto, mwaka 2009 katika utawala awamu ya nne nchini, kukatungwa Sheria ya Mtoto Tanzania, inayolenga kumlinda na kumtetea mtoto na ndio inayotumika hadi sasa.

Kupitia awamu tofauti za uongozi wa nchi, kumekuwapo na uamuzi unaolea na kuboresha ustawi, haki na ulinzi wa mtoto na ndio maana, sasa kunashuhudiwa huduma za bure katika elimu hadi kidato cha nne, uzazi, pia watoto katika umri mdogo, mengine yakiwa yameamuliwa kisera, pia kitikadi nchini.

### KINACHOENDELEA SASA

Wakati anakabidhiwa kiti kuwa Rais, mara moja Dk. Samia Suluhu Hassan akapatiwa jina 'Mama' kwa maana ya wajihi wake kijinsia, historia ya nchi, pia matarajio ya uzazi kiutawala.

Ndicho kinachotawala katika miaka miwili na 'ushee' wa utawala wa Rais Dk. Samia, akiwa katika mazingira ya ushirikiano wa 'umama'na umma anauongoza ukisimama katika wasifu 'mtoto.'

Dhana 'mama ni mama' ikajitokeza katika mkasa siku aliposimama na kumpisha kiti Georgina Magesa, mtoto mwenye umri miaka nane, akimruhusu akae, Rais Dk. Samia, akuifikia hatua hiyo, baada ya kuona makala fupi ya mtoto huyo iliyorushwa kwenye televisheni, akielezea ndoto zake za kutamani siku moja akawa Rais wa Tanzania.

Katika mkasa unaofanana na huo, mtoto mwingine aliyekuwa katika matibabu kwenye Hospitali ya Taifa Muhimbili akidhaminiwa na Rais Dk. Samia, hata alipipata nafuu akaomba akarejeshe shukurani, tukio ambalo alipowa fursa ya kurejesha shukurani kwa 'mama', akaishia kwenye bumbuwazi la furaha iliyoangukia katika kilio cha 'ahsante.'

Vilevile, katika tukio, la 'umama' linalojitokeza upande wa pili, kwa simulizi ya wito kutoka kwa Filomena Chale, mkazi wa London, mjini Songea, akimwomba Rais Dk. Samia msaada wa shilingi milioni 1.5 za matibabu ya mjukuu Karen Mwingira.

Hiyo ni anayesumbuliwa na tatizo la kichwa, matibabu yanayotakiwa kufanyika katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Dar es Salaam, akiamini rais huyo ni nguzo ya msaada wake.

Katika mtazamo wake, mnamo Julai mwaka jana akifungua jengo jipya la Huduma ya Afya ya Mama na Mtoto katika Hospitali ya CCBRT, Dar es Salaam, Rais Dk. Samia, akawataka wauguzi nchini kuacha dharau kwa wajawazito, kuwaepushia na vifo vinavyozuilika.

Dk. Samia akasema lengo la ujenzi wa jengo hilo ni kumpatia mwanamke huduma bora ya uzazi tangu ujauzito, kujifungua na hatua ya uangalizi wa mtoto mchanga.

Hapo akataja mikakati ya kuboresha huduma kwa wajawazito na watoto wachanga, kwamba Wizara ya Afya, inashirikiana na vyama vya madaktari bingwa wa magonjwa ya kinamama na uzazi, wakianzisha mfumo wa kupitia takwimu za vifo vya mama na watoto, wakati wa kujifungua.

Pia akaelekeza mamlaka za kiserikali kuhakikisha madaktari bingwa wanakuwapo katika ngazi ya hospitali za wilaya, ili huduma hizo zipatikane kirahisi.

Maelekezo yake kwa Wizara ya Afya, ni kuhakikisha hospitali hiyo inafikia uwezo wa kuhudumia wanawake 300 kwa siku, iwe na jumla ya vitanda 140 na vyumba vinane ya kinamama kujifungua, hata kupata uwezo wa kuwachunguza mapema na kuwatibu watoto waliozaliwa na ulemavu.

Anasema, kuwapo hospitali hiyo ni utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa 2021/2022 - 2025/2026 wa kupunguza vifo vya uzazi kutoka vifo 321 kwa kila vizazi 100,000 hadi vifo 220.

### ATOA MSHAHARA WAKE

Unasaba wa Rais na watoto nchi mwake unamea katika hatua pale anajitoa zaidi, mwaka jana alipoamua kuchangia fedha zake Sh. milioni 15 kwa Mtoto Ali Kimara (10), ambaye amekuwa akisumbuliwa na changamoto ya kupumua kwa takribani miaka nane, hadi wakati huo.

Mnamo Julai mwaka jana, miezi minne tangu achangie Sh. milioni 15, mara nyingine Dk. Samia akachangia fedha za mshahara wake Sh. milioni 70 kwa asasi ya Doris Mollel Foundation, akiwa mkoani Kigoma, kuhudumia watoto.

> **Kuwapo hospitali hiyo ni utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa 2021/2022 – 2025/2026 wa kupunguza vifo vya uzazi kutoka vifo 321 kwa kila vizazi 100,000 hadi vifo 220.**

Ni fedha ambazo mgawanyiko wake, Sh. milioni 20 akazitoa kuwasaidia watoto waliozaliwa njiti kupitia shirika hilo lisilo la kiserikali, huku kiasi cha Sh. milioni 50 zikienda kununua vifaa tiba vya kuwasaidia watoto hao.

Akitoa shukrani zake, mama wa mtoto njiti, Halima Mathayo anamshukuru Rais Dk. Samia kwa kuboresha huduma za afya nchini, hasa kwa kinamama kwa kutoa zawadi zinazohudumia na kuwalea watoto wao.

"Rais Samia amewashika mkono kinamama waliojifungua watoto njiti kwa kutoa mashuka, blanketi, vitenge, sabuni, pampasi, mafuta ya nywele na mahaitaji mengine, ikiwa ni pamoja ba vyakula kama mchele na sukari," anatamka Waziri Angella Kairuki, mwaka jana akiwa katika Hospitali ya Rufani Maweni, mjini Kigoma.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, katika tuko hilo akatoa ahadi ya serikali kuwaletea vifaa tiba kwa ajili ya kuhudumia watoto njiti, akiorodhesha mashine za kufua hewa ya oksijeni, mashine za kuzalisha hewa joto na zile za kutunza watoto njiti.

Ni hoja inayopokewa na Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa Maweni, Dk. Stanley Binagi, anayesema vifaa tiba na mahitaji hayo, itasaidia utoaji wa huduma bora kwa watoto njiti waliopo na watakaozaliwa katika hospitali hapo.

AFYA

# Msako wa Bodi ya Nyama 'bucha na bucha' hadi kufika machinjioni

## • Madudu kibao, zipo bubu, nyama ya kutu...



Shughuli ya kukagua nyama mjini Mpanda ikiendelea. **PICHA: NEEMA HUSSEIN**

**Na Neema Hussein,** MPANDA

Ni hivi karibuni, Bodi ya Nyama Kanda ya Magharibi, imefanya ukaguzi kuhusu usajili na utambuzi wa wadau katika tasnia ya nyama mkoani Katavi.

Hiyo inatajwa ni kuendelea kusisitiza uzingatiaji Sheria ya Mwaka 2006, inayowataka wafanyabiashara wa wanyama kulinda afya za walaji. Ni ukaguzi unaofanyika, huku bodi hiyo ikihitimisha kazi hiyo katika mkoa wa Katavi, kwa kuwapitia wadau mbalimbali wa tasnia ya nyama kuwakagua.

Hapo wanajumuishwa wanenepeshaji, wamiliki wa machinjio, wamiliki wa minada, pia mabucha, pamoja na wafanyabiashara wa mifugo na wengineo katika mnyororo wa thamani wa nyama na mazao yake.

**OFISA WA BODI**

Joseph Kulwa, ni Ofisa Mfawidhi wa Bodi ya Nyama Kanda ya Magharibi, anasema kitu walichokibaini ni wadau kutofuata sheria ya tasnia ya nyama.

"Sheria hiyo bado hawaitii, hawafuati maelekezo yaliyopo. Cha kwanza, sheria inawataka wadau wasajiliwe na watambulike, lakini tumezunguka jana na leo tumebaini kuna takribani mabucha sita ambayo yamefunguliwa kinyume na taratibu, yaani mabucha bubu.

"Hayo mabucha ni ya watu ambao kwanza ni wadau wetu, lakini wameongeza 'udau' kwa kuongeza biashara ya mabucha, hivyo wanafanya biashara kinyume kwa kutosajiliwa.



"Cha pili, tulichokibaini wadau wetu bado wanaendelea kutotii maelekezo ya sheria yalivyo, kwa kwenda kinyume na utaratibu. Bado mabucha ni machafu, bado upimaji wa afya ni tatizo, bado matumizi ya magogo yapo, matumizi ya nondo chafu na uuzaji nyama ambazo hazijakaguliwa machinjioni.

"Kama tunavyofahamu, sheria hii inataka mnyama akaguliwe machinjioni na auzwe buchani, kwa hiyo hii bado ni changamoto kwa wadau wetu. Kwa hiyo, tunatoa elimu pale inapolazimu tunawapiga faini, ili pengine kuwakumbusha kwamba ni takwa la kisheria, wanatakiwa wafuate utaratibu kadri ya sheria ilivyo.

"Machinjio yetu ya Mpanda hoteli naweza sema wanafanya maboresho, japo bado mapungufu yapo, kama vile matumizi ya nondo chafu machinjioni, kutokuwa na vyoo ambavyo havina sifa, lakini uzio unajengwa, japo haujakamilika, hakuna ofisi za wafanyakazi, pia hakuna utaratibu wa watu kuingia machinjioni.

"Yule ambaye anatakiwa kuingia machinjioni, ni ambaye anafanya shughuli za kuchakata mnyama na mazao yake kama vile utumbo na bidhaa nyingine za nyama, lakini unaona kabisa machinjio inaruhusu wadau mbalimbali. Ni kwa sababu ya kutokuwa na uzio.

"Uzio pia una umuhimu kuzuia wanyama wanaoingia machinjioni kama vile mbwa, fisi, ndege wasiofaa kuingia machinjioni. Tunashukuru kwamba, Manispaa (Mpanda)_ wamiliki wa machinjio wanajitahidi kujenga uzio, hivyo tunawaomba wakamilishe haraka.

"Hatua ambazo kama Bodi ya Nyama tumezichukua, tutaandika wito wa onyo kwa mmiliki, lakini tutatoa kusudio la kufunga machinjio, endapo yale tulioyabaini hayatatekelezwa.

"Wito wangu kwa wadau walio kwenye tasnia ya nyama, watii sheria bila shuruti, watii sheria ya tasnia ya nyama, hakuna sababu ya kukaa tunafungiana, hakuna sababu ya kutozana faini, wayafuate yale ambayo sisi wakaguzi mara nyingi tunawaelekeza.

"Mara nyingi tunavyofanya ukaguzi huu tunakuwa waungwana, tunawaambia hili hapana! Tunawapa muda, sasa kama hawatekelezi, tunalazimika kufunga na kuwapiga faini," amatamka Kulwa na anaendelea:

> **"** Tuliambiwa kuweka vyuma vya aluminiami tuwe na jokofu ndani, kwa hiyo hiyo hata nyama ikilala haiharibiki haraka na vyuma havitengenezi kutu, tofauti na vile vya zamani.

**MSIMAMIZI MACHINJIO**

Juma Gilibert, Msimamizi wa Machinjio ya Mpanda Hoteli, anasema kwa upande wa Manispaa, kwa machinjio changamoto kubwa kwao imekuwa kukosekana uzio.

"Kulingana na upatikanaji bajeti, tumekuwa tukipanga kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya machinjio, ikiwa ni pamoja na kuanza ujenzi wa uzio kama unavyoona (yanajengwa) bado sehemu kidogo tu kumalizia, ambao muda si mrefu tutamalizia.

"Tatizo jingine lilikuwa ufinyu wa sehemu ya kuchinjia, hivyo serikali ilitoa fedha tukatanua sehemu ya kuchinjia, serikali imeendelea kutenga bajeti, ili kuendelea kuboresha miundombinu mingine kama vile ofisi na banda la ngozi," anasema Juma.

**MUUZA NYAMA**

Frank Mwita ni mfanyabiashara wa nyama soko Kuu la Mpanda anasema biashara kwa sasa si mbaya kutokana na uboreshwaji wa mabucha ikilinganishwa na awali mabucha mengi yalikuwa machafu.

"Tuliambiwa kuweka vyuma vya aluminiami tuwe na jokofu ndani, kwa hiyo hiyo hata nyama ikilala haiharibiki haraka na vyuma havitengenezi kutu, tofauti na vile vya zamani," anasema Frank.

Muuzaji mwingine, Hussein Aniseti, anasema hana vyuma, hivyo kutokana na changamoto ya havipatikani Mpanda, inamfanya aviagize kutoka Dar es Salaam na sasa anaahidi kutekeleza maagizo aliyopewa na mamlaka, kuwa na vyuma visivyoweka kutu, hata kuharibu nyama.



## Serikali yatia saini mkataba tathmini athari kimazingira

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

SERIKALI imetia saini mkataba kwa ajili ya kufanya tathmini ya athari ya kimazingira na kijamii kwa lengo la ununuzi wa meli za uvuvi, kupitia mpango wa kuendeleza kilimo na uvuvi (AFDP).

Akizungumza baada ya hafla ya kutia saini mkataba huo, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Dk. Jim Yonaz alisema, mkataba huo utawezesha kufanyika kwa tathmini ya athari ya mazingira pamoja na matengenezo ya meli zitakazotumika katika uvuvi wa bahari kuu ili kupata mazao ya bahari yatakayochangia katika uchumi wa nchi.

Dk. Yonaz alisema, katika tathmini hiyo pia utafanyika upembuzi yakinifu kuundwa kwa vyombo hivyo na kazi itakayofanyika kwa muda wa siku 75 itagharimu Sh. milioni 349.

Alisisitiza watakaokabidhiwa jukumu la kufanya kazi hiyo waifanye kwa umakini ikiwamo kusimamia kwa weledi utekelezaji huo.

"Tanzania tunazo rasilimali nyingi za majini, sasa ili kuhakikisha tunainua uchumi kupitia uchumi wa buluu, serikali imeona ni muhimu kutengeneza meli kubwa zitakazovua katika kina kirefu ili kupata mazao ya bahari," alisema Dk. Yonazi.

Alisema, meli nne zitatengenezwa kwa ajili ya Zanzibar na tano kwa Tanzania Bara, kukamilika kwake kutasaidia kuinua uchumi wa taifa na wananchi kwa ujumla.

Pia aliwahimiza wadau wa uvuvi ambao ni Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) na Shirika la Uvuvi la Zanzibar (ZAFICO), kushirikiana na mkandarasi huyo ili kazi hiyo ifanyike kikamilifu huku akihimiza kila mmoja kuwajibika kwa sehemu yake kwa lengo la kupata matokeo chanya.

Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Ushauri wa masuala ya Mazingira (TANSEQ), Lusako Raphael, amebainisha lengo la kufanya tathmini hiyo ni kuhakikisha mradi hausababishi athari za mazingira.

"Mradi huu unalenga kuwezesha ununuzi wa meli pamoja na uanzishwaji wa viwanda vya kuchakata samaki hivyo tunategemea kupata ushirikiano kutoka kwa wadau wote kama ZAFICO, TAFICO na Wizara ya Kilimo," alisema Raphael.

# RITA yaanza kutoa mafunzo uandishi wosia

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

WAKALA wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), umeanzisha huduma ya kutoa mafunzo ya uandishi na utunzaji wa wosia ambayo inalenga kupunguza tatizo la migogoro ya familia itokanayo na ndugu wa marehemu kugombania mali na kusababisha mauaji.

Ofisa Msajili wa RITA, Emmy Masunga, alibainisha hayo jana jijini hapo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu huduma mbalimbali zinazotolewa na wakala huo kwenye maadhimisho ya miaka mitano tangu kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Alisema, wakala huo ulianzisha huduma ya ushauri, kuandika na kuhifadhi wosia baada ya kubaini kuongezeka kwa tatizo la wajane na watoto kupoteza mali za marehemu ambaye hakuacha wosia.

"Hii imesababisha hata watoto wengine kushindwa kuendelea na masomo na familia kushindwa kupata mahitaji muhimu," alisema Masunga.

Aidha, aliwataka Watanzania kujenga tabia ya kuandika wosia wanapokuwa hai ili kuwaondolea shida

**"Wito wetu kwa watu wote kuona umuhimu wa kuandika wosia wanapokuwa hai ili kuwasaidia watoto wao kupata haki zao tofauti na ilivyo sasa ambapo pamekuwa na matukio mengi ya familia kupotea haki zao kutokana na ndugu kupokonya mali za wajane na watoto wa marehemu," alisema.**

wategemezi wao wanapofariki dunia.

"Wito wetu kwa watu wote kuona umuhimu wa kuandika wosia wanapokuwa hai ili kuwasaidia watoto wao kupata haki zao tofauti na ilivyo sasa ambapo pamekuwa na matukio mengi ya familia kupotea haki zao kutokana na ndugu kupokonya mali za wajane na watoto wa marehemu," alisema.

Pia Msajili huyo aliwataka Watanzania kuondokana na imani potofu kuwa mtu akiandika wosia anajitabiria kifo, watumie fursa hiyo kwa ajili ya manufaa ya familia zao kupata kile wanachostahili wakati wanapokuwa hawapo duniani na anayo nafasi ya kufanya marekebisho kila mara anapohitaji.

Alisema faida za kuandika wosia ni kuepusha watoto au mke/mume kunyang'anywa mali na kumwezesha mwandishi kumchagua msimamizi wa mirathi.

"Pia inaepusha migogoro katika familia ndugu au jamaa, unakupa uhakika wa maisha bora ya baadaye ya warithi wako kulingana na mali ulizonazo, kupunguza usumbufu na gharama wakati wa kuendesha mirathi," alifafanua.

Kadhalika, alisema taarifa zinazopaswa kuandikwa kwenye wosia ni pamoja na msimamizi wa mirathi, wapi mtoa wosia angependa azikwe, idadi ya mali za marehemu na mgawanyo wa mali za marehemu.

"Zipo aina mbili za wosia ambazo ni wa maandishi na wa matamshi/mdomo na anayetakiwa kuandika ni mwananchi yeyote awe na umri wa miaka 18 na kuendelea, awe na akili timamu, wosia uwe wa maandishi au matamishi, ushuhudiwe na watu wanne ukiwa ni wa matamshi, wosia usimnyime mrithi halali wa mali bila sababu zinazotambulika kisheria na uwe umeshuhudiwa na mwanasheria," alisema.

Pia alisema RITA imeanzisha mfumo wa kutoa huduma kidijitali unaofahamika kama eRITA ambao unamwezesha mtu yeyote kupata huduma sehemu yoyote kwa kutumia simu yake ya mkononi.

"Mfumo huu unamwezesha mwananchi kupata huduma ya cheti cha kuzaliwa, kifo pamoja na udhamini kupitia simu yake ya mkononi na anaweza kupata cheti chake katika ofisi yoyote ya RITA iliyopo jirani yake," alisema.



Mwenyekiti wa Machifu wa Mkoa wa Dodoma, Mtemi Bilenje Yasin Ally (katikati), akizungumza jijini Dodoma jana, wakati wa kikao cha kamati ya maandalizi ya tamasha la kimkoa la machifu linalotarajiwa kufanyika Septemba mwaka huu. Wengine ni mlezi wa machifu wa mkoa huo, Mohamed Keba (kushoto), Katibu wa machifu Mkoa, Ndahani Chinagh'anagh'a (wa pili kulia). **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Serukamba aagiza h'shauri kuweka mafundi wengi kwenye miradi

**Na Thobias Mwanakatwe, IKUNGI**

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, amewaagiza maofisa manunuzi katika halmashauri za wilaya mkoani hapa kuweka mafundi wengi kwenye miradi inayotekelezwa kwa kutumia mwongozo wa 'Force Account' badala ya kutoa zabuni kwa mkandarasi mmoja na kusababisha miradi kuchelewa kukamilika.

Serukamba, alitoa agizo hilo jana alipokuwa Wilaya ya Ikungi, katika mfululizo wa ziara ya kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo na kuhimiza ikamilike kabla ya Juni 30, mwaka huu.

"Maofisa manunuzi muache kutoa zabuni za ujenzi wa miradi kwa mkandarasi mmoja pale mradi husika unapofanywa kwa njia ya force account kwani tunaongeza gharama pasipo sababu yoyote na wengi wa makandarasi hao wanachelewesha ukamilikaji kutokana na kuwa na kazi nyingi," alisema.

Serukamba alisema utekelezaji wa miradi kwa 'force account' baada ya kuunda zile kamati tatu wanaweza kuitwa mafundi zaidi ya 10 na kushindanishwa kwa bei kulingana na ujenzi unaofanyika na yule atakayeonekana kuwa na bei ya chini ndio anayepewa kazi.

"Hii habari ya kumtafuta fundi mmoja mkubwa apewe kazi yote yeye na kulipwa fedha zote halafu aanze kutafuta mafundi mara nyingi kazi hiyo inakuwa haikamiliki kwa wakati na haraka kutokana na kuwa na kazi nyingi," alisema.

Alisema ukamilishaji wa miradi kwa njia ya force account ni miradi kufanyika kwa haraka na kupunguza gharama ya ujenzi na faida nyingine watakuwapo wananchi ambao watajitolea na kuwa kazi kubwa ya madiwani ni kuwahamasisha wananchi kujitokeza kujitolea.

Aidha, aliwaomba wahandisi kwenda kutembelea na kukagua miradi inapotekelezwa kwa kuwa uzoefu unaonesha kuwa hawaendi inapofanywa kwa njia ya 'force account' wakiamini kazi hiyo haiwahusu bali inafanywa na kamati zilizoundwa.

Serukamba alisema Rais Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa ya kutoa fedha nyingi kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo na aliomba ikamilishwe kwa viwango vinavyotakiwa na kwa thamani halisi na sio vinginevyo.



# Kesi anayetuhumiwa kumnajisi mtoto wake wa miaka 9 yaendelea

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

MAHAKAMA ya Hakimu Mfawidhi Mkoa wa Mbeya, imeendelea kusikiliza kesi ya unajisi inayomkabili mwanamume mkazi wa Kata ya Ilemi, akituhumiwa kumbaka na kumwingilia kinyume cha maumbile mtoto wake wa miaka tisa.

Shahidi upande wa Jamhuri, Erica Petro, ambaye ni mfanyabiashara aliiambia mahakama kuwa akiwa katika eneo lake la biashara Lyoto alifikiwa na dereva bodaboda asiyemfahamu akiwa amembeba mtoto akiuliza endapo anamfahamu.

Shahidi Erica aliiambia mahakama kwa kuwa alikuwa anamfahamu mtoto huyo aliambatana na dereva bodaboda aliyemleta hadi nyumbani kwa wazazi wake ambapo baada ya kuhojiwa alidai alikutwa Iwambi na bodaboda huyo akitembea kuelekea kwa bibi yake wilayani Mbozi, mkoani Songwe, akidai kubakwa na baba yake na kutishiwa kupigwa na kuuawa ikiwa atamwambia mtu yeyote.

Shahidi huyo alidai, mama mzazi wa mtoto huyo aliendа kituo cha kutolea huduma ili kumfanyia vipimo mwanawe huyo na kubainika kubakwa na kuingiliwa kinyume cha kimaumbile.

Alipopewa nafasi ya kuhoji maswali kwa shahidi huyo mshtakiwa jina limehifadhiwa (45), alihoji kwanini mtoto huyo akutwe Iwambi ikiwa kweli alibakwa, lakini upande wa Jamhuri kupitia shahidi Erica Petro alidai alikutwa akitembea kwenda Mbozi ili kuepuka kadhia ya kunajisiwa na baba yake mzazi.

Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Emelda Aluko na mwenzake George Ngwembe, waliiomba mahakama kuahirisha kesi hiyo hadi tarehe nyingine kwa ajili ya kuhitimisha ushahidi wao kisha kufunga shauri lao.

Hakimu Mfawidhi, Mkoa wa Mbeya katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya, Zawadi Laizer anayesikiliza kesi hiyo aliahirisha shauri hilo namba 6/2023 hadi Juni 13, 2023 na mshtakiwa amerudishwa mahabusu hadi siku ya kesi.

Mshtakiwa huyo ambaye ni mfanyabiashara, ameshtakiwa kwa makosa mawili ya ubakaji kinyume na kifungu namba 130 (1), (2) (e) na 131 (1), (3) sura ya 16 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2022 na kulawiti kinyume na kifungu namba 154 (1) (a) na (2) sura ya 16 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2022.



Mkuu wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Juma Irando (wa nne kulia), akipata maelezo kutoka kwa Katibu wa kikundi cha Wazo Jipya Bakery, Michael Seng'enge (kushoto), alipokagua mradi wa vijana utakaopitiwa na mbio za Mwenge wa Uhuru Juni 11, mwaka huu. Kikundi hicho, kimekopeshwa Sh. milioni 20 kutoka fedha za asilimia 10 za halmashauri. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Walioiba vibao vya anwani za makazi mtaani matatani

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ameagiza watendaji wa kata, vijiji na maofisa tarafa kufanya msako na kuwakamata wananchi wote waliohusika kuiba vibao vya anwani za makazi vilivyowekwa kwenye mitaa mbalimbali mkoani humo.

Alitoa agizo hilo juzi alipopokea ripoti ya uchambuzi ya Sensa ya Watu na Makazi kwa Mkoa wa Mbeya ambayo ilihusisha viongozi mbalimbali wa mkoa huo na timu ya wataalamu waliohusika kwenye mchakato wa kukamilisha kazi hiyo.

Alisema, baadhi ya maeneo vibao vimeng'olewa na watu wasiokuwa waadilifu na kwenda kuviuza kama vyuma chakavu na wengine kuweka katika ofisi zao.

"Tayari watu wameanza kung'oa vibao kwenye mitaa yao na kwenda kuviuza kama vyuma chakavu ili wajipatie pesa sasa naagiza watendaji wote na maofisa tarafa kushughulikia suala hili, najua mnawafahamu na mtawakamata nendeni mkalitekeleze hili ili liwe fundisho kwa wengine kwa sababu wanatuhujumu," alisema Homera.

Aidha, alisema kitendo hicho kinakwamisha jitihada za serikali kurahisisha mawasiliano kwa kuwa kuondolewa kwa vibao hivyo kutasababisha wageni kushindwa kufika maeneo wanayokusudia. Akizungumzia matokeo ya sensa kwa Mkoa wa Mbeya, Homera alisema 2022 idadi ya watu imekuwa 2,343,754 ikilinganishwa na mwaka 2012 iliyokuwa 1,708,548 sawa na ongezeko la 635,206.

Alisema, ongezeko hilo ni sawa na asilimia 3.2 ambao sasa mkoa utaweka mipango madhubuti kwa ajili ya kukamilisha shughuli za miradi ya maendeleo.

"Takwimu hizi zitasaidia kuongeza uwazi ili wawe na uelewa wa matumizi ya matokeo ya sensa kwa ajili ya kutoa michango yao ya maendeleo ya taifa na kushauri namna bora ya kuyapima," alisema Homera.

Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Dormohamed Issa, alisema jiji hilo limeandaa mipango kabambe kwa ajili ya kuwasaidia wananchi kwa kuzingatia idadi ya watu.

Aliwaomba wananchi kuishauri serikali namna bora ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo na kusisitiza kutoa ushirikiano ili ikamilike kwa wakati.

# TARI yafanya majaribio aina 10 mbegu za mpunga

**Na Grace Mwakalinga, MBARALI**

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Kituo cha Uyole imefanya majaribio ya aina 10 za mbegu za mpunga zenye uwezo wa kukomaa ndani ya muda mfupi, kuhimili magonjwa na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa lengo la kuongeza tija kwa wakulima.

Hatua hiyo imekuja baada ya kuripotiwa uwapo wa ugonjwa kwenye zao la mpunga wilayani Mbarali ambao unapunguza uzalishaji.

Mkurugenzi wa TARI, Kituo cha Uyole, Dk. Dennis Tippe alisema utafiti wa mbegu hizo unalenga kutatua vikwazo vinavyowakabili wakulima wa zao hilo ikiwamo mabadiliko ya tabianchi na magonjwa yanayosababisha uzalishaji duni wa zao hilo.

"Kwa muda mrefu imekuwapo mbegu inayotumiwa na wakulima wa mpunga wilayani hapa, lakini kadri siku zinavyoenda uzalishaji unapungua, kwasababu ya kuchafuka kwa mbegu na kupoteza ubora kutokana na kudumu kwa muda mrefu hivyo serikali imekuja na mbegu hizi ambazo zitaleta matokeo chanya kwa wakulima," alisema Dk. Tippe.

Alivishauri vikundi vya wakulima wa mpunga kuwa na utaratibu wa kupeleka mahitaji ya kupima afya ya udongo kwa wataalamu wa kilimo ili kuwasaidia kuweka mbolea sahihi na kwa virutubisho vinavyostahili ili kuboresha kilimo cha mpunga.

Mmoja wa wakulima wilayani Mbarali, Fidelis Mlowe, alisema tayari wamefanya majaribio ya kupanda mbegu hizo na zimeonesha matokeo chanya baada ya mazao yao kustawi vizuri hatua ambayo inaleta matumaini ya kuvuna mavuno mengi.

"Tunashukuru serikali kupitia TARI walitupatia mbegu aina 10 ili tupate mbegu sahihi na baada ya kupanda, mbegu nyingine zimetoa machipukizi 36 hadi 50 hizi mbegu zinaonekana zinafanya vizuri sana," alisema Fidelis Mlowe.

Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Abbas Mubanga, aliwataka wakulima wa mpunga, kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa kilimo ili waweze kuzalisha mazao kwa tija pamoja na kulinda ubora wa mazao yao sokoni.

"Serikali kupitia wataalamu wake inafanya jitihada nyingi kuhakikisha sekta ya kilimo inaleta ukombozi wa kiuchumi kwa wakulima, lakini pia sekta hii inakabiliwa na vikwazo mbalimbali ikiwamo mabadiliko ya tabianchi hivyo tuache kulima kwa mazoea, tuwashirikishe wataalamu wetu ili tukabiliane na mabadiliko hayo na tuvune kwa tija," alisema Mlowe.

# Serikali yabaini matumizi ya kuni kutumika kwa siri

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harous Said Suleiman, amesema matumizi ya nishati ya kuni yanaendelea kufanyika kwa siri katika maeneo ya serikali licha ya elimu inayotolewa ya kulinda na kuhifadhi mazingira kuonekana baadhi ya wananchi wanaojali maslahi yao zaidi kuliko ya taifa.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Pandani, Omar Fakihi Hamad, aliyetaka kujua lini serikali itaanzisha rasmi kampeni maalum kwa ajili ya upandaji miti pembezoni mwa fukwe na ya misitu Unguja na Pemba.

Alisema serikali imo katika maandalizi makubwa ya mpango wa kitaifa wa kuirithisha Zanzibar ya Kijani (Zanzibar Green Legacy Program), ikiwa ni kampeni maalum kwa ajili ya upandaji na utunzaji wa miti maeneo tofauti, mijini na vijijini ikiwamo maeneo ya fukwe.

Alisema lengo ni kuirudisha miti ya asili ya matunda na misitu iliyotoweka kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo za uharibifu wa mazingira Unguja na Pemba.

Kadhalika, utaratibu uliopo wa kupata ruhusa ya kukata miti ni kwanza kupata kibali kutoka Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, kupitia Idara ya Misitu na mwombaji hutakiwa kujaza fomu ya maombi, ambayo hupitia kwa Sheha na wilaya husika.

Aidha, baada ya kujiridhisha kibali cha kukata mti au miti hiyo hutolewa na gharama ya Sh. 2,500 hutolewa kwa kibali cha kukata mti, huingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Mapato ya Serikali.

Alisema katika utekelezaji wa mpango wa kuirudisha Zanzibar ya Kijani, miongoni mwa vipaumbele vyake ni kuimarisha upatikanaji wa nishati mbadala.

"Shabaha kuu ni kuhakikisha kuwa asilimia 90 ya kaya zote nne Zanzibar na watumiaji wote wakubwa wa kuni wanatumia nishati mbadala (LPG au biogesi),"alisema.

# Serikali: Uzalishaji wa samaki waongezeka zaidi tani 14,000

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WIZARA ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar, imesema uzalishaji wa samaki umeongezeka kutoka tani 47,111 mwaka 2021 hadi tani 61,794 kwa mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 31.

Akiwalisha makadirio, mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Waziri wa wizara hiyo, Masoud Suleiman Makame alisema uzalishaji wa samaki kwa mwaka 2021 ulikuwa na thamani ya Shilingi 237,148,468,042 kulinganisha na uzalishaji wa samaki kwa mwaka 2022 wenye thamani ya Shilingi 391,370,146,212.

Alisema kwa mwaka 2022 wastani wa thamani ya samaki kwa kilo moja ilikuwa ni Shilingi 6,333 na mchango wa sekta ya uvuvi kwa thamani ya Pato la Taifa umeongezeka kutoka Sh. bilioni 236.8 kwa mwaka 2021 hadi kufikia Sh. bilioni 243.0 kwa mwaka 2022.

"Usafirishaji wa mazao ya baharini ikiwamo matango bahari, mwani, dagaa, kaa na pweza umeongezeka kutoka tani 19,063 mwaka 2021 hadi tani 23,158 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 21," alisema.

**a Sh. bilioni 6.2 (sawa na asilimia 115 ya makadirio ya kukusanya Shilingi bilioni 5.4 kwa mwaka), ikilinganishwa na leseni 25 zilizotolewa katika kipindi kilichopita na zilizokusanya jumla ya Sh. bilioni 3.3," alisema.**

Alisema, uzalishaji wa mwani umeongezeka kutoka tani 10,531 mwaka 2021 hadi tani 12,594 kwa mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 20.

Aidha, alisema usafirishaji wa mwani nje ya nchi umeongezeka kutoka tani 12,124 mwaka 2021 hadi tani 13,972 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 15.

Akizungumzia uvuvi wa bahari kuu, alisema hadi kufikia Aprili 2023, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (Deep Sea Fishing Authority - DSFA) ilikuwa imetoa leseni za uvuvi wa bahari kuu 48.

Alisema kati ya hizo, leseni tatu zilikuwa ni kwa meli za ndani na leseni 45 zilitolewa kwa meli za uvuvi za nje na vibali vya kuvua nje ya mipaka ya ukanda wa uchumi wa bahari ya Tanzania (Areas Beyond National Jurisdiction) kwa meli saidizi (supply vessels) tano pia vilitolewa.

"Kwa ujumla mamlaka ilikusanya Sh. bilioni 6.2 (sawa na asilimia 115 ya makadirio ya kukusanya Shilingi bilioni 5.4 kwa mwaka), ikilinganishwa na leseni 25 zilizotolewa katika kipindi kilichopita na zilizokusanya jumla ya Sh. bilioni 3.3," alisema.

Hata hivyo, alisema kuimarika kwa makusanyo yatokanayo na leseni kwa uvuvi wa bahari kuu kunatokana na juhudi za makusudi zilizofanywa na viongozi wakuu wa kitaifa ikiwa ni pamoja na kuweka mazingira rafiki ya kuvutia uwekezaji yaliyopo katika sheria ya uendelezaji na usimamizi wa uvuvi wa Bahari Kuu.

Pia Masoud alisema wizara, kupitia kampuni ya uvuvi (ZAFICO), tayari ipo katika mchakato wa ujenzi wa kiwanda cha kusarifu dagaa huko Kama, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, ikiwa ni pamoja na utengenezaji wa chanja maalum za kuanikia dagaa bora na litakalokuwa na bei ya ushindani katika masoko ya kimataifa.

Alisema tayari ZAFICO imejenga kituo cha ugani cha kuelimisha njia bora na za kisasa za uchemshaji, ukaushaji, uhifadhi, usindikaji na utayarishaji wa bidhaa za dagaa.

Alisema katika hatua za awali, wajasiriamali 90 wamepatiwa mafunzo ya uanikaji dagaa.



Mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi (wa tatu kulia), akiongoza matembezi ya kilomita 5 ya kuadhimisha Siku ya Usalama wa Chakula Duniani yaliyoanzia eneo la Mombasa hadi Mapinduzi Square, Kisonge jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Kilimo cha vanila kuwakomboa wakulima kimataifa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

ZAO la vanila limetajwa kuwa na uwezo wa kuwakomboa wakulima na kuingia katika uzalishaji wa kimataifa kutokana na bei yake kuendelea kutawala katika masoko ya biashara ya kimataifa nje ya nchi.

Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, alisema hayo wakati akitoa ufafanuzi na kujibu hoja za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kuhusu mikakati ya wizara katika kushajihisha wakulima kulima kilimo cha mazao ya viungo.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na kwamba wizara kupitia taasisi ya utafiti ya mazao ya Kizimbani, imeanza kutoa elimu na kuwafikia wakulima kuhusu mbinu za kisasa za uzalishaji wa mazao ya viungo katika mageuzi ya kibiashara.

Alisema zao la vanila kwa sasa soko lake ni kubwa nje ya nchi na wakulima wanaweza kupata mafanikio makubwa.

Alisema wizara inashirikiana na Jumuiya ya Ulaya (EU), kuwasaidia wakulima kuwapatia elimu na mbinu za kisasa katika kulima mazao ya viungo ya vanila ikiwamo kuwapatia mbegu bure.

Alisema mradi huo tayari umeanza kupata mafanikio makubwa na zaidi ya wakulima 3,000 wamefikiwa kwa kupatiwa elimu na mgawo wa mbegu za zao hilo pamoja na pilipili manga.

Aliwataja wakulima wa Kizimbani Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja pamoja na Machuwi na Kiboje, Wilaya ya Kati Unguja, kuhamasika na kuongoza kuchangamkia fursa za mazao ya viungo.

"Tunashirikiana na Wizara ya Biashara katika kuwashajihisha wakulima wetu kulima mazao ya viungo ambayo soko lake lipo kubwa la uhakika nje ya nchi," alisema.

Mazao ya viungo ambayo wakulima wameanza kushajihishwa kulima kwa wingi ikiwamo vanila, pilipili manga, pilipili kichaa, iliki, uzile na mdalasini ambayo yote yanastawi vizuri katika ardhi ya visiwa vya Unguja na Pemba.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

NDUGU **YASSIN ELIASA TEIKWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba ya usajili **T444ATC** aina ya **SCANIA** rangi ya multcolor yenye Chasis **No.9047729** na Engine **No.1465201** na kadi ya Trailler yenye namba ya usajili **T736AXV** Rangi Multcolor. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi namba **DOD/DOD/RB/192985/2023**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 16 OF 2023**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE SAMWEL MAKANGE MNJOKAVA**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LATER OF ADMINISTRATION**

**BY JULIUS SAMWEL MAKANGE AND RASHID SAMWEL MAKANGE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules GN 369 OF 1963)**

ALL PERSON claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner. Objections to the grant should be field on or before the 06 day of July, 2023.

Dated at Korogwe this 06 day of June, 2023.

DISTRICT COURT KOROGWE TANZANIA
DISTRICT COURT KOROGWE
RESIDENT MAGISTRATE KOROGWE DISTRICT

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA MADAI NAMBA 9 YA MWAKA 2020**
**GREEN DIAMOND JOINT STOCK CO. ...........MDAI**
**DHIDI YA**
**TATA AFRICA HOLDING (T) CO. .........................KWA:**
**GREEN DIAMOND JOINT STOCK CO. – DAR ES SALAAM**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mdai aliyetajwa hapo juu amefungua shauri dhidi yako, shauri ambalo maelezo yake yameelezwa katika nakala za hati ya madai zinazopatikana katika Mahakama hii, unatakiwa kuhudhuria katika Mahakama hii, wewe mwenyewe au wakili au mwakilishi wako ambaye anaruhusiwa kisheria siku ya tarehe 09/06/2023 saa tatu (3:00) asubuhi mbele ya Mhe. E. E. KAKOLAKI, kujibu madai hayo dhidi yako. Unaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo unatarajiwa kuvitumia katika utetezi wako siku hiyo.

**ANGALIA:** Kama usipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikathibitisha kuwa umepokea taarifa hii ya kuitwa shaurini, basi shauri linaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila uwepo wako.

HATI hii imetolewa kwa MKONO wangu na CHAPA ya Mahakama leo hii tarehe 17 Mwezi 05, 2023.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU
KANDA YA DAR ES SALAAM

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HEMED IDD KIMERA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili **T 629 DCT** aina ya **TOYOTA PREMIO**. Chassis namba **NZT2405016576.** Engine namba **1NZFE865Z242FY.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **IRI/IRI/RB/188729/2023.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**D. BAKKER** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili **T 980 AGW** aina ya **TOYOTA Hilux.** Chassis No. **LN650050781.** ENGINE **NO 2L1357**632. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **ARU/ARU/RB/194297/2023**.

---

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**FREDRICK HEBERT LYAM** anatangaza kupotelewa na za pikipiki zenye namba za usajili **MC 507 AZL, MC 166 BFV, MC 400 BHR, 545 BXX (Toyo).** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/URA/RB/186024/2023.**

---

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**FREDRICK HEBERT LYAM** anatangaza kupotelewa na za pikipiki zenye namba za usajili **MC 463 ARV, MC 600 AUM, MC 504 AUX, MC 204 AYT (Toyo).** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/URA/RB/186024/2023.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**
**MAOMBI NAMBA 39 YA 2023**

**AZIZA IDD MAHUNGULA.....MUOMBAJI**
**JUMA SHOMARI KUNGUGU**
**MAIZA ALMASI MAHUNGULA....MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**

**JUMA SHOMARI KUNGUGU** Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Morogoro tarehe **28/6/2023** mbele ya Mwenyekiti M.Khasim wewe mwenyewe binafsi au utume mwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

Imetolewa kwa **MKONO** wangu na **MUHURI** wa Baraza leo tarehe **02, mwezi juni, 2023**

M.Khasim
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MOROGORO

---

**FORM NO. 58**
**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE**
**OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO. 31 OF 2023**

**In Matter of the Estate of the Late**
**TASIANA HAMZA MWENEGOHA**

**By 1. EMMANUEL FERNUS LYMO**
**2. .................................**

All Persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or latter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the HON.T KANIKI day of **20/06 / 2023.**

Dated at **Morogoro**, this **17** day of **04, 2023**

RESIDENT MAGISTRATE

---

## TANGAZO LA KADI YA GARI ILIYOPOTEA GEITA

**DEOGRATIAS NICOLAS HAULE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 948 DXQ.** NAMBA YA ENGINE; **2AZEAABB154.** CHASSIS NAMBA; **ACU2000BB154.** AINA YA GARI; TOYOTA KLUGER. RANGI YA GARI; NYEUSI. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **GEI/GEI/RB/191817/2023.**

---

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0677020701**
**E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**
**WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.





# Kituo cha Afya Ketumbeine chapatiwa vifaa tiba

**Na Allan Isack, ARUSHA**

HATIMAYE tatizo la muda mrefu la kukosekana kwa vifaa tiba maalumu vya kumpima mgonjwa kabla ya kumfanyia upasuaji, lililokuwa likikabili Kituo cha Afya cha Ketumbeine, Wilaya ya Longido mkoani Arusha, limepatiwa ufumbuzi.

Wahitaji wa huduma hiyo hasa wajawazito walikuwa wakihangaika kwenda Hospitali ya Wilaya ya Longido, kutafuta huduma nje ya kituo hicho.

Jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NCBA, Claver Serumaga, akizungumza wakati wa hafla ya makabidhiano ya vifaa tiba hivyo, alisema wameguswa kukisaidia kituo hicho kutokana na gharama kubwa wanazotumia wananchi wengi wa jamii ya kifugaji ya Kimasai kufuata vipimo hivyo Hospitali ya Wilaya.

Kwa mujibu wa Serumaga, vifaa tiba hivyo vina thamani ya zaidi ya Sh. milioni tatu.

"Walihitaji vifaa kwa ajili ya upasuaji kwa wajawazito pamoja na kitanda cha uchunguzi wa kimatibabu kwa wagonjwa. NCBA tumesema tutaendelea kushirikiana na wadau wengine ili kuunganisha nguvu kusaidia mahitaji mengine yanayohitajika," alisema.

Vifaa hivyo ambavyo ni kitanda maalum cha kumpima mgonjwa kabla ya daktari kufanya upasuaji na seti ya vifaa vya upasuaji, vilikabidhiwa kwa Katibu Tawala Msaidizi, Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha, anayeshughulikia afya, Dk. Silvia Mamkwe.

Baada ya makabidhiano hayo, Mkuu wa Divisheni ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe wa Wilaya ya Longido, Dk. Seleman Mtenjela, alisema msaada huo utakwenda kupunguza adha kwa wagonjwa kufuata huduma mbali na kuongeza juhudi zinazofanywa na serikali.

"Tulipokea vifaa hivi karibuni lakini bado tuna upungufu ikiwamo vya vitanda vya uuguzi na vya upasuaji. Vifaa hivi tulivyopokea vinakwenda kuokoa kinamama ambao huenda walitakiwa kusafiri kilomita 60 kwenda kupata huduma ya upasuaji nje ya Ketumbeine," alieleza Dk. Mtenjela.

Mganga Mfawidhi wa Kituo hicho, Dk. Frank Kimbwereza, aliishukuru Benki ya NCBA kwa msaada huo ambao utakwenda kuokoa maisha ya mama na mtoto akisema awali wajawazito walipopewa uhamisho wa kwenda hospitali nyingine walipata shida.

**"Walihitaji vifaa kwa ajili ya upasuaji kwa wajawazito pamoja na kitanda cha uchunguzi wa kimatibabu kwa wagonjwa. NCBA tumesema tutaendelea kushirikiana na wadau..."**

# Jalada la kesi tuhuma mwanafunzi kunajisiwa latua kwa Gwajima

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

JALADA la kesi ya tuhuma za mwanafunzi wa darasa la nne mkoani Manyara kunajisiwa, limepelekwa kwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima.

Mwanafunzi huyo (jina limehifadhiwa), anadaiwa kunajisiwa miezi saba iliyopita lakini kesi yake haijapelekwa mahakamani hadi sasa huku sababu za kukwama kwake zikiwa hazijawekwa wazi.

Akizungumza na Nipashe, mama mzazi wa mtoto huyo, Mwajuma Mwiru, Mkazi wa Negamsi, Wilaya ya Babati, alimwomba Waziri Gwajima kuingilia kati suala hilo ili mtoto wake akapate haki mahakamani.

"Namwomba Waziri Gwajima na mamlaka za serikali, kulisukuma Jeshi la Polisi Manyara, kupeleka mahakamani kesi ya mwanangu ambaye alinajisiwa na mpangaji wa mjomba wake (mpwa). Alifanya kitendo hicho wakati tukiwa kwenye dua iliyofanyika nyumbani kwa mjomba wake.

**"Mimi nilibaini kuwa mtoto wangu amelawitiwa (kunajisiwa) baada ya kuitwa na mlezi wa kituo kinachoendeshwa na Shirika la Compassion International.**

Aidha, mama huyo ameziomba mamlaka za serikali mkoani humo kumsaidia mtoto wake kupata uhamisho wa shule, kwa kuwa hivi sasa anapata unyanyapaa kutoka kwa wenzake wanaomzomea.

"Mimi nilibaini kuwa mtoto wangu amelawitiwa (kunajisiwa) baada ya kuitwa na mlezi wa kituo kinachoendeshwa na Shirika la Compassion International.

"Nilipoambiwa mtoto wangu ameharibiwa, nilisononeka sana mpaka nilianguka njiani wakati narudi nyumbani. Nilimpeleka Hospitali ya Mkoa na alifanyiwa vipimo na ikathibitika amelawitiwa na ameambikizwa Virusi Vya Ukimwi (VVU)."

Alifafanua kuwa toka mtoto wake amefanyiwa ukatili huo Novemba mwaka jana kesi bado haijaenda mahakamani mpaka sasa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi, George Katabazi, alipotafutwa kutoa ufafanuzi kuhusu tuhuma hizo alisema, jambo hilo halijui ila atamwagiza Mkuu wa Upelelezi wa Mkoa na Wilaya hiyo, kufanya ufuatiliaji wa haraka ili kupata ukweli juu ya jambo hilo.

Alisema: "Nimeagiza wafanye hivyo na wanipe mrejesho. Nimeagiza wapelelezi wa kesi hiyo wabadilishwe na wasiwe na mawasiliano juu ya jambo hilo."




Rebeca Mushi mkazi wa Kisongo jijini Arusha, akinunua simu kwa njia ya mkopo alipotembelea banda la Tigo, kwenye maonyesho ya Kili Fair yaliyofanyika viwanja vya Magereza mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hujuma Bwawa la Boloti zamvuruga DC

**Na Godfrey Mushi,** HAI

HUJUMA dhidi ya serikali inayofanywa kwa makusudi na watu wanaoendesha shughuli za kiuchumi katika Bwawa la Boloti lililoko Kijiji cha Kyuu, Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, 'zimemvuruga' Mkuu wa Wilaya hiyo, Amir Mkalipa.

Mkalipa alisema kuna watu wanaofanya hujuma hizo kwa ajili ya kujinufaisha wao na kufifisha jitihada za serikali kupitia Bodi ya Bonde la Mto Pangani ambayo imepewa jukumu la kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji.

Alikuwa akizungumza jana na wakazi wa vijiji vya Kyuu, Mungushi na Nkwansira wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani.

"Hili bwawa kwa mujibu wa sheria, Tanzania tuna mabonde sita na sisi mkoa wetu tuko kwenye Mamlaka ya Bonde la Pangani. Sasa wana alama zao wameweka mwisho wa eneo la kufanya kazi; kuna wanaofanya shughuli za kibinadamu, hilo jambo hatuwezi kuliruhusu.

"Nimesikia kuna mtu mmoja ameng'oa bicon ya Pangani (alama za mipaka), ni mwiko, ole wake. Mwananchi wa aina hiyo, salama yake ni kubadilisha hiyo tabia ya mwenendo wa namna hiyo."

Utafiti uliofanywa na serikali kwa kushirikiana na Japan mwaka 1990, unaonyesha kuwa bwawa hilo lina uwezo wa kuhifadhi maji ya kumwagilia zaidi ya ekari 500 katika vijiji vya Sanya Station, Rundugai, Kware na Mungushi.

Mkuu wa Divisheni ya Mazingira, Wilaya ya Hai, Lucas Njegite, alisema pia katika Bwawa la Boloti, baadhi ya watu wamevamia bwawa hilo na kuharibu ikolojia yake kwa asilimia 60.

Vilevile, alisema ili kudhibiti uharibifu huo, serikali na wadau mbalimbali wa mazingira wameanza jitihada za kunusuru chanzo hicho, kwa kupanda miti zaidi ya 9,000 kuzunguka bwawa hilo.

## HABARI MICHEZO

# NTIBAZONKIZA AVUNJA REKODI ILIYODUMU MIAKA 15 LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa Simba, Saido Ntibazonkiza amevunja rekodi iliyodumu kwa miaka 15 ya kufunga mabao matano katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Polisi Tanzania iliyokuwa inashikiliwa na straika, Nsa Job, aliyekuwa Azam FC.

**Ntibazonkiza pia ana rekodi ya kufunga 'hat-trick' mbili msimu huu kama alivyowahi kufanya Job.**

Mrundi huyo ambaye alisajiliwa na Simba kipindi cha dirisha dogo, aliiwezesha timu yake kushinda mabao 6-1, mechi ya raundi ya 29 iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam na kufikisha mabao 15, akibakisha moja tu kumfikia, Fiston Mayele wa Yanga.

"Nashukuru timu yangu kwa kupata matokeo mazuri na mimi kufunga mabao matano, kikubwa siangalii sana ufungaji bora, ninachoangalia ni timu kwanza kupata matokeo bora halafu vitu vingine tunaangalia baadaye, Fiston (Mayele) ni mchezaji mzuri na mfungaji mzuri, kama ikitokea nikifanikiwa kuwa mfungaji bora nitafurahi na kumshukuru Mungu," alisema kiungo huyo.

Ntibazonkiza alipachika mabao hayo dakika ya 15, 20, 27, 79 na 89, ikiwa ni 'hat-trick' yake ya pili msimu huu ambao unamalizika kesho, ya kwanza akiifunga Desemba 30, mwaka jana kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Mnyama akiwachapa Tanzania Prisons mabao 7-1.

Mabao hayo alifunga dakika ya 61, 63 na 70, katika mechi ambayo pia nahodha wa Simba, John Bocco, pia alipiga 'hat-trick'.

Inakuwa ni 'hat-trick' ya sita katika Ligi Kuu msimu huu, nyingine zikiwekwa na Bocco (mbili), moja kwenye mechi dhidi ya Ruvu Shooting mechi ikichezwa Novemba 19, mwaka jana Simba ikishinda mabao 4-1.

Mayele alipiga hat trick yake kwenye mechi ya iliyochezwa Novemba 17, mwaka jana, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Yanga ikiifunga Singida Big Stars mabao 4-1, na Ibrahim Mkoko wa Namungo aliyefunga katika mechi dhidi ya KMC, timu yake ikishinda magoli 3-1.

Mara ya mwisho mchezaji kufunga mabao matano kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ilikuwa ni Machi 24, mwaka 2009, msimu wa 2008/09, iliyowekwa na Job, akifunga dakika ya 21, 24, 51, 79 na 87, Azam ikiishindilia Villa Squad magoli 6-2.

Msimu wa Ligi Kuu Bara 2022/2023 unatarajiwa kumalizika kesho kwa timu zote kushuka dimbani wakati tayari Ruvu Shooting na Polisi Tanzania zimeshashuka daraja.



Kiungo mshambuliaji wa Simba, Saido Ntibazonkiza (kushoto), akishangilia pamoja na nahodha wa timu hiyo, John Bocco, baada ya kufunga hat-trick katika mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Polisi Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi. Simba ilishinda mabao 6-1. **PICHA: SIMBA SC**

## TFF, NBC yatambulisha kombe jipya

**Na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF) kwa kushirikiana na wadhamini wakuu wa Ligi Kuu Bara, Benki ya NBC, wametambulisha rasmi kombe jipya atakalokabidhiwa bingwa wa ligi hiyo kwa msimu wa mwaka 2022/2023.

Tayari Yanga ya Dar es Salaam ilishatwaa ubingwa huo ikiwa na michezo miwili mkononi huku nafasi ya pili ikishikwa na watani zao, Simba.

Akizungumza katika hafla fupi ya uzinduzi wa kombe hilo jana, Meneja wa Fedha wa Bodi ya Ligi, Ibrahim Mayela, alisema uzinduzi huo umefanyika baada ya kupokea maoni mbalimbali ya wadau ambao waliyafanyia kazi.

Mayela alisema ubora wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo sasa iko katika nafasi ya tano kwenye viwango vya Afrika pia umepelekea ubora wa kombe uongezeke.

"Msimu uliopita tulifanya mchakato wa kupokea maoni kutoka kwa wadau kuhusu maboresho mbalimbali ya kombe, sasa tumefanikiwa na tunatambulisha kombe hilo ambalo lina viwango bora kama ilivyo kwa ubora wa Ligi ya Tanzania," alisema Mayela.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Mahusiano kwa Umma wa NBC, Godwin Semunyu, alisema waliamua kubadilisha kombe na kununua jipya na lenye mvuto kwa sababu ya ubora wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

## Vita Ligi Kuu Bara yahamia 'Play Off'

**Na Adam Fungamwango**

TOFAUTI na msimu uliopita, raundi moja kabla Ligi Kuu Tanzania Bara kumalizika, vita imehamia katika timu zinazopigana kuepuka kucheza 'play off', huku sehemu zote zilizobaki kila timu ikivuna ilichopanda.

Baada ya mechi zilizochezwa juzi, rasmi Polisi Tanzania imeungana na Ruvu Shooting kushuka daraja, bingwa akiwa ni Yanga huku pia wawakilishi wa Tanzania Bara katika michuano ya kimataifa, timu nne zimejulikana.

Macho na masikio ya mashabiki sasa kesho ili kufahamu timu zipi zitaangukia kucheza mechi za mchujo dhidi ya timu za Ligi ya Championship, Mashujaa FC ya Kigoma.

Timu tano ambazo ni KMC, Mbeya City, Coastal Union, Mtibwa Sugar na Dodoma Jiji zinaonekana zipo katika hatari zaidi ya kwenda kucheza 'play off' kutokana na nafasi zao kwenye msimamo wa ligi.

KMC itakuwa ugenini kucheza dhidi ya Mbeya City, Mtibwa Sugar watawakaribisha Geita Gold, Dodoma Jiji itacheza dhidi ya Ruvu Shooting, na Coastal Union itakuwa Azam Complex kuwakabili Simba.

## Klabu bingwa netiboli yanukia

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya Klabu Bingwa Taifa ya Netiboli yamepangwa kufanyika kuanzia Juni 20 hadi 29, mwaka huu jijini Dar es Salaam, imefahamika.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa Chama cha Netiboli Tanzania (CHANETA), Rose Mkisi (pichani), alisema mashindano hayo yatashirikisha timu 21 kutoka mikoa ya Tanzania Bara.

Mkisi alisema maandalizi kuelekea katika mashindano hayo yanaendelea vyema na chama kinawaomba wadau mbalimbali kujitokeza kudhamini michuano hiyo ili ifanyike kwa ufanisi.



"Tumewaandikia barua wadau wetu mbalimbali kuwaomba watuunge mkono ili tufanikishe jambo letu, tunataka kuona netiboli inarudi kama ilivyokuwa zamani, tunawakumbusha netiboli au michezo si uhuni," alisema Mkisi.

Aliongeza kwa kuwataka wanawake kujiunga kushiriki michezo kwa sababu inajenga afya na inasaidia kutoa ajira lakini mashabiki kujitokeza kushangilia wakati wa michuano.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### TIELEMANS ANUKIA VILLA

KLABU ya Aston Villa imeingia katika kinyang'anyiro cha kumsajili mchezaji huru, Youri Tielemans, mwenye umri wa miaka 26, baada ya kiungo huyo wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji kuondoka Leicester City. ***(Athletic)***

### VIEGA AGOMBEWA ULAYA

CHELSEA imeungana na Barcelona pamoja na Liverpool katika mbio za kumwania kiungo wa Celta Vigo ya Hispania, Gabri Veiga. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 ana kifungu cha kuachiwa cha pauni milioni 34.4. ***(Guardian)***

### MAGUIRE ATAKIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur imeonyesha nia ya kumnunua mlinzi wa Manchester United na England, Harry Maguire, mwenye umri wa miaka 30, na inatumaini inaweza kumshawishi mchezaji mwenzake wa kimataifa, Harry Kane kusalia katika klabu hiyo. ***(Telegraph)***

### WANANE KUUZWA UNITED

MANCHESTER United inataka kuwauza wachezaji wanane msimu huu akiwamo nahodha, Harry Maguire, mshambuliaji, Anthony Martial, mwenye miaka 27, viungo Fred na Scott McTominay, kipa, Dean Henderson na mabeki, Alex Telles, Eric Bailly na Brandon Williams. ***(Mirror)***

### WAARABU WAMTAKA ZAHA

MSHAMBULIAJI wa Crystal Palace na Ivory Coast ambaye mkataba wake umeisha, Wilfried Zaha, mwenye umri wa miaka 30 amepokea ofa ya pauni milioni 15 kwa mwaka ili kuungana na Cristiano Ronaldo katika klabu ya Al-Nassr ya Saudi Arabia. Atletico Madrid pia wanavutiwa na mchezaji huyo. ***(Sky Sports)***

### KANTE MSHAHARA MNONO

KIUNGO wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Ufaransa, N'Golo Kante, mwenye umri wa miaka 32 atapewa mshahara ambao unaweza kufikia pauni milioni 86.2 kwa mwaka na klabu za Saudi Al-Ittihad na Al-Nassr. ***(Guardian)***

### WEAH AKARIBIA JUVENTUS

MSHAMBULIAJI wa Lille na Timu ya Taifa ya Marekani, Timothy Weah, mwenye umri wa miaka 23, anaweza kuwa karibu na uhamisho wa pauni milioni 8.6 kwenda Juventus. ***(Goal)***

### COLWILL AWEKWA SOKONI

KLABU ya Brighton inafanya tathmini ya dau lililoboreshwa la pauni milioni 40 kwa ajili ya kumnunua mlinzi wa Chelsea mwenye umri wa miaka 20, Levi Colwill. ***(Mail)***

### DAHOUD KUTUA BRIGHTON

BRIGHTON inatarajiwa kutangaza kuwasili kwa kiungo wa kati wa Ujerumani, Mahmoud Dahoud, 27 kutoka Borussia Dortmund kwa uhamisho wa bure. ***(Football Insider)***

### WEST HAM YASAKA VIUNGO

KLABU ya West Ham inawafuatilia viungo watatu, James Ward-Prowse mwenye umri wa miaka 28 wa Southampton, Conor Gallagher (23) na Scott McTominay (26). ***(Football Transfers)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HAZARD APANGA KUSTAAFU SOKA

**MADRID,** Hispania

**Uamuzi wa winga huyo aliyeamua kuondoka Madrid umesababishwa na...**

NYOTA wa zamani wa Lile, Chelsea na Real Madrid, Eden Hazard, anapanga kustaafu kabisa kucheza mpira wa miguu ingawa ana ofa mezani kutoka Ligi Kuu ya Marekani, kwa mujibu wa ESPN.

**Kwa mujibu wa ripoti, Klabu ya Vancouver Whitecaps ya Canada ambayo inashiriki Ligi Kuu Marekani (MLS), inamwania mchezaji huyo.**

Hazard mapema wiki hii alifikia muafaka wa kuvunja mkataba wake na Real Madrid ya Hispania, baada ya kukumbwa na majeruhi ya mara kwa mara tangu alipotua hapo akitokea Chelsea.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa zamani wa Ubelgiji hakuwa na wakati mzuri tangu alipojiunga na vigogo hao wa Hispania, Real Madrid na hilo lilisababisha kumfanya kutokupata nafasi ya kucheza hadi kufikia hatua ya kuondoka klabuni hapo.

Hazard amevunja mkataba na Real Madrid kwa makubaliano ya pande zote mbili na hiyo inatokana na mchezaji huyo kutokuona dira ya maendeleo yake ndani ya timu hiyo.

Hivyo mchezaji huyo inaelezwa amepanga kustaafu kabisa kucheza mpira baada ya kuondoka klabuni hapo.

Hazard amekuwa mchezaji bora kwa miaka mingi haswa kipindi akiitumikia Chelsea ya England.

Lakini mambo yalibadilika alipojiunga na Real Madrid mwaka 2018 na kuanza kuandamwa na majeraha na kumfanya kupotea kabisa katika ramani ya soka.

Wengi walitarajia winga huyo ataungana na mastaa mbalimbali kwenda Uarabuni ambapo wanalipwa fedha nyingi zaidi, lakini mchezaji huyo inaelezwa ameamua kuachana na mpira wa miguu baada ya kufanikiwa kushinda kila taji katika ngazi ya klabu.

# PSG YAMTIMUA KOCHA WAKE



**PARIS,** Ufaransa

KOCHA Christophe Galtier amefukuzwa Paris Saint-Germain baada ya kushinda taji la Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, vyanzo vimeiambia ESPN.

Galtier aliiongoza PSG kutwaa taji la ligi hiyo kwa msimu wa 2022/23 lakini akashindwa kuleta mafanikio kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku klabu hiyo ya Ufaransa ikitolewa na Bayern Munich katika hatua ya 16 bora.

Kwa mujibu wa vyanzo vya ESPN, Mkurugenzi wa Michezo wa PSG, Luis Campos, alifahamisha Galtier alifukuzwa na klabu hiyo Jumanne huku kocha zamani wa Bayern Munich, Julian Nagelsmann, akiendelea na mazungumzo na klabu hiyo.

Vyanzo vya habari viliongeza klabu hiyo pia ilifanya mazungumzo na kocha wa zamani wa Timu ya Taifa ya Hispania na Barcelona, Luis Enrique, lakini sasa wamemfanya Nagelsmann kuwa mlengwa wao mkuu, huku kocha huyo wa Ujerumani akitamani, Thierry Henry ajiunge naye kama msaidizi wake.

Kuna imani inayoongezeka makubaliano yanaweza kufanywa kwa Nagelsmann na Henry kujiunga na mabingwa hao wa Ufaransa.

Galtier alijiunga na PSG msimu uliopita wa joto baada ya kuiongoza Nice kumaliza katika nafasi ya tisa msimu wa 2021-22 na amekuwa na majukumu ya kuinoa Lille na Saint-Etienne.

Lionel Messi na Sergio Ramos pia wataondoka katika klabu hiyo msimu huu wa joto baada ya kumalizika kwa mikataba yao.

Vyanzo viliiambia ESPN mnamo Mei, mwaka huu Neymar pia yuko tayari kuondoka PSG msimu wa joto na klabu iko tayari kumwachia ikiwa watapata ofa inayofaa.

# Di Maria kutimka Juventus

**TURIN,** Italia

WINGA wa kimataifa wa Argentina, Angel Di Maria, ambaye alikuwa anakipiga katika Juventus inayoshiriki Ligi Kuu Italia maarufu Serie A, anatimka ndani ya timu hiyo kama mchezaji huru.

Di Maria alisaini mkataba wa mwaka mmoja ndani na Juventus akitokea kwa mabingwa wa Ufaransa, PSG katika majira ya joto Juni, mwaka jana.

Lakini mchezaji huyo ametangaza kutimka klabuni hapo mara moja kama mchezaji huru na hadi sasa haijafahamika ataenda klabu gani.

Winga huyo amekua katika ubora mkubwa ndani ya Juventus licha ya timu hiyo kutofanya vizuri msimu huu katika michuano ambayo wameshiriki na klabu kadhaa zimeelezwa kumnyemelea mchezaji huyo.

Benfica ambayo ndio timu ya kwanza ya Angel Di Maria kucheza barani Ulaya baada ya kutoka Argentina ina matumaini ya kumrudisha mchezaji huyo katika viunga vya Uwanja wa Estadio da Luz.

Vyanzo mbalimbali pia vinaeleza huenda Di Maria akaungana na magwiji wengine kuelekea Saudia Arabia ambapo mastaa wengi sana wanakimbilia.

Kwani hivi karibuni Karim Benzema ameondoka ndani ya Real Madrid na kutimkia huko hivyo inawezekana na mchezaji huyo akaungana nao huko.





# *Walker hatihati kuikosa fainali*

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER City inatumaini, Kyle Walker, atakuwa fiti kwa ajili ya mechi ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya licha ya kukosa mazoezi hapo juzi.

Walker alikaa nje ya kipindi cha mazoezi kwa sababu ya tatizo la mgongo lililotokea wakati wa fainali ya Kombe la FA Jumamosi iliyopita.

Nyota huyo alitolewa dakika ya mwisho ya ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Manchester United na anakabiliwa na kinyang'anyiro dhidi ya muda ili kuthibitisha yuko fiti kabla ya fainali hiyo ya Ulaya watakayocheza dhidi ya Inter huko mjini Istanbul keshokutwa.

"Alikuwa na tatizo la mgongo," alisema Kocha Pep Guardiola akiwaambia waandishi wa habari juzi.

"Juzi (Jumatatu) hakuwa vizuri. Hatukutaka kuchukua hatari na tutaona kitakachotokea siku zijazo."

Pambano la City dhidi ya Inter litakuwa mechi ya kwanza kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu Egland kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu walipofungwa bao 1-0 na Chelsea mwaka 2021.

Guardiola alipanga kikosi cha kustaajabisha siku hiyo, akianza mechi bila kiungo anayetambulika, uamuzi ambao ulimgharimu wakati, Kai Havertz alipofunga bao pekee kwenye mchezo huo.

## Nonga: Mbeya City tulipoteza umakini

**Na Faustine Feliciane,** MBEYA

KOCHA Msaidizi wa Mbeya City, Paul Nonga, amesema matokeo ya sare ya mabao 3-3 waliyoyapata dhidi ya mabingwa wa Ligi Kuu Bara, Yanga yalitokana na kikosi chake kukosa umakini na utulivu.

Mbeya City ilikuwa inaongoza kwa mabao 3-0, lakini ilipoteza umakini na kuruhusu wageni kusawazisha magoli yao na hivyo kugawana pointi.

"Ni makosa makubwa sana tuliyafanya baada ya kuwa mbele kwa mabao matatu, tulipunguza umakini, lakini hatukuwaheshimu wapinzani wetu, walitumia makosa yetu kutuadhibu, ni matokeo yaliyotuumiza sana.

Kwa sasa hatuna cha zaidi, ni kuangalia mchezo wetu ujao, tushinde ili tuone mwisho wa siku nini kitatokea, tuna mchezo mwingine mgumu wa mwisho," alisema Nonga.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa timu hiyo alisema makosa yaliyofanywa na safu ya ulinzi yalipelekea kushindwa kulinda pointi tatu muhimu walizokuwa wanahitaji wakiwa nyumbani.

Mbeya City sasa ina pointi 31 na wanahitaji kushinda mchezo wao wa mwisho utakaochezwa kesho dhidi ya KMC hatima yao itajulikana baada ya kumalizika michezo yote.

## Ni vita ya Mayele na Ntibazonkiza

INATOKA UKURASA 24

awali kilichokuja Mbeya lakini sasa tumeamua aje kwa ajili ya mchezo wa mwisho," alisema mmoja wa kiongozi wa Yanga.

Mayele hakuwa sehemu ya mipango ya michezo yote miwili ya kumalizia msimu inayochezwa jijini hapa.



Kuwasili kwa Mayele katika mchezo wa kesho kutakoleza vita ya kuwania tuzo ya ufungaji bora ambayo awali alionekana tayari itakwenda kwa Mkongomani huyo bila shaka lakini mabao ya Ntibazonkiza katika mchezo wa juzi yalibadilisha upepo.

Simba iliyoko katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara itamaliza msimu huu kwa kuwakaribisha Coastal Union kutoka jijini Tanga ambayo pia inahitaji ushindi ili kujiweka mahali salama zaidi.

Msimu uliopita Mayele ambaye alikuwa akipewa nafasi kubwa ya kutwa tuzo hiyo, alizidiwa kwa bao moja na aliyekuwa mshambuliaji wa Geita Gold, George Mpole, aliyefikisha idadi ya mabao 17.

# MKUDE AZIGONGANISHA SIMBA SC, SINGIDA BS

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera (Robertinho), anatarajia kukumbana na wakati mgumu wa kumzuia kiungo Jonas Mkude asiondoke katika timu hiyo baada ya kuwapo kwa taarifa za nyota huyo kutakiwa na Singida Big Stars.

Mkataba wa Mkude na Simba unamalizika mwishoni mwa msimu huu na tayari Robertinho amesema kiungo huyo yupo katika mipango yake ya msimu ujao.

**Taarifa za uhakika ziliifikia Nipashe jana zinasema Mkude ameanza mazungumzo na Singida Big Stars lakini waajiri wake wa sasa wakiwa wameonyesha nia ya kumhitaji abakie kikosini.**

"Mkude amekuwa chaguo la kwanza kusalia ndani ya kikosi cha Simba, baada ya kocha (Robertinho) kuwataka viongozi kuhakikisha anabaki licha ya kutokuwa na nafasi kwenye kikosi cha kwanza, kocha ametaka kiungo huyo kutoenda kokote kwa sababu anaimani wachezaji wazawa wanaweza kusaidia timu," kilisema chanzo hicho.

Kiliongeza bado Mkude hajafanya uamuzi wa timu ipi asaini mkataba kwa sababu anataka kujiridhisha anamwaga wino katika timu itakayompa maslahi mazuri.

"Mkude amesema atazingatia maslahi, mpira ni kazi yake, ofa nzuri kati ya timu hizo mbili ndio itaamua hatima yake," kiliongeza chanzo chetu.

Tayari Singida Big Stars yenye makao yake mkoani Singida imeshafanikiwa kuinasa saini ya golikipa namba mbili wa Wekundu wa Msimbazi, Beno Kakolanya.

Singida Big Stars inajipanga kuimarisha kikosi chake ili ifanye vizuri katika Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika watakayoshiriki msimu ujao.




Mshindi wa Jackpot bonus ya SportPesa, Thomas Ikombe, akishikilia mfano wa hundi ya Sh. milioni 10.9 aliyoshinda baada ya kubashiri kwa usahihi baadhi ya mechi za Jackpot. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



## *Fei Toto, Azam kimeeleweka*

INATOKA UKURASA 24

Kimataifa (CAS), ili kudai haki yake ya kuondoka Yanga.

Aliongeza endapo atashindwa kupata haki yake CAS, yuko tayari kuachana na soka lakini si kurejea ndani ya kikosi cha Yanga ambayo inaongoza wa Injinia, Hersi Said, ambaye alidai mara kadhaa kiongozi huyo amemkosea.

"Mimi tatizo langu kubwa ni Rais wa timu (Hersi Said) ndio maana nilipokaa naye chini nilimweleza naomba tumalizane ili kila mmoja aendelee na mambo yake, mimi niendelee na maisha yangu. Kama Hersi akiondoka Yanga hata leo, nipo tayari kurudi Yanga, sina tatizo na klabu wala mashabiki," alisema kiungo huyo katika mahojiano.

Michezo
Alhamisi Juni 8, 2023
Nipashe



Hazard apanga kustaafu UKURASA 21

# Fei Toto, Azam FC kimeeleweka

## ●●● Matajiri hao wamwandalia jezi namba sita, utambulisho wake...

**Na Saada Akida**

KAULI ya mama, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kuutaka uongozi wa Yanga kumalizana na kiungo, Feisal Salum 'Fei Toto' imefanyiwa kazi kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara kukubali kumwachia Mzanzibari huyo na sasa anatarajiwa kutambuliwa rasmi na Azam FC, imefahamika.

**Rais Samia aliwataka Yanga kuhakikisha wanamaliza mgogoro wa Fei Toto ambaye aliamua kuvunja mkataba na klabu hiyo kutokana na kushindwa kulipwa maslahi bora.**

Taarifa zilizopatikana jijini jana zinasema Fei Toto alishakamilisha mazungumzo ya kujiunga na Azam FC kwa mkataba wa miaka miwili na utaanzia msimu wa 2023/2024.

Chanzo chetu kilisema mabosi wa Yanga walikuwa na kikao 'kirefu' kuanzia juzi usiku hadi jana mchana chenye lengo la kufikia uamuzi kuhusiana na mchezaji huyo lakini mazungumzo hayakuwa na mafanikio kwa sababu tayari Fei Toto alikuwa ameshafikia uamuzi wa kutafuta changamoto mpya.

Licha ya Azam kufanya siri mchakato wa usajili wa kiungo huyo, taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo ya Chamazi zilisema kila kitu kilikuwa kimekamilika, na hakuna kikao ambacho kingebadilisha uamuzi wa klabu gani ataitumikia.

Taarifa zilisema nyota huyo amesajiliwa kwa dau la Sh. milioni 350 na atalipwa mshahara wa Sh. milioni 15 kwa mwezi, akipewa nyumba pamoja na gari la kifahari.

"Viongozi wa Yanga walikuwa na kikao kizito na kiungo huyo ili kuweka sawa mambo yao, kilichukuwa muda mrefu lakini hakijabadilisha uamuzi wa Fei Toto, haikuwa rahisi kwa viongozi wote kukubali kirahisi, mjadala ulikuwa kama umezaliwa upya," kilisema chanzo hicho.

Kiliongeza msimamo wa Fei Toto uliwachanganya baadhi ya viongozi ambao walikuwa tayari Yanga itoe kiasi chochote cha fedha ili kufanikisha kiungo huyo anabakia klabuni hapo.

"Azam FC wanasubiri tu Yanga wamalize kikao naye, 'Fei Toto' ni mchezaji wa Azam FC tayari na wameshaandaa jezi yake ambayo ataivaa katika msimu ujao," kilisema chanzo hicho.

Kiliongeza nyota huyo alitarajiwa kuondoka Dar es Salaam jana na kuelekea Zanzibar kuendelea na mapumziko yake kabla ya kurudi jijini ili kutambulishwa.

Desemba, mwaka jana Fei Toto, ambaye pia ni kiungo wa Timu ya Taifa (Taifa Stars) ali, aliwasilisha barua ya kuvunja mkataba wake na Yanga na kuilipa klabu hiyo Sh. milioni 112 kama vipengele vya mkataba aliokuwa nao vinavyomtaka.

Yanga ilikataa uamuzi huo, na iliamua kufungua malalamiko katika Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), na Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya shirikisho hilo iliamua mchezaji huyo ni mali ya mabingwa hao na anatakiwa kurejea klabuni ili kumaliza tofauti zao.

Hivi karibuni katika mahojiano na kituo kimoja cha redio hapa nchini, kiungo huyo alisisitiza hayuko tayari kurejea Yanga na tayari ameshawasilisha fedha nusu katika Mahakama ya Usuluhishi ya

INAENDELEA UKURASA 23




Kombe ambalo wanatarajiwa kukabidhiwa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2022/2023, Yanga. Kombe hilo lilitambulishwa rasmi jana na wadhamini wakuu wa ligi, Benki ya NBC na Shirikisho la Soka Nchini (TFF). **PICHA: TFF**

# Ni vita ya Mayele na Ntibazonkiza

**Na Faustine Feliciane,** MBEYA

IKIWA imebakia mechi moja ili kumaliza msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara mwaka 2022/2023, kiungo mshambuliaji wa Simba, Saido Ntibazonkiza ameamsha vita mpya ya kuwania Kiatu cha Dhahabu dhidi ya straika wa Yanga, Fiston Mayele.

Mkongomani Mayele ambaye amefunga mabao 16 alikuwa hana presha yoyote ya kutwaa tuzo hiyo mpaka 'alipoamshwa' na Ntibazonkiza aliyefikisha magoli 15, baada ya juzi kupachika mabao matano Simba ikiibuka na ushinda wa 6-1 dhidi ya Polisi Tanzania.

Mabosi wa Yanga walimwacha Mayele lakini klabu hiyo imelazimika kumpandisha ndege jana mchana kuja jijini hapa ili kuuwahi mchezo wa mwisho dhidi ya Tanzania Prisons.

Mayele hakuwa sehemu ya mipango ya kikosi kilichowasili jijini hapa Jumatatu usiku kwa ajili ya kucheza dhidi ya Mbeya City, lakini kasi ya Ntibazonkiza imewafanya Yanga kumjumuisha katika mchezo wa kesho.

Awali ilisemekana Mayele alikuwa anajiandaa kwenda kwao Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), ili kujiunga na timu ya taifa.

Taarifa kutoka Yanga zinasema Mayele alitegemea kuungana na timu jana mchana na kesho atakuwa sehemu ya kikosi kitakachoumana na Tanzania Prisons.

"Mayele anasafiri leo (jana) mchana, hakuwepo katika kikosi cha



INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >